Huduma Yenye Nguvu

Denzil R. Miller

Huduma Yenye Nguvu

Uhudumu Katika
Nguvu Na
Upako Wa
Roho Mtakatifu

Denzil R. Miller

Imenakiliwa

Maandiko yote ya Biblia yamenukuliwa kutoka kwenye THE HOLY BIBLE IN KISWAHILI, Union Version, ©United Bible Societies, 1952.

Hairuhusiwi kuchapishwa wala kunakiliwa kwa aina yoyote ile bila kibali cha kimaandishi kutoka kwa mtunzi kabla ya kuchapisha. Haki zote zimehifadhiwa.

©2011 Denzil Ray Miller
Springfield, MO, USA

Translated from the author's book
POWER ENCOUNTER: Ministering in the Power and Anointing of the Holy Spirit

Kiswahili Version

Yaliyomo

Utangulizi 1

KIFUNGU I: Kufahamu Huduma yenye Nguvu

Sura ya 1: Huduma yenye Nguvu Iamefafanuliwa 7
Sura ya 2: Huduma yenye Nguvu za Imeelezwa 15
Sura ya 3: Huduma yenye Nguvu na Ufalme wa Mungu 23
Sura ya 4: Huduma yenye Nguvu na Kuhubiri Injili 31

KIFUNGU II: Maandalizi ya Huduma yenye Nguvu

Sura ya 5: Mambo Muhimu na Maandalizi ya Huduma yenye Nguvu 41
Sura ya 6: Roho Mtakatifu na Huduma yenye Nguvu 53
Sura ya 7: Kuongozwa na Roho 65
Sura ya 8: Silaha za Vita vyetu 75

KIFUNGU III: Utendaji wa Huduma yenye Nguvu

Sura ya 9: Jinsi ya Kuponya Wagonjwa 87
Sura ya 10: Jinsi ya Kutoa Pepo wachafu 97
Sura ya 11: Jinsi ya Kupambana na Huwashinda Pepo Watawala wa " Maeneo" 107
Sura ya 12: Jinsi ya Kuomba na watu Wajazwe Roho Mtakatifu 115

Appendix 1 125
Appendix 2 127
Bibliography 129

— Huduma Yenye Nguvu —

Utangulizi

Katika miaka ya karibuni kumekuwepo na wito kutoka kwa viongozi wa makanisa na uongozi wa Ngazi za utawala wa Vyuo vya Biblia katika bara zima la Afrika wakihitaji kupatikane mafundisho yanayohusu masuala ya huduma za wachungaji wa Kiafrika, wainjilisti na viongozi wa makanisa. Mafundisho yanayohusu huduma yenye Nguvu za Kiroho. Wengi wanauliza, "Tunawezaje kuhudumu katika Nguvu na upako wa Roho Mtakatifu? Tunawezaje kuombea wagonjwa na kushuhudia uponyaji wao? Tunawezaje kuwaongoza wakristo waliomo makanisani mwetu katika ubatizo wa Roho Mtakatifu?"

Kitabu hiki kimeandikwa ili kujibu maswali hayo kwa njia tatu tofauti: Kwanza, kitabu hiki kitaweka msingi wa Biblia kuhusu huduma yenye Nguvu za Roho Mtakatifu. Ni katika msingi huu imara tu ambapo huduma ya kudumu ya Roho Mtakatifu inaweza kujengwa. Haya yatajadiliwa katika kifungu cha kwanza cha kitabu hiki kinachohusu, "Kuielewa huduma yenye Nguvu." Pili, kitabu hiki kitaeleza pia matayarisho binafsi ambayo yatahitajika kwa mtu atakayehitaji kuhudumu katika nguvu za Roho Mtakatifu. Je anahitajika awe mtu wa namna gani? Je ni mambo gani anahitaji ayapitie katika maisha yake kabla ya kuingia katika huduma kama hii? Masuala haya yameelezwa katika Kifungu cha Pili cha kitabu hiki, kinachozungumzia kuhusu "Matayarisho ya Huduma yenye Nguvu." Hatimaye tunapenda kutoa ushauri jinsi mtu anavyoweza kuitenda Huduma yenye Nguvu. Kifungu cha Tatu "Jinsi ya kuitenda Huduma yenye Nguvu." Tunategemea kwamba kitabu hiki kitafaa kutoa mafundisho bayana kwa wale wanaopenda kutii agizo kuu la Bwana Yesu, kuihubiri injili kwa ishara zitakazofuatana (Marko 16:15-20).

Mapendekezo kwa Ajili ya Kusoma

Endapo mwanafunzi atafaidika na mafunzo ya kozi hii, ni hakika kwamba haitatokana na usomaji wa kitabu kinadharia pekee. Ni kweli kwamba usomaji wa kitabu hiki ni muhimu lakini, ili kuwepo na mafanikio mazuri ni vema kuchanganya nadharia na kujifunza kimatendo. Kumbuka, lengo letu si kufaulu

mitihani tu, bali ni kuona kwamba wanafunzi wetu wanafahamu vema kuhudumu katika Nguvu na Upako wa Roho Mtakatifu na ishara zikifuata huduma hiyo.

Mafunzo ya Kitaaluma

Baada ya kuyashika haya yote tunatoa mapendekezo yafuatayo kuhusu kozi hii: Kwanza, mafundisho ya kila somo ni vema baada ya kusoma yafanyiwe kazi katika maisha ya kila mwanafunzi. Mwalimu anaweza kufanikisha jambo hili kwa kufundisha vema pamoja na kuwapa wanafunzi vifungu vya kusoma, majadiliano ya darasani, mitihani ya kuandika na ile ya kuwauliza wanafunzi maswali darasani n.k. Katika kitabu hiki tumeuliza maswali mengi ili kumsaidia mwanafunzi afikirie sana masuala yote yanayojadiliwa. Utaona maswali hayo na alama kama, S 1, S 2, n.k. Maswali hayo yaliyomo katika vifungu vyenye kivuli chepesi, yanaweza kutumika katika darasa kama maswali ya awali ya kuanzishia mijadala.

Mafunzo ya Kiutendaji

Kama nyongeza juu ya mafunzo ya darasani, mafunzo ya kiutendaji ni muhimu. Hili laweza kufanyika kwa njia kadha. Mwalimu anaweza kuchukua uzito kuamua ni njia gani atatumia kuwafundisha wanafunzi kimatendo. (1) Mwalimu anaweza kuamua kila juma kuwa na kipindi katika maabara ya mafunzo, na (2) anaweza pia kuwatia moyo wanafunzi kujihusisha katika utendaji halisi wa huduma hii katika maeneo mbalimbali wanapokwenda kuhudumu. Tutaeleza zaidi kuhusu jambo hili.

“Maabara ya Mafunzo”

Kama ilivyopendekezwa awali, njia mojawapo ambayo mwalimu anaweza kuwasaidia wanafunzi jinsi ya kushiriki na Roho Mtakatifu katika kuitenda huduma yenye nguvu ni kwa njia ya Maabara ya mafunzo kila juma. Kila juma wanafunzi wapangiwe kukutana pamoja na mwalimu ili kuabudu, kuomba na kuamini Mungu apate kutembea katikati yao. Mwalimu awatie moyo wanafunzi kumsikiliza Roho Mtakatifu, kuombeana endapo yupo anayeumwa katikati yao, na kumruhusu Roho wa Mungu apate kugawa vipawa katika maisha yao. Ni vema mwalimu asiwe kama “mtaalam” katika mikutano ya namna hii bali naye achangamane katika kundi la kujifunza. Anaweza akatamka hivi kwa wanafunzi, “Tumekuja kujifunza pamoja.” Kwa ruhusa ya uongozi wa chuo mikutano kama hii yaweza hatimaye kujumuisha wanafunzi wote katika chuo ili kuendeleza mikutano ya mchana katika “kupokea Roho Mtakatifu” au “Ibada za uponyaji.”

Katika mikutano kama hii walimu na wanafunzi wanaweza kufanyia mazoezi mambo ambayo wamejifunza madarasani. Kwa jinsi Mungu atakavyotembea na kubariki ibada hizo, ndivyo ambavyo wanafunzi wataendelea kutiwa moyo.

Mazoezi kwa Vitendo

Namna ya pili ambayo mwalimu anaweza kuwasaidia wanafunzi kuyafahamu vema mafunzo wanayojifunza darasani ni kuyageuza mafunzo hayo katika matendo. Jambo hili linaweza kufanyika katika njia mbili. Njia ya kwanza ni kwa mazoezi. Mwalimu anaweza kuwatuma wanafunzi wawili wawili ili kwenda kuifanya huduma katika Nguvu za Roho Mtakatifu. Baada ya huduma hiyo ambayo itahusu kuponya wagonjwa, kutoa pepo, au kuombea wakristo waliookoka kujazwa na Roho Mtakatifu, wanafunzi watatakiwa kurudi ili kutoa taarifa kwa mwalimu wa darasa. Majadiliano yatafuata ambapo mwalimu atawatia nguvu, atawasahihisha na kuwaelekeza vema wanafunzi. Utatambua kwamba hii ndiyo njia ambayo Yesu alitumia katika kuwafundisha wale sabini, Luka 10:1-24.

Njia nyingine ambayo mwalimu anaweza kuwaongoza wanafunzi katika mazoezi ya huduma ni kwa njia ya kwenda nao katika huduma. Anaweza kuligawanya darasa katika makundi na kwenda na kundi moja kila wakati. Pia mwalimu anaweza kupanga mipango na makanisa ya jirani kuhusu safari hizo za huduma katika makanisa hayo. Siku zilizopangwa kwa huduma zifikapo mwalimu na wanafunzi wanaweza kwenda kufanya huduma, wakiwahudumia watu katika mahitaji yao.

Mwalimu na darasa pia yawabudi kutumia nafasi zipatikanapo kutoa huduma katika chuo chenyewe. Je kuna wanafunzi wanaohitaji uponyaji? Je kuna wanafunzi wanaohitaji kujazwa Roho Mtakatifu? Kama wapo basi huduma ya nguvu za Roho Mtakatifu yaweza kufanyika katika mamlaka ya Jina la Yesu na nguvu za Roho Mtakatifu.

— Kifungu I —

Kuielewa Huduma Yenye Nguvu

— Sura Ya Kwanza —

Huduma Yenye Nguvu Imefafanuliwa

HITAJI LA HUDUMA YENYE NGUVU

Wakati Yesu alipopaa mbinguni hakuacha kanisa nyonge. Alitupa nguvu yote tunayohitaji kumaliza kazi. Kabla hajarudi kwa Baba yake aliahidi kulipatia kanisa nguvu ya kuihubiri injili duniani kote (Mdo 1:8). Aliitimiza ahadi hiyo siku ya Pentekoste (Mdo 2). Kanisa la kwanza lilihudumu katika nguvu kwa mafanikio makubwa. Ni tamko la kitabu hiki kwamba kanisa leo bado linahitaji nguvu ile ile kama litahitaji kufanikisha kazi ya kuwahubiri watu wote wa dunia hii. Kuna sababu kadhaa zinazolifanya kanisa leo kuwa na huduma iliyojaa nguvu za Mungu. Nitazitaja nne:

Tumo Vitani

Biblia inafundisha wazi kwamba sisi tunaojiita wana wa Mungu tumo katika vita kubwa ya kiroho. Vita hii tunayopambana ni dhidi ya shetani na wafuasi wake. Katika Mathayo 13:39 Yesu anatuambia kwamba "adui yetu ... ni shetani." (Pia angalia Luka 10:19). Paulo anazungumza kuhusu mapambano ya kiroho

> Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama, bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho (Efe 6:12).

Paulo anaendelea kusema kwamba lazima tutumie nguvu za silaha za kiroho ili kupigana vita hii ya kiroho:

> Maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome" (2Kor 10:4).

Ngome ambazo mtume ananena habari zake ni ngome za kiroho zilizowekwa na adui. Kwa hiyo kwanza ya yote lazima tuwe na huduma yenye nguvu kwa sababu tumo vitani.

Adui anazo Nguvu.

Sababu ya pili inayotufanya tuhitaji huduma yenye nguvu ni kwamba adui yetu shetani, ni adui mwenye nguvu. Katika Luka 10:19 Yesu anasema kwamba "Nguvu yote ya adui." Katika dunia nzima amekusanya jeshi la pepo waliojitoa kupinga uenezaji wa injili. Kama tutahitaji kumshinda shetani ni lazima tupambane na nguvu zake kwa nguvu iliyo kubwa zaidi. Tunaweza tu kulitimiza hili kwa huduma inayotembea katika nguvu za Roho Mtakatifu.

Kazi ni Kubwa

Sababu nyingine inayotufanya tuhitaji huduma yenye nguvu ni kwamba kazi tuliyonayo ni kubwa kiasi kwamba huduma ya nguvu ni njia pekee ambayo tunaweza kuimaliza kazi hii. Kazi hiyo niisemayo ni ile ya kulitimiza agizo la Bwana Yesu kuihubiri injili ulimwenguni pote kuwa ushuhuda kwa mataifa yote kabla hajaja tena (Mt 24:14). Leo kumebakia watu wanaozidi 2.5 bilioni katika dunia ambao hawajapata ushuhuda wa kutosha wa injili. Je tutawafikiaje watu wengi namna hii. wengi wao wakiishi katika nchi zinazotawala uhuru wa dini na kupinga kabisa ueneaji wa ukristo? Yesu alituahidi kwamba atatupatia nguvu za kumaliza kazi hii:

> Lakini mtapokea nguvu, akisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi" (Mdo 1:8).

Pia alisema kwamba endapo tutakwenda na kuihubiri injili, yeye atalithibitisha neno lake kwa ishara za nguvu zitakazofuatana nalo. "Akawaambia, enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri injili kwa kila kiumbe ... Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: Kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa nao watapata afya" (Mk 16:15-18). Kutokana na Yesu, njia ya kueneza ufalme wake duniani ni kwa nguvu, hii ni, katika nguvu za Roho Mtakatifu. Silikiza maneno yake:

> Tangu siku za Yohana Mbatizaji hata sasa ufalme wa mbinguni hupatikana kwa nguvu, nao wenye nguvu wauteka" (Mt 11:12).

Huduma yenye Nguvu Inafanya Kazi

Sababu ya mwisho inayotufanya tuhusike na huduma yenye nguvu ni kwa sababu huduma ya namna hiyo inafanya kazi. Mafanikia makubwa ya kanisa la mitume yanaweza kuwa ni kwa sababu sehemu kubwa ya huduma hiyo ilifanyika katika nguvu za kimuujiza za Roho Mtakatifu -- na ishara zilizofuatana.

Lile lililofanyika katika kanisa la mitume hakika lawezekana pia kufanyika leo. Katika kitabu cha *Power Evangelism* au Uinjilisti wenye nguvu , John Wimber anaandika, "Katika mapana ya dunia nzima asilimia 70 ya ukuaji wa makanisa unafanyika katika vikundi vya Kipentekoste na kikarismatiki"[1] (charismatic). Vikundi hivi ndivyo vilevile vinavyoamini na kutegemea nguvu za Roho Mtakatifu katikati yao. Katika kitabu hicho hicho mwandishi anamnukuu C. Peter Wagner akisema,

> Kuna uhusiano wa karibu sana kati ya ukuaji wa makanisa leo na huduma ya uponyaji ... Injili inapopenyeza eneo, endapo hatutaenda na ufahamu wa matumizi ya nguvu za miujiza za Roho Mtakatifu, kazi yetu haitakuwa na maendeleo ya kutosha…[2]

Kama tunahitaji kuona mafanukio ya huduma ya mitume katika bidii yetu ya uinjilisti, ni muhimu kuiga njia ambazo mitume walizitumia. Lazima tutumie nguvu zile zile walizokuwa nazo. Lazima tujifunze kama walivyofanya, jinsi ya kutembea na kuhudumu katika nguvu za Roho Mtakatifu.

---

[1]John Wimber, *Power Evangelism,* (San Francisco: Harper and Row Publishers, 1986) uk. 31.

[2]Ibid, uk. 39.

UFAFANUZI WA MANENO

Ili kuwa na ufahamu wa huduma yenye nguvu ni nini, tunahitaji kuifafanua. Pia tunahitaji kufafanua maneno yanayohusiana na huduma ya kimiujiza.

Mapambano Dhidi ya Nguvu za Giza

Kuna njia mbili ambazo tunaweza kufafanua maana ya mapambano dhidi ya nguvu za giza: tunaweza kufafanua kwa ufinyu au kwa mapana zaidi. Tukifafanua kwa ufinyu, mapambano dhidi ya nguvu za giza yanahusu hasa kupambana na nguvu za giza (mapepo) katika nguvu za Jina la Yesu. Wimber anamnukuu Allen Tippett ifuatavyo: "Pambano dhidi ya nguvu za giza) ni pambano la ufalme wa Mungu na ufalme wa giza."[3] Mtaalamu wa mambo ya utume C. Peter Wagner, kama alivyonukuliwa na Opal Reddin katika kitabu, Power Encounter, A Pentecostal perspective, (muangalio wa Kipentekoste kuhusu mapambano dhidi ya nguvu za giza), kitabu hicho kinatoa ufafanuzi unaofanana: "Mapambano dhidi ya nguvu za giza ni udhihirisho wa wazi kabisa kwamba Yesu Kristo ni mwenye nguvu zaidi kuliko miungu na mizimu inayoabudiwa na kuogopwa na mataifa ya watu."[4] Ingawa hatupingani na ufafanuzi huu, tunaona kwamba ni ufafanuzi mfinyu mno kwa somo hili.

Ufafanuzi kwa upana zaidi, mapambano dhidi ya nguvu za giza ni udhihirisho wa nguvu za Mungu zikitumika kuendeleza ufalme wake duniani. John Wimber anafafanua kwa mapana zaidi: "Kila utawala wa nguvu unapolazimika ushindwe katika ushindani ili injili iweze kuaminiwa ndilo chimbuko la mapambano dhidi ya nguvu za ibilisi. . .. Kufukuzwa kwa mapepo katika mapambano dhidi ya nguvu za giza ni sehemu tu ya mapambano ambapo nguvu za shetani zinajidhihirisha katika hali ya mapepo … Wakati ufalme wa Mungu unakutana ana kwa ana na ufalme wa dinia hii (wakati Yesu anakutana na shetani), kunakuwa na pambano (pambano dhidi ya nguvu za giza)."[5]

---

[3]Ibid uk.16 (imenukuliwa kutoka kwa Allen Tipett, *People movements* in Southeast Polynesia).

[4]Opal Reddin, ed., *Power Encounter, A Pentecostal Perspective* (Springfield, MO: Central Bible College, 1989) uk. 4.

[5]Wimber, uk. 16

Haduma ya Kuihubiri Kweli

Haduma ya kuihubiri kweli ni mahubiri ya injili ya Yesu Kristo ama kabla au baada ya mapambano dhidi ya nguvu za giza. Wakati mapambano dhidi ya nguvu za giza ni mapambano dhidi ya nguvu za shetani, huduma ya kuihubiri kweli ni mapambano dhidi ya mafundisho ya uongo ya dini au vyama vinavyowashikilia watu katika utumwa. Ni muhimu 'kweli' neno la Mungu nyakati zote lifuatane na mapambano dhidi ya nguvu za giza. Kichwa cha somo hili kitazungumzwa kwa urefu katika sura ya 4, "Mapambano dhidi ya nguvu za giza na kuihubiri injili."

Huduma yenye Nguvu

Katika kitabu hiki kizima tutatumia maneno, "Huduma yenye Nguvu." Ni muhimu basi tufafanue ni jinsi gani tutatumia maneno haya. Huduma yenye nguvu, kama tutakavyotumia katika somo hili, ni huduma yoyote ya kimiujiza yenye chimbuko katika Roho wa Mungu, inapotumika kuendeleza ufalme wa Mungu duniani. Inahusisha ishara, maajabu, uponyaji, na kutoa pepo, huduma ya karama za Roho, au udhihirisho wowote wa nguvu za Mungu kwa nia ya kuendeleza ufalme wake.

Nguvu za Uponyaji

Kwa makusudi yetu ya sasa tutapanga uponyaji katika makundi mawili. Kundi la kwanza tutaliita *uponyaji wa agano*. Uponyaji wa agano ni uponyaji kama ulivyotolewa katika kazi ya Kristo msalabani (Isa. 53:4-5). Huu ndio uponyaji alioutoa kwa watu wote wenye agano na Mungu; hii inamaanisha. Wale wote waliomfanya Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wao. Katika Mathayo 15:25 Yesu analiita jambo hili "chakula cha watoto." Pamoja na wokovu, ni sehemu ya mahitaji ya ajabu ya watoto ambayo kristo aliyatenda msalabani.

Kundi la pili la uponyaji ni *uponyaji wa nguvu.* Maana yake ni uponyaji ambao unatumika kama udhihirisho wa uwepo wa ufalme wa Mungu. Hapa mara nyingi Mungu huponya hata wale wasiomwamini. Namna hii ya uponyaji inatumika kwa kuambatana na mahubiri ya injili ili kuthibitisha kweli ya yale yanayohubiriwa. Mara nyingi uponyaji wa namna hii umeitwa "ishara na miujiza" katika vitabu vya injili na Matendo ya mitume.

Huduma ya Injili

Huduma ya injili yenye nguvu ni matokeo tunapochanganya mapambano dhidi ya nguvu za giza na huduma ya kuihubiri kweli au neno la Mungu. Naweza

kuelekeza kimchoro katika chati ifuatayo:

Mapambano dhidi ya nguvu za giza + Huduma ya kuihubiri kweli = *Huduma ya injili yenye nguvu*

Kutokana na John Wimber, "(Huduma ya injii yenye nguvu) ni maelezo ya injili (ambayo) huja kwa udhihirisho wa nguvu za Mungu kwa njia za ishara na maajabu….. Huduma ya injili yenye nguvu ni uinjiisti ambao unafuatiwa na uthibitisho wa kimiujiwa wa uwepo wa Mungu."[6] Huduma ya injili yenye nguvu hufanyika wakati kuna udhihirisho wa nguvu za kimiujiza za Mungu JUMLISHA mahubiri ya injili yaliyo wazi na yanayozikamata dhamiri za watu na kuwafanya waikubali injili.

Ishara na Maajabu

Maneno haya yanatokea mara kwa mara katika Agano Jipya "Ishara na miujiza." Katika Matendo ya mitume kwanza maneno haya yanaonekana katika sura ya2, msitari wa 22. Hapa maneno haya yanaelezea kuhusu huduma ya Yesu. Sehemu ya pili yanatajwa katika sura ya 2, msitari wa 43. Hapa iliyotendeka kuhusiana na huduma ya kanisa iliyotendeka mara baada ya Siku ya Pentekoste: Kila mtu akaingiwa na hofu; maajabu mengi na ishara zikafanywa na mitume.

Angalia: Uwe mwangalifu kusoma mistari ifuatayo inayozungumzia "ishara na ajabu" katika uinjilisti wa Agano Jipya: Matendo 4:29-30; 5:12; 6:8; 14:3; Ru 15;19; Ebr 2:3,4.

Katika maandiko maneno "ishara na maajabu" mara nyingi hutumika pamoja, ili kuonyesha jinsi mambo hayo mawili yanavyokwenda pamoja. Ishara ni kitu kinachoonyesha kwenye kitu kingine. "Ishara" katika Agano Jipya (Kigriki: semeion) ni matokeo ya miujiza yanayoonyesha kwamba ufalme wa Mungu umekuja na kwamba ujumbe wa injili ni kweli. Katika

[6]Wimber, uk. 35

Marko 16:15 Yesu anafundisha wazi kwamba atayathibitisha mahubiri ya injili kwa ishara zitakazofuatana nayo. Na katika msitari wa 20 ishara hizi zinasemekana kuthibitisha ujumbe wa injili kama ulivyohubiriwa na mitume. Tunapoendelea kuhubiri injili, sisi pia tunaweza kutegemea Mungu kuthibitisha ujumbe kwa ishara zitakazofuatia.

Neno "ajabu" (Kigriki: tera) linazungumzia kuhusu muujiza wa ajabu wa Mungu ambao unamfanya mtazamaji kushangaa, kama wakati Yesu alipomponya kijana aliyepagawa na mapepo katika Luka 9:43:

> Wote wakashangaa, wakiuona ukuu wa Mungu (na) walikuwa wakiyastaajabia mambo yote aliyoyafanya.

Katika Matendo ya mitume hii "ajabu" ya watu ilihusisha mshangao mkubwa (Mdo 2:7; 3:10); wakaingiwa hofu (Mdo 2:43); wakashangaa wote (Mdo 2:12); wote alimtukuza Mungu (Mdo 4:21); hofu nyingi (Mdo 5:5,11); ikawa furaha kubwa (Mdo 8:8); akashangaa (Mdo 8:13) hata imani iokoayo (Mdo 9:42 na 1Kor 2:4-5).

Daktari Jesse K. Moon akizungumza kuhusu makusudi ya ishara na maajabu katika Agano Jipya:

1. Kuhakikisha Umasihi wa Kristo na kuwafanya watu wamwamini (Mdo 2:22; Ebr 2:4);
2. Kuwavuta watu wasikilize injili;
3. Kama ushahidi kwamba Kristo yu hai (amefufuka) ni Bwana wa Kanisa;
4. Kuthibitisha neno lililohubiriwa (Mdo 4:29, 30; 14:3; Rum 15:19; Ebr 2:3, 4);
5. Kutambulisha waumini na dini ya kweli (2Kor12:12; Mk 16:15-18);
6. Kukutana na mahitaji ya wanadamu, na
7. Kuendeleza ufalme wa Mungu duniani (Mdo 5:12-14; 8:5-13).[7]

[7]Reddin, uk. 238.

Kwa sababu hizo zote yatubidi tuombe sana ili ishara na maajabu viwe sehemu katika huduma zetu katika kuihubiri injili ya Kristo leo kama ilivyokuwa katika siku za mitume.

MWISHO

Mahubri yenye upako yakifuatiwa na ishara na maajabu ni ufunguo muhimu wa kufikia ulimwengu na injili ya Kristo. Lazima tufike katika ufahamu timilifu kuelewa ni nini maana ya kuhudumu katika nguvu na karama za Roho Mtakatifu. Tukianza kuwa na ufahamu huo tutaanza kuona matokeo ya Agano Jipya katika huduma zetu za uinjilisti. Hili ndilo kusudi la kitabu hiki. Ili upate kujaa mambo haya, unaposoma na kujifunza masomo yafuatayo, ninaomba kwamba kwa njia ya imani na kujiachilia kwa Roho Mtakatifu, wewe pia utaanza kuhudumu katika nguvu za kiumitume na matokeo ya huduma zilezile za Agano Jipya.

— Sura Ya Pili —

Huduma Yenye Nguvu Imeelezwa

UTANGULIZI

Kuna maelezo mbalimbali ya mapambano dhidi ya nguvu za giza katika maandiko. Tumechagua mifano michache kutoka kote katika Agano la Kale na Agano Jipya kwa ajili ya somo hili.

HUDUMA YENYE NGUVU ILIVYODHIHIRISHWA
KATIKA AGANO LA KALE

Katika agano la kale tunaona mifano mizuri ya huduma yenye nguvu. Tumechagua mifano miwili ili kueleza hoja yetu.

Musa Anapambana na "miungu" ya Misri

Soma habari ya jinsi Musa alivyoshindana na miungu ya Misri katika Kutoka 7-13. Fahamu jinsi Mungu alivyomwambia Musa kwamba mapambano hayo yote kati yake na Farao ni mapambano kati ya Mungu na "miungu yote ya Misri" (Kut 12:12). Kutokana na maandiko ya Paulo tunajifunza ya kwamba "miungu ya Misri" ilikuwa hasa ni majeshi ya pepo wabaya (1Kor 10:20). Katika kitabu chake, ishara, maajabu, na ufalme wa Mungu, Don Williams anasema, "Kutoka 5-12 inazungumzia matendo makuu ya Mungu, ishara na maajabu yanayoanguka kama ukungu wa mabomu ya vita yaliyoanguka katika mji wa London.[8]

[8]London Blitz ilikuwa ni mapigo ya mabomu juu ya mji wa London, uingereza yaliyoangushwa na ndege za vita za kijerumani katika Vita Kuu ya pili.

Hapa tunaona huduma yenye nguvu ikitendeka jambo ambalo ni udhihirisho wa wazi kabisa kwamba Mungu ana nguvu zaidi kuliko miungu ya Misri. Katika kila pigo, Mungu alikuwa akipambana na mmoja au zaidi ya miungu ya misri.[9] Kutokana na Fred Haltom, Mungu alipeleka mapigo mbalimbali ili kupambana na kila mmoja katika miungu ya Misri:

> Alipeleka mapigo ya damu, vyura, na chawa kama mapigo kwa *Nu*, mungu wa mto Naili; *Hekt*, mungu mke wa nchi ile; na *Geb*, mungu wa dunia. Alipeleka mapigo ya Nzi, magonjwa juu ya wanyama, majipu juu ya wanadamu kama mashambulizi juu ya Scarob, mungu wa wadudu; *Apis*, mungu ng'ombe; na *Thoth*, mungu wa ufahamu na elimu ya uganga. Alipeleka upepo, nzige na giza kama mashambulizi juu ya *Ntu*, mungu wa anga; *Anubis* mlinzi wa mashamba; na *Ra*, mungu wa jua. Na hatimaye vifo vya wazaliwa wa kwanza wa Misri kama shambulizi kwa *Farao* mwenyewe, mungu-mfalme.[10]

Kutokana na hayo ya juu, tunaweza kujumuisha kuwa miungu ya Misri ilikuwa falme na majeshi ya pepo wabaya vikishikilia watu katika utumwa wa kiroho. Kutoka kwa wana wa Israel katika utumwa wa Misri ilikuwa ni zaidi ya ukombozi wa kimwili wa watu wa Mungu. Ilikuwa pia ukombozi wa kiroho kutoka katika utawala wa nguvu za giza,kwenda katika uhuru wa kumwabudu YEHOVA peke yake.

Eliya Anashindana na Manabii wa Baali juu ya Mlima Karmeli

Katika wafalme wa kwanza 18:20-46 soma habari ya kusisimua kuhusu mapambano dhidi ya nguvu za giza kati ya Eliya nabii na Baali, mungu wa Kanani aliyevuviwa na nguvu za mapepo. Merril C. Unger ameandika, "Dalili ya kuwepo kwa mapepo katika Agano la Kale, kama sio kupagawa, ilikuwa ni

---

[9]Don William, sign, wonders and the Kingdom of God (Ann Arbor, MI: Servant Publications, 1989) uk. 82.

[10]Fred Haltom, Old Testament Encounters, "Power Encounter, A Pentecontal Perspective, uk. 103.

namna ya ibada za kipagani za makuhani wa Baali."[11] Kumbuka Eliya hakuwa tu anapambana na dini ya kuabudu miungu ya Baali, bali alipambana na mapepo yaliyokuwa nyuma ya dini hiyo, yakiipa nguvu zake.

Tambua kwamba mapambano hayo yalihusisha vyote mapambano dhidi ya nguvu za giza pamoja na huduma kwa njia ya kuihubiri kweli (1Wafalme 18:21). Katika mapambano haya YEHOVA, kupeleka moto kutoka mbinguni kuyalamba maji ilionyesha ukuu wake zaidi kuliko Baali. Wakati huo huo msitari wa 21, Eliya anawahubiri watu na kuwahamasisha kumfuata Mungu wa kweli aishiye.

Mapambano haya dhidi ya nguvu za giza yalisaidia kuionyesha Israeli na wapagani ambao Israeli walikutana nao kwamba YEHOVA ni Mungu pekee astahiliye kutumikiwa na kuabudiwa.

HUDUMA YENYE NGUVU ILIVYODHIHIRISHWA KATIKA HUDUMA YA YESU

Huduma ya Yesu ilijaa nguvu. Kupitia udhihirisho huo wa nguvu Yesu alionyesha hakika kwamba alikuwa Ndiye "mpakwa mafuta" aliyetumwa na Mungu. Pia alionyesha kuwa ufalme wa Mungu ulikuwa umekuja kuupindua ufalme wa shetani (Lk 11:20). Tunaona huduma yenye nguvu ikiwa imedhihirishwa kwa njia nne katika huduma ya Yesu: (1) katika makusudi ya huduma yeke, (2) katika utendaji wa huduma yake, (3) katika mafundisho ya huduma yake, na (4) katika kukabidhi huduma yake kwa wale waliomfuatia. Sasa hebu tuangalie katika kila njia mojawapo.

Katika Kusudi la Huduma Yake

Biblia inanena waziwazi kwamba moja ya makusudi ya kuja kwa Yesu ilikuwa "ni kuziharibu kazi za shetani" (1Yoh 3:8). Hata mapepo aliyopambana nayo yalielewa ya kwamba Yesu alikuja kuyaharibu:

> Na mara palikuwa ndani ya sinagogi lao mtu mwenye pepo mchafu; akapaza sauti, akisema, "Tuna nini nawe, Yesu wa Nazareti? Je! Umekuja kutuangamiza? (Mk 1:23-24).

Katika Luka 4:18-19 Yesu alitamka agenda za huduma yake. Huduma yake

[11]Merril C. Unger, Biblical Demonology (Wheaton, IL: Scripture Press, 1971).

ilisimamia juu ya mambo sita:

1. *Upako:* Alikuja ili kuhudumu katika upako wa Roho Mtakatifu. ("Roho wa Bwana yu juu yangu kwa maana amenitia mafuta … ")
2. *Kuhubiri:* Alikuja kuhubiri injili kwa watu waliopotea. ("…kuwahubiri maskini habari njema")
3. *Kuwaweka wafungwa huru:* Alikuja kuwafungulia walewaliofungwa na dhambi na shetani. (Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao . . .")
4. *Uponyaji:* Alikuja kuwaponya wagonjwa. ("…na vipofu kupata kuona tena, … ")
5. *Kuwaacha huru waliosetwa:* Alikuja kuwafungulia wale walio katika utumwa - kiroho, kimwili, kihisia, Kidini, kiuchumi na kijamii . (" … kuwaacha huru waliosetwa:)
6. *Kutangaza Kuja kwa Ufalme wa Mungu:* Alitangaza kuwa wakati umetimia kwa ajili ya kuja ufalme wa Mungu ("… kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa.")

Katika Utendaji wa Huduma Yake

Yesu hakutangaza tu kwamba amekuja kupambana na kuziharibu kazi za shetani, bali pia alidhihirisha jambo hilo katika utendaji wa huduma yake.

Sehemu mbili za mkazo wa huduma ya Yesu zilikuwa: (1) kuhubiri/kufundisha na (2) uponyaji (angalia: Mt 4:23; 9:35). Mara nyingi aliyachanganya mambo hayo mawili. Hivyo alichanganya mapambano dhidi ya nguvu za giza na huduma ya kuihubiri kweli katika mikakati ya huduma yake.

Kuna mifano mingi sana ya mapambano dhidi ya nguvu za giza katika huduma ya Yesu. Tumechagua mifano minne tu ili kuwakilisha katika somo letu.

1. Majaribu yake nyikani. (Soma Luka 4:1-13). Katika majaribu yake nyikani Yesu alikutana ana kwa ana katika mapambano na shetani. Luka anasema ya kuwa Yesu aliingia katika mapambano na shetani akiwa "amejaa nguvu za Roho Mtakatifu" (mstari 1). Hili lilikuwa pambano kuu la kwanza la Yesu dhidi ya nguvu za giza. Hapa mwanzo tu wa huduma yake, alidhihirisha nguvu si tu juu ya pepo, bali pia juu ya mfalme wa mapepo, shetani mwenyewe. Habari za kushindwa kwa nahodha wao bila shaka zilienea haraka katika ulimwengu wa mapepo, kwa sababu kutokea wakati huo na kuendelea mapepo yanaonekana kutambua na kuogopa nguvu za Yesu. (Angalia: Mk 1:23-24 kama mfano.)

2. Muujiza wake wa kwanza katika Marko. (Soma Marko 1:21-27; 34,39; 3:10-11). Muujiza wa kwanza katika injili ya Marko ni mfano halisi wa

mapambani ya Yesu dhidi ya nguvu za mapepo. Kulikuwepo na jambo fulani kuhusiana na uwepo wa Yesu ambalo liliyatahayarisha mapepo. Yakitahayarishwa na uwepo wake, yalilia kwa sauti ya woga. Yesu aliyaamuru mapepo, "Nyamaza" na "Mtoke . . ." Hayakuwa na uchaguzi bali kumtii.

3. Mapambano yake na mtu mwenye pepo katika nchi wa Wagerasi. (Soma Marko 5:1-20). Hadithi ya Yesu alipomtoa pepo mtu aliyepagawa katika nchi ya Wagerasi ni mfano mzuri wa mapambano ya Yesu katika kutoa pepo yaliyoelezwa katika maandiko. Tena kama katika mfano wetu wa mwisho, mapepo haya pia yanaonekana kutahayarishwa na uwepo wake Yesu. Na tena mtu aliyepagawa anakombolewa kabisa kutokana na mapepo kwa amri ya Yesu.

4. Alivyomponya kijana aliyepagawa na mapepo. (Soma Marko 9:14-32). Kijana aliyepagawa katika Marko 9 tena anadhihirisha jinsi Yesu alivyopambana wazi kabisa na kuzishinda nguvu za mapepo. Kwa mara nyingine tena mapepo ilibidi yatii amri yake Yesu. Wanafunzi wake walipomuuliza ni kwa nini hawakuweza kumtoa pepo, Yesu aliwaonyesha upungufu wao katika maombi kama sababu yao ya kutokuwa na nguvu (mstari 29).

Yesu alifanya ishara, maajabu na miujiza katika huduma yake yote; muda hautoshi kutuwezesha kuangalia mambo yote haya. Hata hivyo yabidi uifanye huduma ya Yesu kuwa mafundisho ya maisha yako yote, pia jitahidi kumuiga yeye katika mambo yote aliyoyasema na kuyafanya. Tunaweza kujifunza mengi kuhusu kuponya wagonjwa na kushughulika na pepo kwa njia ya mafunzo haya pamoja na mapambano mengine ya Yesu dhidi ya nguvu za giza.

Katika Mafundisho ya Wanafunzi Wake

Yesu hakuja tu kuziharibu kazi za shetani bali aliwafundisha pia wanafunzi wake kufanya hivyo hivyo. Ni wazi kwamba, sababu moja ambayo Biblia inatupatia maelezo mengi na ya kina jinsi Yesu alivyoponya wagonjwa, na jinsi alivyowakomboa wale waliokuwa katika kifungo, ni ili sisi kama ilivyokuwa kwa wanafunzi wake kumi na wawili, tuweze kuchunguza jinsi alivyohudumu, na kama mitume, nasi tumuige.

Nyakati nyingi tunamwona Yesu akiwafundisha wanafunzi wake jinsi ya kuhudumu katika nguvu za Roho. Katika Luka 9:1-6 na Luka 10:1-23 Yesu aliwatuma wanafunzi wake katika safari ya mafunzo ya kazi ya utume. Safari ya pili aliwatuma 70, Yesu alihitaji walete ripoti kwake (mstari 17). Baada ya kupokea ripoti hiyo, Yesu alichukua muda kuwafundisha. Hapa anawaeleza wazi kwamba amewapa mamlaka juu "ya nguvu zote za adui" (Luka 10:19).

Katika sura inayofuata (Lk 11:14-26), Yesu anawapa wanafunzi wake

mafundisho zaidi jinsi ya kushughulika na nguvu za mapepo. Sasa waweza kutaka kusoma kwa utaratibu na kujifunza sehemu hiyo ya maandiko.

Katika Kuikabidhi Huduma yake kwa wale Waliomfuatia

Katika kuikabidhi kazi ya huduma yake kwa wanafunzi wake, Yesu aliweka wazi ya kwamba watahusika katika huduma yenye nguvu, kama vile yeye mwenyewe alivyohusika. Katika kuwateua wale mitume kumi na wawili, Yesu aliwatuma "aliwapeleka wapate kuhubiri tena wawe na amri juu ya pepo" (Mk.3:14). Ni wazi kwamba walihitajika kuwa na huduma ile ile ya namna mbili kama alivyoifanya Bwana Yesu, yaani huduma dhidi ya nguvu za giza na kuihubiri kweli yaani neno la Mungu.

Katika Luka 9:1-2, wakati Yesu alipowatuma wale kumi na wawili "akawapa uwezo na mamlaka juu ya pepo wote na kuponya maradhi. Akawatuma wautangaze ufalme wa Mungu, na kupoza wagonjwa." Tena tunaona sehemu mbili za huduma, huduma ya vitendo na ile ya kulinena neno la Mungu (nguvu na kuhubiri) vimetiliwa mkazo! Halafu, katika Luka 10 Yesu alipowatuma wale 70 aliwapa nguvu na mamlaka kutoa pepo (Lk 10:1;17-20).

Katika "agizo kuu", kama ilivyoandikwa katika Marko, baada ya Yesu kutoa agizo la kuipeleka injili ulimwenguni pote, aliahidi kwamba tunaweza pia kutegemea ishara zile zile kufuatia huduma zetu kama zilivyo fuatia huduma yake (Mk 16:15-18). Kutokana na rekodi ya maandiko, wanafunzi wake walikwenda wakatimiza huduma hiyo ya sehemu mbili yaani huduma yenye nguvu. (Soma: mistari 19-20). Sisi kama wale waliosikia maneno yale, lazima tuende katika nguvu za Roho Mtakatifu kuihubiri injili na ishara zikifuatana nasi.

Kitendo cha mwisho cha Yesu cha kuikabidhi huduma yake ya nguvu kwa wafuasi wake ilikuwa ni kuwapatia nguvu ya upako ule ule uliomwezesha yeye katika huduma yake duniani (Mdo 10:38). Alifanya hili katika siku ya Pentekoste "wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka" (Mdo 2:4). "Nguvu ile ile ya Kipentekoste" inapatikana kwetu leo, ili sisi nasi tuweze kuzifanya kazi za Yesu (Linganisha Yn 14:26 na 16:7).

HUDUMA YENYE NGUVU KATIKA KANISA LA KWANZA

Wakiisha kupokea nguvu za Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste, mitume walikwenda na kuiga huduma ya Yesu. Kama huduma yaYesu ilivyokuwa, huduma zao pia zilikuwa kuhubiri neno na vitendo. Hawakuihubiri tu injili, bali pia kwa njia za miujiza, ishara na maajabu, waliifanya kazi ile ile aliyoifanya Yesu,wakidhihirisha kuwa ufalme wa Mungu umekuja kwa nguvu kuu.

Uchunguzi Kuhusu Huduma ya Kanisa la Kwanza

Huduma ya kanisa katika kitabu cha Matendo ya mitume ni kuiendeleza huduma ya Roho Mtakatifu ambayo alimpaka mafuta Yesu ili kutenda kazi. Tafakari sentensi isemayo "aliyoanza Yesu kufanya na kufundisha" katika Matendo 1:1:

> Kitabu kile cha kwanza nalikiandika, Theofilo, katika habari ya mambo yote *aliyoanza Yesu kufanya na kufundisha* (mkazo wa mwandishi).

Maneno haya yana lengo la kusema kwamba, sasa kwamba Yesu ameisharejea mbinguni, kanisa litaendeleza huduma yake, pamoja na kazi zake za nguvu. Na haya ndiyo ambayo kanisa la kwanza lilifanya.

Ishara na maajabu vilikuwa msingi wa huduma ya kanisa la kwanza. Usomaji wa uangalifu wa kitabu cha Matendo ya mitume unadhihirisha kwamba mitume katika utendaji wa huduma walifuata kanuni ile ile iliyoanzishwa na Yesu ya kuhubiri Neno na kuidhihirisha kazi ya huduma kwa matendo. Huduma yao ilihusisha ishara na maajabu, uponyaji, na kutoa pepo, miujiza ya uumbaji wa asili na masuala ya chakula, ufufuaji wa wafu, kunena kwa lugha, unabii, maono, na miujiza mingine isiyo ya kawaida.

Matokeo ya kuchanganya ishara na maajabu pamoja na kuihubiri injili yenye upako, mshangao na ajabu vilionekana katikati ya watu; injili ilihubiriwa kwa nguvu kubwa ya ushawishi; na maelfu ya watu waliokolewa. Mambo haya haya yanaweza kutokea leo, endapo sisi, kama mitume, tutafuata utendaji huu wa aina mbili ambao Yesu alionyesha mfano wake.

Mifano Michache ya Huduma yenye Nguvu Katika Kanisa la Kwanza

Hebu sasa tuangalie mifano michache ya huduma yenye nguvu katika kitabu cha Matendo ya mitume. Hapa kuna mifano miwili. Unaposoma kila mfano, jibu maswali manne kuhusu kila huduma yenye nguvu ilipotendeka.

1. Pentekoste. Kwa uangalifu soma Matendo 2:1-41. Sasa jibu maswali yafuatayo:

a. Je! Ni matendo gani ya nguvu za Mungu yalitendeka katika siku ya Pentekoste?
b. Je! Makusanyiko ya watu waliitika vipi kwenye matendo hayo ya udhihirisho wa nguvu?
c. Je! Huduma ya kuihubiri kweli ilitendeka? Kama ndiyo tafadhari eleza kwa kifupi.
d. Je! Kulikuwa na matokeo gani katika huduma yenye nguvu iliyotendeka siku hiyo?

2. Uponyaji mbele ya Mlango Mzuri (Matendo ya mitume 3:1-26) Sasa, kwa uangalifu soma Matendo 3:1-26. Jibu maswali yale yale manne kama ulivyofanya katika mfano wa awali:

a. Je! Ni udhihirisho gani wa nguvu za Mungu ulitokea mbele ya Mlango Mzuri wa Hekalu?
b. Je! Muitikio wa makusanyiko ya watu ulikuwaje kutokana na udhihirisho huo wa nguvu za Mungu?
c. Je! Huduma ya kuihubiri injili ilitendeka? Kama ndiyo, eleza kwa ufupi.
d. Je! Kulikuwa na matokeo gani katika huduma yenye nguvu iliyotendeka siku hiyo?

— Sura Ya Tatu —

Huduma Yenye Nguvu Na Ufalme Wa Mungu

UFALME WA MUNGU UMEFAFANULIWA

Je! Unafikiri nini unaposikia maneno "ufalme wa Mungu?" Wakristo wengi wanao ufahamu mdogo sana au hawana kabisa kuhusiana na "ufalme wa Mungu". Hii ni hatari, kwa sababu ufalme wa Mungu ni moja ya mambo makubwa yaliyomo katika Agano Jipya. Ufahamu wa kutosha wa ufalme wa Mungu ni muhimu sana kwa uinjilisti wenye nguvu.

Utawala wa Mungu

Tunapolifikiria neno "ufalme" katika maana hii ya Agano Jipya, tusifikirie kuwa ni eneo fulani la kijeografia, bali tufikirie kama ni utawala au sehemu iliyo chini ya mamlaka ya Mungu, au mamlaka yake juu ya uumbaji wake. Tunaposema ufalme wa Mungu umekuja, tunamaanisha kwamba Mungu amekuja kuuweka ufalme au utawala wake duniani.

Maneno Mawili ya Muhimu ya Ufalme

Ufalme wa Mungu unaweza kufikiriwa kuwa upo sasa na pia utakuja baadaye. Ufalme umekuja na pia utakuja. Tunahitimisha wazo kwa namna hii: anaandika Don Williams, "Ni kweli ufalme upo hapa, lakini haupo katika ukamilifu wake. Wakristo waliookolewa basi, wanaishi katika ufalme uliopo na unaokuja."[12]

---

[12]Williams, uk. 107.

1. Kwa hiyo, ufalme wa Mungu tayari upo. Ulikuja katika na kwa kupitia kazi ya Yesu Kristo (Lk 17:20-21). Baadaye ulikuja tena wakati Roho Mtakatifu alipomwagwa katika siku ya Pentekoste (Mk.9:1; Mdo.1:8). Ilikuwa ni kwa njia ya Pentekoste ambapo Yesu alihamishia huduma yake ya ufalme juu ya kanisa. Peter Kuzmic anasema, "Watu sasa wanauteka (ufalme wa Mungu) au unashikwa na wenye nguvu (Mt 11:12-13; Lk 16:16). Mapinduzi ya utawala wa shetani tayari yamekwisha anza, na nguvu ya ufalme ujao iko tayari ikitenda kazi katika ulimwengu wa sasa, na baraka za masihi zinapatikana kwa wale wanaoitikia wito wake."[13]

2. Lakini ufalme wa Mungu pia unakuja. Ufalme wa Mungu utakuja katika utimilifu wake wakati wa kuja kwa Kristo mara ya pili (Ufu 11:15). Kwa hiyo wakati ufalme wa Mungu umekwisha kuja na uvamizi dhidi ya ufalme shetani tayari umeshaanza, kunabakia ufalme ujao juu ya nchi. Hili litatokea wakati Mwana wa Adamu atakapokuja "katika nguvu na utukufu mwingi" (Mt 24:30), kumshinda shetani na kuuweka utawala wake wa haki duniani.

Kweli hii (kweli ya kwamba ufalme wa Mungu umekwisha kuja, na tena unakuja) inaeleza hali halisi ya maisha yetu ya sasa. Inaeleza vyote ushindi dhidi ya shetani upande mmoja, na maendeleo ya mapambano dhidi yake upande wa pili. Inaeleza kwa nini wengi leo wanapokea uponyaji ghafla wakati ambapo wengine wengi wanabakia wagonjwa na wanafariki dunia. Inaeleza kwa nini tuna nguvu dhidi ya mapepo, wakati shetani bado anaendelea kuwatawala watu wengi katika maeneo mengi ya ulimwengu. Ufalme wa Mungu umekuja kwa kiasi; ingawaje, siku moja utakuja katika utimilifu wake. Sasa tunazo nguvu na mamlaka juu ya mapepo, lakini hatimaye nguvu zote za giza zitashindwa kabisa.

---

[13]Peter Kuzmic, "Kingdom of God," *Dictionary of Pentecostal and Charismatic Movements,* (Grand Rapids: Zondervan Publishing House, 1988) uk. 523.

KUJA KWA UFALME WA MUNGU

Yesu Alikuja Kutangaza utawala wa Mungu

Ujumbe wa ufalme wa Mungu ulikuwa ni msingi wa mahubiri ya Yesu. Sikiliza maneno yake:

> Imenipasa kuihubiri habari njema ya ufalme wa Mungu katika miji mingine pia; *maana kwa sababu hiyo nalitumwa* (Lk 4:43, mkazo wa mwandishi. Angalia pia: Mt 4:23; Mk 1:14-15; Lk 8:1, 9:11).

Kutokana na Peter Kuzmic, "Swala la ufalme wa Mungu linachukua sehemu ya umuhimu sana katika mafundisho na utume wa Yesu. "Wazo hili kuu" la Yesu, kama lilivyoitwa, ni kiini cha mahubiri na ufunguo wa kuielewa huduma."[14]

Yesu alianza huduma kwa kutangaza, "Wakati imetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia… " (Mk 1:15; angalia pia Mt 3:1). Akianza huduma yake namna hii, Yesu alikuwa akitangaza kuja kwa utawala wa Mungu duniani. Alikuwa akisema kwamba ufalme wa Mungu umefika, na ya kwamba ulikuwa sasa karibu na yeyote atakayetaka kuupokea. "Mwaka wa Bwana uliokubalika" (Lk 4:19) umekuja. Mungu amekuja katika Yesu Kristo ili kurejesha kile kilichokuwa chake, na kuleta baraka za mbinguni kwa mwanadamu aliyeko duniani.

Katika vitabu vya injili, ufalme wa Mungu ulikuwa pia ni msingi wa mahubiri ya mitume. Mahali popote ambapoYesu aliwapeleka kuhudumu, aliwaelekeza kuhubiri ufalme wa Mungu na kudhihirisha nguvu yake (Mt 10:7; Lk 9:2; 10:9, 11).

Kuja kwa Ufalme wa Mungu Kumeleta Vita

Mungu amekuja kwanza katika Kristo, na sasa katika kanisa lake, lililotiwa nguvu na Roho Mtakatifu, ili kurejesha kile ambacho shetani amekiiba. Amekuja kwa nguvu kurejesha kile ambacho kwa haki ni chake. Sasa kwa sababu ufalme wa Mungu umekuja, mapambano yameanza. Shetani aliyewatawala watu anapingwa vikali na Mungu, kwa hiyo vita kali imeanza. (Angalia Efe 6:12).

---

[14]Kuzmic, uk. 522.

Kuja kwa Ufalme wa Mungu ni kwa Nguvu

Wakati ufalme wa Mungu unapokuja, hauji kiwoga, wala hauji kwa kujitetea—unakuja katika nguvu. Paulo alisema, "Kwa maana ufalme wa Mungu hauwi katika neno, bali katika nguvu" (1Kor 4:20). Kwa kweli, ufalme wa Mungu hauji katika njia nyingine yoyote. Kwa sababu ya upinzani wa kijeuri wa shetani dhidi ya ufalme unaokuja, basi ufalme wa Mungu lazima usonge mbele kwa nguvu. Mvamizi lazima atolewe kwa nguvu. Sikiliza maneno haya ya Yesu:

> Lakini mimi nikitoa pepo kwa Roho wa Mungu, basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia. Ama, awezaje mtu kuingia ndani ya nyumba ya mtu mwenye nguvu na kuviteka vyombo vyake, asipomfunga kwanza yule mwenye nguvu? Ndipo atakapoiteka nyumba yake" (Mt 12:28-29).

Hivyo, kanisa lazima litembee katika nguvu kama litahitaji kupeleka mbele ufalme wa Mungu hapa duniani. Siku moja Yesu alizungumzia siku ambayo wanafunzi wake watauona ufalme wa Mungu ukija katika nguvu:

> Amin nawaambia, pana watu katika hawa wasimamao hapa, ambao hawataonja mauti kabisa, hata watakapouona ufalme wa Mungu umekuja kwa nguvu (Mk 9:1).

Wanafunzi walikuwa wameuona ufalme wa Mungu ukitembea katika nguvu katika huduma ya Yesu; hata hivyo, Yesu alipotoa tamko hili alikuwa akizungumzia wakati ujao. Na wakati huo alioutaja utatokea wakati ujao lakini pia ulio karibu. Utatokea kabla ya vifo vya kati ya wale waliokuwepo. Yesu alikuwa akizungumzia siku ya Pentekoste wakati kanisa lake litakuwa limevikwa uwezo utokao juu (Lk 24:49). Tunaweza kusema pia kwamba tunauona ufalme wa Mungu ukija katika nguvu kila wakati tunapomuona mtu amejazwa au kuguswa na Roho wa Mungu (Mdo 1:8).

Ishara ya Kuja kwa Ufalme

Kati ya vitu vingine, ishara, maajabu na miujiza vinashuhudia ya kwamba ufalme wa Mungu upo hapa. Hiki ni kivuli kinachoonyesha ni vipi itakuwa wakati ufalme wa Mungu utakapokuja katika utimilifu wake. Uponyaji leo ni kivuli cha mwisho wa kuteseka na magonjwa (Ufu 21:4). Kutoa pepo ni ishara ya uvamizi wa Mungu katika eneo la shetani na ni ishara ya kuharibiwa kabisa kwa shetani Yesu atakaporudi (Ufu 20:10).

Katika kile kinachoitwa na wengi "sala ya Bwana," Yesu alifundisha

kwamba "Ufalme wako uje" (Mt 6:10), alikuwa akitufundisha kuomba hasa kwa ajili ya vitu vitatu:

1. Tunatakiwa kuomba kwa ajili ya watu wapate kuokolewa. Ufalme wa Mungu unakuja kwa mtu binafsi wakati anapokuwa amezaliwa mara ya pili. Ndivyo Yesu alivyomaanisha aliposema, "...ufalme wa Mungu umo ndani yenu" (Lk 17:21).

2. Tunatakiwa kuombea watu ili wapate kujazwa na Roho, wapone, na wakombolewe na uonezi wa mapepo. Ufalme wa Mungu unakuja katika nguvu wakati watu wanapojazwa na Roho au kuachiwa huru kwa nguvu za Mungu (Mt 12:28 na Lk11:20; Lk10:9).

3. Tunahitaji kuomba ili Yesu arudi tena (Ufu 22:20). Yesu atakapokuja tena atamshinda shetani na kuusimamisha ufalme wake duniani. Ndipo Ufalme wa Mungu utakuwa umekuja katika utimilifu wake.

KUHUBIRI INJILI YA UFALME WA MUNGU

Tumeitwa Kuihubiri Injili ya Ufalme

Yesu aliwatuma wanafunzi waende kuhubiri habari njema za ufalme. Walitakiwa watangaze kwamba Mungu, kwa njia ya Kristo, amekuja kuusimamisha ufalme wake. Sikiliza maneno yake:

> Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja (Mt 24:14).

Katika vitabu vinne vya injili Yesu alisema kuhusu ufalme wa Mungu, au maneno yanayofanana , ufalme wa mbinguni, karibu mara 90. Katika siku alizokuwepo baada ya kufufuka, kabla hajarudi mbinguni, tunaambiwa kwamba alitumia siku 40 na wanafunzi wake "na kuyanena yaliyohusu ufalme wa Mungu" (Mdo 1:3). Ni vitu gani ambavyo vilihusu ufalme wa Mungu ambavyo alizungumzia? Kitu kimoja cha muhimu ambacho alizungumzia ilikuwa ni kujazwa na Roho Mtakatifu (Mdo 1:4-5). Pia alizungumzia kushuhudia katika nguvu za Roho (Mdo 1:8). Yesu aliwaagiza wanafunzi wake kuihubiri "injili yaufalme wa Mungu." Alipowatuma wale thenashara aliwapa maagizo yafuatayo:

> Akawaita wale thenashara, akawapa uwezo na mamlaka juu ya pepo wote na kuponya maradhi. *Akawatuma wautangaze ufalme wa Mungu, na kupoza wagonjwa"* (Lk 9:1-2, mkazo wa mwandishi).
>
> Na katika kuenenda kwenu, hubirini, mkisema, ufalme wa mbinguni umekaribia. Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; Mmepata bure, toeni bure (Mt 10:7-8).

Kwa wale sabini aliwapa agizo linalofanana:

> Wapozeni wagonjwa waliomo, waambieni, ufalme wa Mungu umekaribia (Lk 10:9).

Kuhubiri kwa ufalme wa Mungu kuliendelea katika kitabu chote cha Matendo ya mitume. Hapa tunaona kanisa likihubiri na kufundisha injili ya ufalme. Wakati Filipo alipotelemkia Samaria tunasoma ya kuwa alimhubiri Kristo (Mdo 8:5), alitenda miujiza (8:6), na "alihubiri habari njema za ufalme wa Mungu na jina la Yesu Kristo" (8:12).

Katika Efeso Paulo alifundisha kwa muda wa miezi mitatu kuhusu ufalme wa Mungu (Mdo 19:8; 20:25). Na katika Rumi "alihubiri habari za ufalme wa Mungu na kufundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo" (Mdo 28:30).

Injili ya Ufalme Imeelezwa

Je! Ni nini basi injili ya ufalme ambayo Yesu aliwatuma wao, na sisi pia kuitangaza. Kumekuwa na ufafanuzi mwingi uliokwishatolewa kuhusu "injili ya ufalme". Watu kadha wenye kuchukulia maandiko ya Biblia kuwa yaliandikwa kuhusu nyakati fulani fulani tu, wanafundisha kwamba injili ya ufalme siyo injili hii tunayoihubiri leo, bali ni matangazo tu kuhusu kuja kwa Kristo ambayo yatahubiriwa tu wakati wa dhiki kuu, baada ya kanisa kunyakuliwa. Jambo hili, kwa kweli, siyo sahihi kwa sababu kama ilivyonukuliwa hapo juu, Yesu alituagiza kuihubiri injili ya ufalme kabla ya kuja kwake tena (Mt 24:14). Paulo ametuonya wazi ya kuwa tujihadhari na mtu awaye yote atakayekuja na kuihubiri *"injili nyingine*" (Ga 1:6-9) kuliko ile aliyoihubiri yeye.

George Eldon Ladd anafafanua injili ya ufalme kuwa ni "Habari Njema za ufalme wa Mungu." Anaendelea kusema, "Injili ya Ufalme ni Injili ambayo

ilihubiriwa na mitume katika kanisa la kwanza."[15] Wakati hatutofautiani na Ladd; tunapenda kuongezea tafsiri yake: Injili ya ufalme ni habari njema zinazotangazwa kutumia njia zilezile ambazo Yesu na wanafunzi wake walizitumia. Tom Marshall anatoa tafsiri hii nzuri kabisa ya injili ya ufalme: "Injili ya ufalme," anaandika, "ni Injili ya wokovu pamoja na nguvu za zamani zijazo."[16]

Yesu na kanisa la kwanza hawakutangaza tu kuhusu kuja kwa ufalme wa Mungu, na kupinduliwa kwa ufalme wa shetani, bali pia walidhihirisha nguvu za ulimwengu ujao kwa kuponya wagonjwa, kutoa pepo, na udhihirisho wa nguvu za Roho Mtakatifu. Msikilize Yesu akizungumzia jinsi ufalme wa Mungu utakavyosonga mbele:

> Torati na manabii vilikuwapo mpaka Yohana; tangu wakati huo habari njema za ufalme wa Mungu hutangazwa, na kila mtu hujiingiza kwa nguvu (Lk 16:16).
>
> Tangu siku za Yohana mbatizaji hata sasa ufalme wa mbinguni hupatikana kwa nguvu, nao wenye nguvu wauteka (Mt 11:12).

Sisi sio tu watangazaji wa ujumbe wa Yesu, bali pia ni waigizaji wa njia zake na uthibitisho wa nguvu za ufalme. Don Williams anasema, "Endapo tutashika agenda ya Yesu ya huduma, tutaomba upako wa nguvu za Mungu, ili tukiwa na nguvu juu yetu tuweze kuwahubiri maskini, wafungwa kufunguliwa kwao, vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru waliosetwa, na kutangaza 'mwaka wa Bwana uliokubaliwa (Lk 4:18-19)."[17]

Yesu alipowatuma wale Thenashara, "Aliwapa nguvu na mamlaka juu ya pepo wote na kuponya maradhi, akawatuma wautangaze ufalme wa Mungu na kupoza wagonjwa" (Lk 9:1-20). Baadaye alipowatuma wale sabini kutangaza kuja kwa ufalme wa Mungu aliwaambia:

---

[15]George Eldon Ladd, "The Gospel of the Kingdom," *Perspectives on the World Christiam Movement, A Reader* (Pasadena, CA: William Carey Library, 1981), uk. 59.

[16]Tom Marshall, *Foundations for a Healing Ministry,* (West Sussex, ENG: Sovereign World, 1988), uk. 51.

[17]Williams, uk. 139.

> Na mji wowote mtakaouingia, wakiwakaribisha, vileni vyakula vilivyowekwa mbele yenu; wapozeni wagonjwa waliomo, waambieni, ufalme wa Mungu umekaribia (Lk 10:8-9).

Hiyo ndiyo maana ya kuhubiri injili ya ufalme. Inamaanisha kuhubiri injili, lakini inamaanisha pia kufanya hivyo katika nguvu na upako wa Roho Mtakatifu na ishara zinazofuatana. Tumeitwa na Mungu na kupakwa mafuta na Roho wake ili kufanya hivyo tu.

— Sura ya Nne —

Huduma Yenye Nguvu Na Kuihubiri Injili

Mapambano dhidi ya nguvu za giza ni sehemu muhimu ya kuhubiri injili ya kweli. Katika Sura ya 3, "Huduma yenye nguvu na ufalme wa Mungu," tulizungumzia kuhusu kuhubiri "injili ya ufalme wa Mungu." Katika sura hii tutalipanua somo la kuhubiri injili na jinsi linavyohusiana na mapambano dhidi ya nguvu za giza. Somo mathubuti kuhusu huduma ya Yesu na mitume linathibitisha ya kuwa mapambano dhidi ya nguvu za giza ilikuwa sehemu ya muhimu katika huduma zote mbili. Mapambano dhidi ya nguvu za giza mara nyingi yaliambatana (au kutanguliwa) na mahubiri ya ujumbe wa injili. Ushuhuda wenye nguvu kuhusu kweli ya ujumbe wao ulikuwa ndiyo matokeo, pamoja na watu wengi waliokuwa wakiokolewa.

KUTENDA NA KUTANGAZA: SEHEMU MBILI ZA MUHIMU ZA USHUHUDA MADHUBUTI WA INJILI

Sehemu mbili madhubuti za ushuhuda wa injili ni kudhihirika kwa utendaji na kutangaza. Kwa kutangaza tuna maana ya kuihubiri injili. Kwa utendaji tuna maana ishara, maajabu, na miujiza iliyofuatia mahubiri ya injili. Nguvu ya injili lazima kwanza ithihirishwe, halafu ndipo kweli inaweza kuhubiriwa. Hii ni "Kuonyesha na kusema" katika hali yake ya juu. Nguvu za giza lazima kwanza zishindwe, ndipo ushindi unapoweza kutangazwa.

Kuyafanya Mambo ya Kwanza kuwa ya Kwanza

Katika Mathayo 12:28-29 Yesu alitufundisha ya kwamba lazima mara nyingi tupambane vita vya kiroho kabla ya injili haijahubiriwa kikamilifu. Sikiliza maneno yake:

> Lakini mimi nikitoa pepo kwa Roho wa Mungu, basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia. Ama awezaje mtu kuingia ndani ya nyumba ya mtu mwenye nguvu na kuviteka vyombo vyake, asipomfunga kwanza yule mwenye nguvu? *Ndipo atakapoiteka nyumba yake* (mkazo wa mwandishi).

Yesu anasema ya kuwa ni muhimu kuyafanya "mambo ya kwanza kuwa ya kwanza" katika kuihubiri injili. Kwanza, "tunamfunga mtu mwenye nguvu," *NDIPO* "tunaiteka nyumba yake." Mtu mwenye nguvu katika habari hii ni pepo kwenye nguvu anayetawala au maisha ya mtu binafsi, au jamii au eneo la mahali fulani. "Nyumba yake" ni mahali alipoiweka ngome yake. "Vyombo vyake" inawakilisha Roho ya mhusika, au roho za watu katika jamii au eneo la mahali fulani ambapo shetani amewaweka watu hao katika hali ya utumwa.

MTU MWENYE NGUVU wa Mathayo 12:28-29		
	Anapomtawala Mtu	Anapotawala jamii au eneo la mahali fulani
Mtu mwenye Nguvu	Pepo mwenye nguvu anamtawala mtu	Pepo mwenye nguvu akitawala jamii au eneo la mahali
Nyumba ya mtu Mwenye Nguvu	mtu chini ya utawala wa pepo	Jamii au eneo la mahali chini ya utawala wa pepo
Vyombo vya mtu mwenye Nguvu	Roho ya mtu	Roho za watu wa jamii fulani au eneo la mahali fulani

Yesu anatuambia ya kuwa kabla ya kuteka nyumba ya mtu mwenye nguvu na kuvichukua vyombo vyake, maana yake, kabla hatujampokonya roho za watu anaowashikilia mateka, lazima tupambane naye na kumshinda. Ninaamini ya kwamba, ishara ambayo Yesu amewaahidi wale wanaotimiza agizo kuu ni kwamba "watatoa pepo" (Mk 16:17). Mpangilio wa kwanza wa kazi ni kuzishinda nguvu za mapepo, ndipo tunaweza kutangaza kwa uhuru wokovu kwa wale walioshikiliwa mateka.

Nguvu Nyingi!

Kama tulivyokwisha kuona katika sura ya 1, Kristo amekwisha kutupatia

zana zote zinazotakiwa kuimaliza kazi. Zana mbili alizotupatia ni Roho mtakatifu na injili. Njia isiyoshindwa katika kutoa ushuhuda wa injili yenye nguvu na ushawishi ni ifuatayo:

Nguvu za Roho Mtakatifu	**+**	**Nguvu ya njili**	**=**	**Matokeo ya Ajabu**

Hebu kwa kifupi tuchunguze zana moja moja kati ya hizo.

1. Nguvu ya Roho Mtakatifu. Kwanza, Kristo ametupatia nguvu za Roho Mtakatifu. Katika Matendo 1:8 Yesu alituahidi ya kwamba tutapokea nguvu akiisha kutujilia Roho Mtakatifu. Kwa hiyo ni muhimu kwa yeyote yule anayetegemea kuhusika na kuishuhudia injili kuwa amejazwa na Roho Mtakatifu (angalia sura ya 6, "ubatizo wa Roho Mtakatifu na huduma yenye nguvu" kwa utimilifu wa somo hili). Siyo tu lazima tujazwe na Roho, bali ni lazima pia tujue jinsi ya kuzitumia nguvu hizo za Roho Mtakatifu katika huduma . (Tutalizungumzia jambo hili baadaye).

2. NGUVU ZAIDI ... Nguvu ya Injili. Tena, Kristo ametupatia injili. Hivyo ni muhimu sana tuwe na ufahamu mzuri wa nguvu hizo na kujua jinsi ya kuitumia vema injili. Katika Rumi 1:15-16 Paulo ameeleza uhakika wake katika injili:

> Kwa hiyo upande wangu mimi ni tayari kuihubiri injili hata na kwenu ninyi mnaokaa Rumi. Kwa maana siionei haya injili, kwa sababu ni uweza wa Mungu uletao wokovu, kwa kila aaminiye....

Tazama jinsi Paulo anavyoieleza injili ya kwamba "ni uweza wa Mungu uletao wokovu." Tena katika Rumi 10:17 Paulo anatuambia ya kwamba injili inayo ndani yake nguvu inayoumba imani katika maisha ya wale wanaoisikia: "Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo."

Kwa kuangalia vizuri maana katika mtiririko wa kifungu hicho cha maandiko ya Paulo, utagundua ya kwamba anazungumzia hasa injili. Anasema ya kwamba injili , ujumbe wa Kristo, inayo nguvu kubwa ya kuleta imani katika mioyo ya wasikiao!

Yesu katika kuzungumzia nguvu hii iletayo imani katika mfano wa kumea mbegu (Mk 4:26-29). Hapa anafananisha injili na mbegu:

> Akasema, 'ufalme wa Mungu, mfano wake ni kama mtu aliyemwaga mbegu juu ya nchi; akawa akilala na kuondoka, usiku na mchana, nayo mbegu ikamea na kukua asivyojua yeye, maana nchi huzaa yenyewe… (Mistari 26-28a).

Kama mbegu, injili ina nguvu ndani yake ya kutoa mavuno. Jinsi ilivyo na nguvu injili ya Yesu! Kama tu tutaitangaza, ina nguvu ndani yake yenyewe ya kutoa mavuno.

Lakini ni nini hasa maana ya kuhubiri injili hii ambayo tunazungumzia? Ni kuhubiri "neno la Kristo!" (Rum 10:17). Ni ujumbe wa Yesu na yale yote aliyoyatenda, Yote anayoyatenda, na yote yale atakayoyatenda baadaye. Katikati ya ujumbe huu wa injili ni kifo, kuzikwa na kufufuka kwa Kristo (soma kwa uangalifu: 1Kor 15:1-4). Tusije tukashindwa kuhubiri ujumbe wenye nguvu. Mara nyingi wale wanaoitwa "wahubiri wa injili" wanahubiri sehemu ndogo tu ya injili ya Yesu. Sisi tusishindwe kuhubiri habari njema za Yesu kwa ujasiri, kwa sababu ni habari hizo tu ambazo zinazo nguvu ya Mungu iwaleteayo watu wokovu (1Kor 1:18).

3. SAWA SAWA NA ... Matokeo ya Ajabu. Kama kwa uaminifu tutachanganya zana hizo mbili—nguvu ya Roho Mtakatifu na Nguvu ya Injili—tunaweza kutegemea matokeo ya ajabu. Hili ndilo lililotokea katika kanisa la kwanza katika kitabu cha Matendo ya mitume.

Tunaweza kufuatilia ukuaji wa ajabu wa kanisa la Agano Jipya kupitia mistari kadha katika kitabu cha Matendo ya mitume. Litakuwa ni zoezi la kufurahisha na la faida kwako kusoma na kuiwekea alama mistari ifuatayo katika Biblia yako. Unaposoma, tambua jinsi kanisa lilivyokua kutoka waumini 120 hadi maelfu kwa muda mfupi. Tambua pia jinsi ambavyo ukuaji huo wa ajabu ulivyoletwa kwa kuchanganya nguvu ya Roho Mtakatifu na uaminifu katika kuihubiri injili.

Ukuaji wa Kanisa la Kwanza katika Kitabu cha Matendo ya Mitume

---

Matendo 1:15; 2:41; 2:47; 4:4; 5:14; 6:1; 6:7; 8:6; 9:35; 9:42; 11:21; 11:24; 11:26; 12:24; 13:49; 14:1; 14:21; 16:5; 17:4; 19:18; 19:20; 19:26

MAPAMBANO DHIDI YA NGUVU ZA GIZA YALIVYOONEKANA KATIKA HUDUMA YA YESU NA KANISA LA KWANZA

Yalivyoonekana Katika Mahubiri na Mafundisho ya Yesu

Katika huduma yake Yesu alichanganya kufundisha na kuhubiri injili na uthibitisho wa nguvu za Roho Mtakatifu (angalia Mt 4:23 na 9:35). Hii ilisababisha makundi makubwa kuja kusikiliza ujumbe wake na kumfuata (Mt 4:24-25; 9:36).

Katika kuwaagiza (Mk 3:13-15) na baadaye kuwatuma wale thenashara (Lk 9:1-2), na katika kuwatuma wale sabini, Yesu aliwawezesha na kuwaelekeza kutoa pepo, kuponya wagonjwa, na kuihubiri injili ya ufalme (Lk 10:9).

Hatimaye akitoa agizo kuu la kuhubiri injili ulimwenguni pote, Yesu aliahidi uwezo wa kimungu ambao ungekuja tu kwa njia ya kujazwa na Roho Mtakatifu. (Soma kwa uangalifu Mk 16:17-18; Lk 24:48-49; Yn 22:21-22; Mdo 1:8).

B. Yalivyoonekana Katika Mahubiri na Mafundisho ya Kanisa la Kwanza

1. Katika Matendo ya Mitume. Katika Matendo ya mitume, tunaona waziwazi namna ya kushuhudia. Kanisa la kwanza nyakati zote walichanganya mahubiri ya injili na udhihirisho wa nguvu za Roho Mtakatifu. Ingawa namna hiyo ya huduma inaonekana katika kitabu kizima cha Matendo ya mitume, nitanukuu mifano minne tu kati yake:

a. Pentekoste. Mfano wetu wa kwanza ulitokea siku ya Pentekoste (Mdo 2:1-41). Hapa kulianzia na matendo makuu ya nguvu za Mungu. Maelfu ya watu walioingia katika nyua za hekalu ili kuabudu siku ile hawakuwa na wazo wala hamu ya kusikiliza mahubiri ya wafuasi wa Yesu. Lakini ghafla wakasikia kutoka mbinguni "uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi" (mstari 2). Katika mshangao wao, waliona "zimewatokea ndimi zilizogawanyika kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao" (mstari 3); ndipo wakawasikia wale 120 wakianza "kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka" (mstari 4).

Wakati ule ule, "mabadiliko ya imani" makubwa yakatendeka katika mioyo ya wale walioshuhudia matendo makuu ya nguvu za Mungu na uwepo wake. Kwa sababu ya miujiza walioishuhudia, mtazamo wao mzima ukawa umebadilika ghafla. Hawakuwa tena wapitaji wasio na hamu na mambo ya wafuasi wa Yesu; bali walikuwa sasa washiriki wa mkutano ule wakiwa tayari kuamini na kuipokea injili. Petro aliposimama kuhubiri, walikuwa tayari wanayo hamu na yale

aliyotaka kusema. Na, Petro alipomaliza mahubiri yake,watu 3,000 waliitikia.

"Mabadiliko ya imani" wakati wa Pentekoste

Watu kabla ya muujiza wa Pentekoste		Watu baada ya muujiza wa Pentekoste
Hawakuwa na hamu	.....>.....>.....>.....>.....>.....>.....>.....>.....>.....> ***Mabadiliko ya Imani***	Walikuwa tayari kuamini

b. Mlango mzuri. Mfano wetu wa pili ulitokea muda mfupi tu baadaye. Tena tunaona mitume wakifuata namna ile ile ya kuchanganya udhihirisho wa nguvu za Roho Mtakatifu na mahubiri ya wazi ya injili ya Kristo. Hii ilitokea kwenye ingilio la hekalu liitwalo Mlango Mzuri (Mdo 3:1-4:4). Matokeo ya udhihirisho wa nguvu ya Mungu, mtu aliyezaliwa kiwete anaponywa, kundi lile lile ambalo awali halikuwa na nia ya kuwasikiliza wafuasi wa Yesu, kwa mara nyingine tena "imani yao inazidi kubadilishwa." Ghafla "wakajaa ushangao wakastaajabia...[na] wakawakusanyikia mbio wakishangaa sana" (3:10-11). Kwa mara nyingine tena Petro alisimama na kuhubiri injili ya Kristo, matokea yake yalikuwa kwamba wengi walisikia na kuamini ujumbe wake "Na hesabu ya watu waume ikawa kama elfu tano" (4:4).

c. Filipo katika Samaria. Tunaona mtiririko huo huo— muunganiko kati ya utendaji wa nguvu za Roho Mtakatifu na kuhubiriwa kwa injili kukiendelea katika huduma ya Filipo katika Matendo 8:1-7. Maandiko matakatifu yanasema ya kuwa "Filipo akatelemka akaingia mji wa Samaria, akawahubiri Kristo" (mstari 5). Pamoja na kuhubiri injili, pia alidhihirisha nguvu za Mungu: "Na makutano kwa nia moja wakasikiliza maneno yale yaliyosemwa na Filipo na walipoyasikia na kuziona ishara alizokuwa akizifanya" (mstari 6). Ishara hizo za kimiujiza zilikuwa kutoa pepo, na uponywaji wa wengi waliopooza na viwete. Matokeo yalikuwaje? Makutano kwa nia moja wakasikiliza maneno yale yaliyosemwa (mstari 6); "...walipomwamini Filipo akihubiri habari njema za ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo" (mstari 12); na "..ikawa furaha kuu katika mji ule" (mstari 8).

d. Paulo katika Lystra. Mfano wa mwisho wa namna ambavyo kanisa la

kwanza lilivyochanganya utendaji wa matendo ya nguvu za Roho Mtakatifu na mahubiri ya injili unapatikana katika huduma pa Paulo katika mji wa Galatia wa Lystra (Mdo 14:8-10):

> Na huko Lystra palikuwa na mtu mmoja, dhaifu wa miguu, kiwete tangu tumboni mwa mamaye, ambaye hajaenda kabisa. Mtu huyo alimsikia Paulo alipokuwa akinena; ambaye alimkazia macho na kuona ya kuwa ana imani ya kuponywa, akasema kwa sauti kuu, simama kwa miguu yako sawasawa. Akasimama upesi akaenda.

Kama katika sehemu zote katika kitabu cha Matendo ya Mitume, Paulo alitumia nafasi hii kuhubiri ujumbe wa injili (angalia mistari 7; 15-17).

Ikiwa tutahitaji kuona matokeo yale yale katika huduma za Agano Jipya, lazima basi tutumie mifano hii kama changamoto kwa huduma zetu za uinjilisti.

2. Katika mafundisho ya Paulo. Si tu kwamba tunaona utendaji na mahubiri vikiwa vimeonyeshwa katika huduma ya Yesu na mitume hapo mwanzo, pia tunaona mafundisho ya wazi katika barua za Paulo. Katika barua yake ya kwanza kwa kanisa la Korintho, Paulo, akizungumzia kuhusu mambo katika huduma yake aliyokuwa ameyafanya katikati yao anaandika,

> Maana niliazimu nisijue neno lolote kwenu ila *Yesu Kristo, naye amesulibiwa.* . .. Neno langu na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali *kwa dalili za Roho na za nguvu,* ili imani yenu isijengwe katika hekima za wanadamu, bali katika nguvu za Mungu" (1Kor 2:2-5, mkazo wa mwandishi).

Wakati alipokuwa na Wakorintho, huduma ya Paulo ilikuwa na msingi wa vitu viwili: ujumbe wa "Yesu Kristo aliyesulibiwa," na "udhihirisho wa nguvu za Roho." Katika 2Wkorintho 12:12 aliwakumbusha ya kwamba, alipokuwa nao, "kweli ishara za mtume -- ishara, maajabu na miujiza -- vilitendwa katikati [yao]. . .." Katika 1Wakorintho 14:23-26 Paulo analieleza kanisa kuwa litegemee udhihirisho wa nguvu na uwepo wa Roho wakutanikapo. Alipokuwa akielezea huduma yake kwa Warumi, Paulo aliwakumbusha ya kuwa huduma yake ilikuwa na ishara zilizokuwa na udhihirisho wa nguvu za Roho:

> Maana sitathubutu kutaja neno asilolitenda Kristo kwa kazi yangu, mataifa wapate kutii, *kwa neno au kwa tendo*—kwa nguvu za ishara na maajabu, katika nguvu za Roho Mtakatifu; hata ikawa tangu Yerusalemu, na kando kando yake mpaka Iliriko

nimekwisha kuihubiri injili ya Kristo kwa utimilifu" (Rum 15:18-20, mkazo wangu).

Tambua ya kwamba ujumbe wa Paulo ulikuwa na vyote "yale *niliyonena* na *kutenda*." Alitenda "ishara na miujiza kwa njia ya nguvu za Roho Mtakatifu," na pia "aliihubiri injili ya Kristo kwa utimilifu."

Hatimaye, katika 1Wathesalonike 1:5 Paulo anawakumbusha Wathesalonike jinsi injili ilivyowafikia:

> Injili yetu haikuwafikia katika maneno tu, bali katika nguvu, na katika Roho Mtakatifu na uthibitifu mwingi.

Tena tunaona namna ile ile ya kuihubiri injili pamoja na utendaji wa nguvu za Roho, vikileta majibu ya dhahiri na ya kudumu—ambayo ni kanisa la Thesalonike lenyewe.

MWISHO

Tumeonyesha katika sura hii ya kuwa kuna mambo muhimu mawili katika huduma ya kweli ya injili ya Kristo. Moja ni udhihirisho wa nguvu za Roho wa Mungu; na lingine ni kuihubiri injili kwa uwazi. Endapo tutahitaji ushuhuda wetu kuwa na manufaa, lazima pia tujifunze kutumia njia zilezile ambazo Yesu na mitume walizitumia.

— Kifungu Cha II —

Matayarisho Ya Huduma Yenye Nguvu

— Sura ya Tano —

Mambo Ya Muhimu Katika Matayarisho Ya Huduma Yenye Nguvu

Katika somo letu la huduma yenye nguvu, sasa tunaanza Kifungu cha II, "Matayarisho ya Huduma Yenye Nguvu." Yeyote anayehitaji kuhusika katika huduma ya uinjilisti wenye nguvu lazima atilie maanani chanzo cha maelekezo ya huduma yake na matayarisho yake yenyewe. Katika somo hili tutaangalia mambo yote mawili. Tutajibu maswali yafuatayo: "Je! Ni mambo gani muhimu katika huduma ya mapambano dhidi ya nguvu za giza? Na "Je ni matayarisho gani yanahitajika ili kuwa na huduma madhubuti na yenye nguvu?"

MAMBO MUHIMU KATIKA HUDUMA YENYE NGUVU

Yako mambo mengi ambayo yanahusika na ujenzi wa huduma yenye nguvu katika maisha ya mtenda kazi wa Kristo. Katika somo hili tutashughulikia mambo matano ambayo tunafikiria ya kwamba ni ya muhimu.

Upako

Jambo la kwanza la muhimu katika huduma ya mapambano dhidi ya nguvu za giza ni upako. Neno upako tinamaanisha uwepo wa Roho Mtakatifu unaokuja kukaa juu ya mkristo aliyekwisha kujazwa na Roho mtakatifu anapokuwa yuko katika huduma. Ipo mifano mingi katika Biblia inayohusu upako. Upako wa Roho Mtakatifu ulimjia Petro wakati yeye na Yohana walipoitwa mbele ya baraza la wakubwa na wazee na waandishi ili kueleza tendo lao la kumponya mtu kiwete na kuhubiri injili katika ua wa hekalu sehemu iliyoitwa tao la Sulemani:

> Ndipo Petro, *akijaa Roho Mtakatifu,* akawaambia… (Mdo 4:8. Mkazo wa mwandishi).

Angalia sehemu ya sentensi "akijaa Roho Mtakatifu." Hii haikuwa mwanzo wa kujazwa Roho Mtakatifu kwa Petro kule kulikomjia siku ya Pentekoste. Hii ilikuwa ni uwepo wa Roho Mtakatifu aliyempaka upako ili azungumze katika nguvu za Roho. Ilikuwa ni utimilifu wa unabii wa Yesu katika Luka 12:11-12. Mfasiri wa Biblia Don Stamps anaandika kuhusiana na mstari huo: "Petro alipokea ujazo mpya wa Roho Mtakatifu uliomletea uvuvio mpya, hekima na ujasiri ambao kwa njia ya huo aliweza kuihubiri kweli ya Mungu."[18] Hivi ndivyo tunavyomaanisha tunapozungumzia kuhusu upako.

Baadaye siku hiyo hiyo, Petro na Yohana waliporudi kutoa ripoti, upako wa Roho Mtakatifu ukaja juu ya kikundi chote wakati walipokuwa wakiomba:

> Hata walipokwisha kumuomba Mungu, mahali pale walipokusanyika pakatikiswa, *wote wakajaa Roho Mtakatifu,* wakanena neno la Mungu kwa ujasiri (Mdo 4:31, mkazo wa mwandishi).

Tena wote walijazwa na, au kupakwa na Roho Mtakatifu. Hakuna wasiwasi ya kwamba huo ni upako wa Roho Mtakatifu unaozungumzwa katika mistari miwili ya baadaye:

> Na mitume wakatoa ushuhuda wa kufufuka kwake Yesu kwa nguvu nyingi na *neema nyingi ikawa juu yao wote* (Mdo 4:33, mkazo wa mwandishi).

"Neema nyingi [ikawa] juu yao wote," ikaleta matokeo ya "nguvu nyingi," jambo ambalo kwa mara nyingine lilikuwa ni upako wa Roho Mtakatifu.

Stefano alikuwa ni mtu "aliyejaa imani na Roho Mtakatifu" (Mdo 6:5). Katika Matendo 6 tunasoma kuhusu yeye kuwa amepakwa na Roho Mtakatifu:

---

[18]Don Stamps, *Full Life Study Bible, New Testament* (Deerfield FL: Life Publishers, 1990), tazama Matendo 4:8 uk. 236.

> Na Stefano akijaa *neema na uwezo,* alikuwa akifanya maajabu na ishara kubwa katikati ya watu … lakini hawakuweza kushindana na hiyo hekima na huyo *Roho aliyesema naye* (mistari 8, 10, mkazo wa mwandishi).

Watu waliweza hata kuuona upako wa Roho Mtakatifu usoni mwake alipokuwa akinena:

> Watu wote walioketi katika ile baraza wakamkazia macho yao wakamwona uso wake kuwa kama uso wa malaika (Mdo 6:15).

Ilikuwa ni upako wa Roho Mtakatifu uliomjia Paulo katika kisiwa cha Kipro akimdhihirishia hukumu ya Mungu ambayo ilikuwa imwangukie Elima, mchawi.

> Lakini Sauli, ambaye ndiye Paulo, *akijaa Roho Mtakatifu,* akamkazia macho, akasema, ewe mwenye kujaa hila na uovu wote, mwana wa ibilisi, adui wa haki yote, huachi kuzipotoa njia za Bwana zilizonyoka? Basi angalia mkono wa Bwana u juu yako, nawe utakuwa kipofu, usione jua kwa muda. Mara kiwi kikamwangukia na kiza, akazunguka-zunguka na kumtafuta mtu wa kumshika mkono na kumwongoza (Mdo 13:9-11, mkazo wa mwandishi).

Kama mtu akihitaji kuhudumu katika nguvu za Roho Mtakatifu kama wale wakristo wa kanisa la kwanza, yeye pia lazima ajifunze kutembea katika Roho na kuwa tayari kujitoa na kutii maongozo ya Roho kama vile anavyotaka.

Imani

Imani ni kiungo kingine cha muhimu katika huduma yenye nguvu. Imani imefafanuliwa katika njia nyingi. "Imani katika Kristo," anasema mmisionari mkongwe Hugh Jeter, "ni ujasiri katika Kristo. Ni kuamini ya kuwa yeye ndiye kama anavyosema mwenyewe, na atafanya yale anayosema atafanya … Imani yaweza kuwa mfu. Lakini imani nyakati zote hutenda kazi."[19] "Imani," anasema mwandishi mwingine "inamaanisha kwamba umeamini kile ambacho Mungu ameahidi, na kile unachoomba, ni chako, na kwamba umekipokea, (hata kabla

[19]Hugh Jeter, *By His Stripes* (Springfield, MO: Gospel Publishing House, 1977), Uk. 173.

hujakipokea, hata kabla hujakiona au kukipapasa)."[20] Kwa makusudi yetu tutafafanua imani kama uwezekano wa kumwamini Mungu kwa ajili ya miujiza. Imani ya jinsi hiyo huangalia kwa Mungu bila kuchoka ili atimize neno lake kwa ishara. Imani ya jinsi hiyo imeonyeshwa katika ujasiri wa Petro wakati, akimuona Yesu akitembea juu ya maji, alimwita,

> Bwana ikiwa ni wewe niamuru nije kwako juu ya maji. Akasema, njoo. Petro akashuka chomboni, akaenda kwa miguu juu ya maji, ili kumwendea Yesu (Mt 14:28-29).

Imani ya jinsi hii ilikuwa ni ule uchu wa Petro na Yohana wakati walipomwambia yule mtu mbele ya Mlango Mzuri "tuangalie" (Mdo 3:4). Walikuwa na kitu alichohitaji, na walikuwa na uchu wa kukitoa! Mtu anayehitaji kutumiwa katika huduma yenye nguvu lazima, kama Roho anavyoongoza, ahudumu katika nguvu ya upako wa Roho Mtakatifu.

Ujasiri

Ujasiri ni kujitoa, kuwa tayari, kudiriki kuchukua hatua ya imani, hata kama kudiriki kuchukua hatua hiyo ya imani kwaweza kuleta kushindwa na kuadhirika. Ujasiri wa jinsi hiyo umeonyeshwa katika huduma ya Paulo, wakati kule Lystra alidiriki kufanya kitendo ambacho kingeweza kumletea kushindwa na kuadhirika. Wakati alipokuwa akihubiri mbele ya kusanyiko la watu, Paulo alihisi moyoni mwake ya kwamba mtu mmoja kiwete, ambaye alikuwa hajawahi kutembea, alikuwa na imani ya kupona. Paulo akalia kwa sauti kuu, "Simama kwa miguu yako sawasawa, akasimama upesi akaenda" (Mdo 14:10).

Je! Ingekuwaje kama mtu huyu asingetembea? Paulo angeweza kuadhirika, na huduma yake labda ingeweza kuishia Lystra. Hata hivyo, Paulo alikuwa jasiri wa imani, alikuwa tayari kudiriki kushindwa, matokeo yake uamsho mkubwa ukatokea katika mji ule. Ujasiri wa jinsi hiyo unaweza kuja tu kutokana na kujitoa kwa Mungu, imani kuu katika neno lake na kujazwa na Roho Mtakatifu (Mdo 4:31).

Huduma yenye nguvu inahusisha sana uchukuaji wa hatua za jinsi hiyo.

---

[20]T. L. Osborn, *How to Receive Miracle Healing* (Nairobi: Evangel Publishing House, 1955), uk. 169.

Hatupewi uhakika kila wakati tunapoombea wagonjwa kuponywa au kila tunapokutana na mapambano dhidi ya nguvu za mapepo. Wale ambao kila wakati wanapenda kujiokoa na fedheha "kwa kujilinda" hawataweza kuwa na huduma madhubuti na yenye nguvu. Mafanikio yatakuja tu kwa wale watakaoamua kutenda kwa imani na ujasiri.

Kuongozwa na Roho Mtakatifu

Kuongozwa na Roho Mtakatifu ni jambo la nne muhimu katika huduma yenye nguvu. Kabla mtu hajahudumu kwa nguvu katika jambo lolote lazima kwanza apambanue mapenzi ya Mungu katika jambo hilo, akitambua ya kuwa Mungu hawezi kulibariki jambo lolote lililo nje ya mapenzi yake. Mhudumu wa Kipentekoste ni lazima nyakati zote ajiulize, "Je! Ni nini mapenzi ya Mungu katika jambo hili? Je! Mungu anahitaji atembee kwa namna gani? Je! Anafanya nini? Na Je nawezaje kujipanga sambamba na mapenzi yake?

Yesu mfano wetu mkuu katika huduma, nyakati zote alifanya mapenzi ya Baba yake. Kamwe hakuhudumu kwa mapenzi yake mwenyewe, bali nyakati zote alifuata mapenzi ya Baba yake wa mbinguni kwa njia ya Roho Mtakatifu aliyemjaza. Kwa uangalifu jaribu kufikiria kuhusu mambo yafuatayo katika huduma ya Yesu:

> Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe *ila lile ambalo amwona Baba analitenda, kwa maana yote ayatendayo yeye, ndiyo ayatendayo mwana vile vile.* Kwa maana Baba anampenda mwana, naye humwonyesha yote ayatendayo mwenyewe; hata na kazi kubwa zaidi kuliko hizo atamwonyesha (Yn 5:15-20).
>
> *Sifanyi neno kwa nafsi yangu, ila kama Baba alivyonifundisha* (Yn 8:28).
>
> Kwa sababu mimi sineni kwa nafsi yangu tu, bali Baba aliyenipeleka, yeye mwenyewe ameniagiza nitakayonena na nitakayosema… . basi *hayo ninenayo mimi kama Baba alivyoniambia, ndivyo ninenavyo* (Yn 12:49-50, mkazo wa mwandishi).

Je! Umeona jinsi ambavyo Yesu alisema tu na kufanya yale ambayo Baba alimwambia kusema au kuyafanya. Siku moja kando ya birika iitwayo Kiebrania Bethzatha, jamii kubwa ya wagonjwa walikuwa wamelala… . vipofu, viwete, nao waliopooza (Yn 5:4). Yesu alimponya mmoja wao (mstari 8). Je! Alimchaguaje huyo tu kumponya? Kutokana na rekodi (Yn 5:19-20), Yesu alimchagua huyo kwa sababu alikuwa akifuata maelekezo ya Baba yake wa mbinguni. Katika Roho alimwona alichokuwa akifanya Baba yake, na akafanya hivyo hivyo. Hiyo

ilikuwa ndiyo siri ya huduma yake kubwa ya uponyaji.

Kama nasi, kama Yesu, tutahitaji kuhudumu katika nguvu, lazima sisi pia tusikilize sauti ya Baba na tupambanue kwa uhakika ni nini anachokifanya? Ni nani anayetaka kumponya? Ni kwa jinsi gani anataka kumponya? Ni nini mwitikio wangu katika Roho katika jambo hili. Haya ndiyo maswali ambayo lazima yaulizwe na kujibiwa kama tutataka kuhudumu katika nguvu. Maswali haya yanaweza tu kujibiwa na Baba mwenyewe kwa njia ya Roho aliyetupa.

Mtu mmoja amesema, "Huduma ya nguvu ni nyepesi. Unalohitaji kulitenda ni kuisikia sauti ya Mungu na kuitii;" Hii ni kweli. Mara tukigundua Baba anafanya nini, linakuwa ni jambo la kujipanga na mipango yake. Tutajadili habari ya kuongozwa na Roho Mtakatifu zaidi katika Sura ya 7, "Kuongozwa na Roho Mtakatifu na Huduma yenye nguvu."

Unyenyekevu

Unyenyekevu ni uwezo wa kujiona kama vile Mungu atuonavyo, yaani kujiona kama vile tulivyo. Hili ni jambo la tano muhimu ambalo ni kiungo muhimu na cha mafanikio katika huduma yenye nguvu. Paulo anazungumzia hali hiyo katika Rum 12:3 asemapo, "Usinie makuu kupita inavyokupasa kunia, bali uwe na nia ya kiasi.…"

Anawataka waumini waishi maisha ya unyenyekevu, yaliyo
huru na kiburi, kule kujiona mtu wa maana: "Msitende neno lolote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake" (Fil 2:3).

Anayamalizia mafundisho yake kuhusu unyenyekevu anaposema, "Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu. . .." (Fil 2:5). Ndipo anapoendelea kuelezea tabia ya Yesu ambayo haikuwa na ubinafsi kabisa:

> Ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho. Bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya utumwa, akawa ana mfano wa wanadamu; tena alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba!" (Fil 2:6-8).

Hali hiyo ya unyenyekevu ni jambo la muhimu la tano la huduma yenye nguvu.

Jinsi mioyo yetu ilivyovunjwa tena na tena katika miaka hii yote tumekuwa

tukiona janga linalohusu watu ambao, kwanza walitumika na Mungu kwa namna kubwa, wakianguka kwa ajili ya roho ya kiburi. Wakisahau maonyo ya wazi ya maandiko, walianza kujiona na kujifikiria wenyewe kwa hali ya juu na hatimaye kuanguka kutokana na uzito wa kiburi chao. Ni kweli "Kiburi hutangulia maanguko" (Mith 16:18).

Nafikiria hakuna namna ya huduma ya Kikristo iliyojaa majaribu ya kiburi kuliko huduma yenye nguvu. Nguvu inalewesha, na ni rahisi kwa mtumishi anayetumiwa sana na Mungu kulewa na kile afikiriacho kuwa ni nguvu na mafanikio yake mwenyewe. Na ni mara nyingi watu wanakuwepo kumhakikishia umaarufu wake. Kwa kuiona miujiza aifanyayo, watu hufurahia kumheshimu kama vile ni mungu mdogo "wametushukia kwa mfano wa wanadamu!" (Mdo 14:11). Fedha na nafasi ya heshima huja kirahisi, na mara huanza kufikiria na kuamini kwamba baraka za Mungu ni kwa ajili yake. Mtumishi huyo huwa tayari kwa anguko kubwa.

Kuna sababu ya pili ambayo huwa ni sababu ya kuanguka kwa wengine. Maanguko haya kuwa siyo kwa ajili ya mafanikio ya huduma yenye nguvu, bali hutokea kwa kukosa mafanikio hayo. Kwa sababu wengine wanatamani mno kutumiwa na Mungu kwa namna kubwa au kwa sababu wanatamani sana kule kuonekana na watu kama watumishi wenye nguvu kubwa wanaighoshi kweli. Nyakati nyingine wanaanza kuinakili miujiza au kufanya mambo zaidi ya maandiko. Wanakuwa wako tayari kuridhika na jambo ambalo siyo halisi badala ya, kwa unyenyekevu kumtegemea Mungu kwa matendo ya kweli. Jinsi inavyohuzunisha na ilivyo janga kubwa.

Katika kuhudumu katika huduma yenye nguvu, tusije tukasahau ya kwamba nguvu yote ni ya Mungu na hivyo utukufu wote. Wakati wale sabini na wawili waliporudi kutoka kwenye huduma, walitoa ripoti kwa Yesu, "Bwana hata pepo wanatutii kwa jina lako" (Lk 10:17). Yesu alifurahi pamoja nao. Halafu akawapa onyo "Lakini msifurahi kwa vile pepo wanavyowatii; bali furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa mbinguni" (Mstari 20). Alikuwa anawaambia, "Msijiinue kwa yale mliyoyatenda kwa ajili ya Mungu, bali furahini kwa yale Mungu aliyowatendea." Unyenyekevu ni jambo muhimu kwa huduma yoyote ambayo itadumu katika miujiza.

MATAYARISHO YA HUDUMA YENYE NGUVU

Sasa tuangalie matayarisho ya binafsi kwa ajili ya huduma yenye nguvu. Kuna mambo matano hasa ambayo mtu lazima ayaangalie wakati wa maandalizi binafsi kwa ajili ya uinjilisti wenye nguvu.

Chunguza Nia Yako

Kwanza kabisa katika maandalizi ya huduma yenye nguvu mtu lazima ajichunguze mwenyewe ni kwa nini anataka kujihusisha na huduma ya jinsi hiyo. Jambo tulitendalo kwa ajili ya Mungu ni muhimu sana; *kwa nini* tunalitenda ni muhimu tena zaidi. Lazima tuwe na uhakika kuhusu nia zetu katika kutaka kutumika na Mungu katika huduma ya uinjilisti wenye nguvu. Katika Matendo, sura ya 8, Simoni yule mchawi aliitaka huduma yenye nguvu, lakini nia yake ya ndani haikuwa nzuri. Alitamani sana aonekane kuwa ni mtu mwenye nguvu, hata akawa yuko tayari kununua kwa gharama kipawa hicho. Petro akitambua nia zake mbaya, alimkemea akimwambia, "Huna fungu wala huna sehemu katika jambo hili, kwa kuwa sio moyo wako si mnyofu mbele za Mungu" (Mdo 8:21). Je! Ni wangapi leo pia wanahitaji huduma ya nguvu kutokana na nia mbaya?

Je! Ni nia gani mbaya au nzuri katika kutaka kujihusisha na huduma yenye nguvu? Nia mbaya ni pamoja na kiburi, tamaa ya kujinufaisha na kujiendeleza na hitaji la kutumia nguvu juu ya watu. Nia nzuri katika kutaka kujihusisha na huduma yenye nguvu ni pamoja na shauku ya kumtukuza Mungu, upendo na shauku ya kutaka kuwasaidia watu, na nia ya kuendeleza ufalme wa Mungu duniani.

Imarisha Uhusiano wako na Mungu

Jambo la pili ambalo mtumishi anahitaji alifanye katika matayarisho kwa ajili ya huduma ya miujiza ni kuimarisha uhusiano wake na Mungu. Lazima atambue kwamba anaweza tu kuhudumu kwa uhakika kutokana na uhusiano mzuri na Mungu. Lazima atambue ya kwamba kamwe huduma yake haitaweza kuwa na nguvu kuliko mshikamano alionao na Mungu. Kama tulivyokwisha kuona awali katika sura hii, Yesu mwenyewe alihudumu kutokana na uhusiano wake na Baba. Je! Unakumbuka Yesu alisemaje? "Kwa kuwa Baba ampenda mwana, naye humwonyesha yote ayatendayo" (Yn 5:20). Ilitokana na uhusiano huu wa upendo na Baba yake kwamba huduma ya Yesu ilitendeka. Katika hali hiyo hiyo, manabii walihudumu kutokana na ushirika wao na Yesu, na pia na Baba, kwa kuwa Biblia yasema kwamba watu "wakawatambua ya kwamba walikuwa

pamoja na Yesu" (Mdo 4:13). Endapo unatamani kutumika na Mungu katika huduma ya uinjilisti wenye nguvu, wewe pia, kama Yesu na mitume, lazima utumie muda wa kutosha kuimarisha uhusiano wako na Mungu kwa njia ya maombi, kusoma maandiko na kuyatafakari, na kujitoa kabisa ili kufuata mapenzi yake.

Ongeza Ufahamu Wako

Njia ya tatu ya kujiandaa binafsi kwa ajili ya huduma ya miujiza ni kuongeza ufahamu wako kuhusu somo hili. Kusoma na kuitumia misingi iliyomo katika kitabu hiki ni njia ya kwanza nzuri katika kuongeza ufahamu, lakini hii ni mwanzo tu. Hapa kuna njia nyingine ambazo unaweza kuongeza ufahamu kuhusu huduma ya kimaandiko yenye nguvu.

1) Kutoka katika Agano Jipya soma na kusoma tena vitabu vya Injili na Matendo ya mitume. Mwandishi huyu anaweza kushuhudia kutokana na ujuzi wake binafsi kuhusu jambo hili ya kwamba, ukamilifu wa kusoma kimpangilio, kusoma tena na tena, kwa vitabu hivi kunaweza kabisa kuyabadilisha maisha yako. Kumefanya hivyo kwake. Wakati mmoja mhudumu mkongwe aliyekuwa akitumika sana katika huduma za uponyaji na kutoa pepo aliulizwa na mtumishi kijana, "Je! Unaweza kunielekeza vitabu vyovyote vizuri katika somo la uponyaji?" "Ndio" alijibu yule mzee, "Naweza kukuelekeza vitabu vinne vya ajabu sana." Kusikia hivyo yule kijana alitoa karatasi na kalamu tayari kuandika. "Je! Ni vipi hivyo vitabu vinne vya ajabu?" aliuliza, "Lazima nivipate." Mhubiri yule mkongwe alijibu, "Mathayo, Marko, Luka na Yohana." Fanya mazoezi ya kusoma na kusoma tena vitabu vinne vya Injili na Matendo ya mitume, wakati wote ukijiuliza maswali kama, "Je! Yesu na mitume walihudumu vipi katika nguvu? Je! Waliwaponyaje wagonjwa na kutoa pepo? Ni nini ilikuwa siri ya mafanikio yao? Je! Ninawezaje kuiga maisha na huduma zao?"

2) Pia unaweza kusoma vitabu ambavyo vina masomo ya jinsi hiyo vilivyoandikwa na watumishi wa Mungu wengine mashuhuri. Lakini angalia: Siyo kila kitabu kilichoandikwa kuhusu somo hili kina misingi sahihi ya Biblia, wala si kwamba waandishi wote wa vitabu vya jinsi hiyo ni watumishi wenye sifa njema na heshima.

Utii

Nne, lazima ujiandae kwa ajili ya huduma yenye nguvu kwa kutii na kufuata mapenzi ya Mungu. Yesu alijitiisha mwenyewe chini ya mapenzi ya Baba yake wa mbinguni, na akapokea baraka za Baba yake. Sisi pia, kama tutahitaji

kupokea baraka za Mungu, lazima tutii na tujitiishe wenyewe chini ya mapenzi yake. Lazima tusisahau:Mungu atatoa upako kwa mipango yake tu, pia ameahidi kulithibitisha neno lake kwa ishara zifuatanazo nalo (Mk 16:15-20).

Pata Uzoefu

Hatimate, endapo unahitaji kuhusika na huduma ya uinjilisti yenye nguvu, lazima upate uzoefu -- wote wa kiroho na wa kiutendaji.

1. Uzoefu wa kiroho. Uzoefu wa kiroho lazima uhusishe kuzaliwa mara ya pili (Yn 3:3-7). Biblia inatuambia habari ya watu waliojaribu kufanya huduma yenye nguvu pasipo kuwa wamezaliwa mara ya pili:

> Baadhi ya wayahudi wenye kutanga-tanga, nao ni wapunga pepo, wakajaribu kutaja jina la Bwana Yesu juu yao waliopagawa na pepo wachafu wakisema, 'Nawaapisha kwa Yesu, yule anayehubiriwa na Paulo. Walikuwako wana saba wa mtu mmoja Skewa, myahudi, kuhani mkuu, waliofanya hivyo. Yule pepo mchafu akawajibu, akawaambia, Yesu namjua na Paulo namfahamu, lakini ninyi ni nani? Na yule mtu aliyepagawa pepo mchafu akawarukia wawili, akawaweza, akawashinda, hata wakatoka mbio katika nyumba ile hali wa uchi na kujeruhiwa. (Mdo 19:13-16)

Habari hii na iwe kama onyo kwa wale wanaotaka kujihusisha na huduma yenye nguvu pasipo kuzaliwa mara ya pili.

Pia, ili kuhudumu katika nguvu mtu lazima ajazwe na Roho kama walivyokuwa wale mitume wa karne ya kwanza (Mdo 2:4). Ubatizo wa Roho Mtakatifu ulikuwa ndiyo chimbuko la nguvu ya ajabu ya kiroho katika kanisa la Matendo, na unabakia kuwa chanzo cha kiroho kwetu pia. Tutajadili kuhusu utendaji wa nguvu hii katika sura ya 6, "Roho Mtakatifu na huduma yenye nguvu."

2. Uzoefu wa kiutendaji. Kama ilivyo katika kazi yoyote, ujuzi katika huduma ya nguvu hupatikana kwa kupitia uzoefu wa kiutendaji. Mtu anayehitaji kuwa mzoefu katika eneo la huduma hii, lazima afanye hivyo kwa kupitia mazoezi halisi ya kiutendaji. Uzoefu huu unapatikana kwa ubora zaidi, kwa kufanya na mhudumu mwenye uzoefu. Hivi ndivyo wale thenashara, chini ya uongozi wa Yesu, walivyopata uzoefu. Jinsi tunavyojihusisha katika huduma yenye nguvu na kujizoeza katika vyote, mafanikio na kushindwa, tunajifunza zaidi kuwa wahudumu hodari wa Kristo.

MWISHO

Kama hitimisho, yeyote anayetaka kutumika katika huduma yenye nguvu lazima atilie maanani kweli kweli kuhusu matayarisho yake binafsi. Asisahau ya kuwa tunahudumu, si kwa njia ya nguvu zetu, bali kutokana na nguvu zitokazo kwa Mungu.

— Sura ya Sita —

Roho Mtakatifu Na Huduma Yenye Nguvu

Kabla mtu hajahusika na huduma yenye nguvu, ni lazima afahamu na abatizwe na Roho Mtakatifu. Hii ni kawaida kwa wakristo (wote katika Agano Jipya na pia leo), na ndiyo chanzo cha nguvu za kiroho katika maisha ya mtu na katika huduma. Katika somo hili tutaangalia swala hili. Pia tutaangalia karama za Roho Mtakatifu jinsi zinavyohusiana na huduma yenye nguvu.

UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU NA HUDUMA YENYE NGUVU

Ubatizo wa Roho Mtakatifu Umefafanuliwa

Tunaweza kusema mambo mengi kuhusu kufafanua maana ya ubatizo wa Roho Mtakatifu; hata hivyo, tutataja mambo matano tu:

1. Lengu kuu la utume wa Kristo duniani. Kulingana na mfafanuzi wa Biblia, Don Stamps, "moja ya lengo kuu la huduma ya Yesu duniani lilikuwa ni kuwabatiza wafuasi wake katika Roho Mtakatifu."[21] Kutokea mwanzo mpango wa Yesu haukuwa tu kupata wafuasi, ili kuwa na kundi lionekanalo mbele za watu. Mpango wake ulikuwa kuushinda ulimwengu, kwa kutumia watu waliofundishwa vema na kupewa zana. Zana hizo ni Roho Mtakatifu. Yohana Mbatizaji mwanzoni mwa huduma ya Yesu alisema, "Yeye ambaye utamwona Roho akishuka na kukaa juu yake, huyo ndiye abatizaye kwa Roho Mtakatifu" (Yn 1:33). Kwa hiyo kutokea mwanzo Yesu aliamua kuwabatiza wafuasi wake

[21]Don Stamps, "Baptism in the Holy Spirit," *Full Life Study Bible New Testament,* uk. 228.

kwa Roho Mtakatifu. Lilikuwa ndilo lengo la huduma yake.

2. Kuzamishwa na kujazwa na Roho Mtakatifu. Ubatizo wa Roho Mtakatifu unaweza kuelezwa kuwa ni kuzamishwa, na kujazwa, na Roho Mtakatifu. Katika Matendo 1:4-5 Yesu aliita kitendo cha ubatizo ni kuzamishwa katika Roho Mtakatifu:

> Hata alipokuwa amekutana nao aliwaagiza wasitoke Yerusalem, bali waingoje ahadi ya Baba, ambayo mlisikia habari zake kwangu; ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi *mtabatizwa na [kuzamishwa ndani ya] Roho Mtakatifu* (mkazo wa mwandishi).

Siku kumi baadaye, siku ya Pentekoste, Roho akaja. Biblia inasema ya kwamba wote wakajazwa Roho Mtakatifu:

> Wote *wakajazwa Roho Mtakatifu,* wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka (Mdo 2:4, mkazo wa mwandishi).

Kama chombo kilicho wazi kinaweza wakati huo huo, kuzamishwa na kujazwa na maji, ndivyo ilivyokuwa kwa wakristo hao siku ya Pentekoste. Na ndivyo inavyoweza kuwa kwa watu wote wa Mungu.

3. Utendaji wa Roho Mtakatifu katika kumbatiza mtu ni tofauti na ni pekee na kule kumzaa mtu upya kiroho. Ubatizo wa Roho Mtakatifu hautendeki wakati sambamba na wokovu kama watu kadha wanavyotaka tuamini. Ni utendaji wa tofauti na pekee kutoka kile kitendo cha awali cha wokovu. Kama vile wale thenashara walivyookoka kwanza (Yn 20:22), na baadaye wakajazwa na Roho Mtakatifu (Mdo 2:4). Pia kama watu wa Samaria walivyookoka kwanza (Mdo 8:12, 14), na baadaye "wakampokea Roho Mtakatifu" (Mdo 8:17), ndivyo ilivyo kwetu leo. Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni utendaji wa Roho Mtakatifu katika maisha ya mkristo tofauti na pekee na kuzaliwa mara ya pili.

Je! Umezaliwa mara ya pili? Je! Wewe u mwana wa Mungu? Kama ndivyo, basi unaweza kutafuta kujazwa na Roho Mtakatifu kama ilivyokuwa kwa wakristo wa kanisa la karne ya kwanza.

4. Kuvikwa uweza utokao juu. Katika Luka 24:49 Yesu alielezea ubatizo katika Roho Mtakatifu kama "kuvikwa" na nguvu kutoka juu: "Na tazama nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uweza utokao juu."

Picha Yesu anayoionyesha hapa ni ile ya mtu anayevikwa na nguvu za Mungu, na akiisha kuvikwa, yuko tayari kufanya kazi ya Mungu. Yesu aliahidi

wazi nguvu kama hiyo kwa wafuasi wake baada ya Roho Mtakatifu kuwajilia juu yao. "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia Roho Mtakatifu juu yenu" (Mdo 1:8). Neno la kiyunani hapa lililotafsiriwa "kuwajilia juu yenu" (eperchomai) ni neno lilelile lililotumika katika Luka 1:35 likielezea Roho Mtakatifu kuja juu ya Maria kabla ya kuzaliwa Yesu: "Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake aliye juu zitakufunika" (Lk 1:35).

Ni wazi maana yake hapa, kama katika Matendo 1:8 ni ya kuzungukwa kabisa, nakuzingirwa kabisa kwa nguvu za Mungu. Ndivyo inavyotokea kwa mkristo aliyebatizwa katika Roho Mtakatifu.

5. Ahadi ya wakristo wote walioamini. Kila mkristo aliyezaliwa mara ya pili, anaweza na anatakiwa kubatizwa katika Roho Mtakatifu. Kuhusu wale 120 waliokusanyika siku ya Pentekoste, Biblia inasema "wote walijazwa Roho Mtakatifu." Haisemi ya kuwa 119 walijazwa, na mmoja hakujazwa. Inasema wote walijazwa.

Kutokea mwanzo Mungu alitaka tuyafahamu mapenzi yake kuhusu swala la kubatizwa na Roho Mtakatifu. Ni mapenzi yake kuwa kila mtu aliyeamini ajazwe na Roho Mtakatifu. Petro aliweka jambo hili wazi aliposimama siku ya Pentekoste akasema kuhusu "Karama ya Roho Mtakatifu": "Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali na kwa wale watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie" (Mdo 2:39).

Kwa hiyo ahadi ya ubatizo katika Roho Mtakatifu, na nguvu ambazo zinaletwa na ubatizo huo, ni kwa "wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Hii inamaanisha, rafiki yangu, kuwa ahadi hiyo ni kwa ajili yako pia. Je! Unaweza kumwita Bwana leo, na kumuomba akujaze na Roho wake Mtakatifu?

Umuhimu wa Ubatizo wa Roho Mtakatifu Katika Huduma yenye Nguvu

Hata kama ni jambo la wazi, lakini tutalisema hata hivyo: Kabala ya kuingia katika huduma ya uinjilisti wenye nguvu, ni lazima kujazwa na nguvu za Roho Mtakatifu. Ujazo huo wa nguvu huja kwa njia ya ubatizo katika Roho Mtakatifu ambao tumekuwa tukijadili (angalia Mdo 1:8). Umuhimu wa jambo hili katika huduma yenye nguvu umeonyeshwa katika njia mbili:

1. Ubatizo katika Roho Mtakatifu ni agizo katika maandiko. Kwanza, umuhimu wa ubatizo katika Roho Mtakatifu ni jambo dhahiri kwa sababu ni agizo kutokana na maandiko. Katika barua yake kwa wakristo wa Efeso, Paulo anawaagiza waumini hao maagizo mawili. Tunategemea kuyatii yote: "Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho" (Efe 5:18).

Katika agizo lake la mwisho kwa wanafunzi wake kabla ya kupaa kwake

kwenda mbinguni, Yesu aliwaagiza kujazwa na Roho, (Mdo 1:4-5). Wakati wa siku zake arobaini baada ya kufufuka, Yesu aliwaagiza wafuasi wake wasianze kushuhudia watu hadi watakapokuwa wamebatizwa katika Roho Mtakatifu (Lk 24:49; Mdo 1:4, 5, 8). Yesu alielewa wazi ya kwamba huduma aliyowaitia wanafunzi wake ilikuwa ni kubwa kuliko uwezo wa kibinadamu. Walihitajika wasithubutu kuifanya kwa nguvu zao wenyewe. Lazima kwanza "wavikwe na uweza utokao juu."

Jambo hilo ni kweli hata leo. Kabla hatujajaribu kuingia katika huduma yoyote, zaidi huduma yenye nguvu, sisi pia lazima tujazwe nguvu za Roho Mtakatifu. Tutakuwa ni wajinga endapo tutawaza vinginevyo!

2. Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni chimbuko letu la nguvu. Umuhimu wa ubatizo wa Roho Mtakatifu katika huduma ya nguvu pia unadhihirika kwa sababu Roho Mtakatifu ni chimbuko letu la nguvu za huduma ya jinsi hiyo. Ilikuwa hivyo kwa wote, Yesu na kanisa la kwanza, na ndivyo ilivyo kwetu leo.

Nguvu ya Yesu kwa ajili ya huduma ilikuja kwa ajili ya upako wa Roho Mtakatifu. Upako huo kwanza ulitokea wakati wa ubatizo wake katika mto Yordani (Lk 4:22). Ilikuwa hadi baada ya kupakwa mafuta na Roho Mtakatifu ndipo alipoingia katika huduma yake ya umasihi. Sikiliza maneno haya ya mtume Petro kuhusu huduma ya Yesu:

> Habari za Yesu wa Nazareti, jinsi Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu; naye akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na ibilisi; kwa maana Mungu alikuwa pamoja naye (Mdo 10:38).

Ingawa tunaamini kwa uthabiti ya kwamba Yesu alikuwa, na hakuisha kuwa mwana wa Mungu wa milele, pia tunajua ya kwamba alipokuwepo hapa duniani, aliamua kuhudumu chini ya upako wa Roho Mtakatifu. Alifanya hivi ili aweke ramani ya huduma kwa ajili yetu kuifuata.

Ni muhimu kutambua ya kwamba Yesu hakuweza kumponya hata mgonjwa mmoja, hakutoa hata pepo mmoja, wala hakufanya muujiza wowote hadi alipokwisha kupakwa mafuta ya Roho Mtakatifu wakati wa ubatizo wake. Hata hivyo, baada ya upako wake na Roho, mara moja alianza kuhudumu sehemu mbalimbali katika nguvu. Usomaji wa uangalifu wa mistari ifuatayo kutoka katika injili ya Luka utaelezea kwa wazi jambo hili: Lk 4:1-2; 4:14; 18:21, 5:17; 6:19. Kama upako huo wa Roho ulikuwa ni wa muhimu kwa Yesu katika kuitenda huduma yake, si zaidi utakuwa ni wa muhimu kwetu pia leo!

Ni wazi pia kutokana na usomaji wa kitabu cha Matendo, ya kwamba ubatizo wa Roho Mtakatifu ulikuwa ni msingi wa huduma ya kanisa la Agano Jipya.

Kitabu hiki cha Agano Jipya kinarudia tena na tena kusisitiza ya kuwa ubatizo wa Roho Mtakatifu ni zawadi ya Mungu kwa kanisa. Zawadi hii imetolewa kwa kanisa ili lipate kuiendeleza kazi ya Yesu na ili kanisa tilimize utume wake wa kupeleka injili hadi miisho ya nchi (Mdo 1:8).

Karibu sehemu kama sita katika Matendo tunaambiwa kuhusu watu kubatizwa, au kujazwa na Roho (Mdo 2:4; 4:33; 8:17; 9:17-18; 10:44-46; 19:6). Matendo makuu ya nguvu za Mungu yaliambatana na kumwagwa huko kwa Roho Mtakatifu na matokeo yake kuingizwa kwa idadi kubwa ya watu katika ufalme wa Mungu. Pia tunaona katika Matendo ya kwamba upako uliofuatana na vitendo hivyo vya kubatizwa na Roho ilikuwa ndiyo chanzo cha nguvu ya miujiza katika kanisa. Ilikuwa ni baada ya kumwaga kwa Roho (Mdo 4:31) kwamba tunapata rekodi hii, "Na mitume wakatoa ushuhuda wa kufufuka kwake Yesu kwa nguvu nyingi, na neema nyingi ikawa juu yao wote" (Mdo 4:33).

Kwa hiyo, unaona ya kuwa Roho Mtakatifu alikuwa chanzo cha nguvu kote katika huduma ya Yesu na ya kanisa la Agano Jipya. Kwa walrostp wa kitabu cha Matendo ya mitume nguvu hii ilikuwa ni matokeo ya kubatizwa kwa Roho Mtakatifu. Nguvu kama hiyo ingalipo leo pia kwetu endapo sisi pia tutajazwa na Roho.

Je! Unawezaje Kupokea Roho Mtakatifu Leo

Katika sehemu hii ya somo letu swali linaibuka, "Je! ni kwa jinsi gani tunaweza kubatizwa na Roho Mtakatifu leo:" Ni matumaini yetu ya kwamba baada ya kusoma maelekezo haya rahisi, utapokea karama iliyoahidiwa ya Roho Mtakatifu.

1. Masharti ya upokeaji wa Roho Mtakatifu. Yako masharti mawili muhimu kabla mtu hajabatizwa na Roho Mtakatifu. Kabla mtu hajajazwa na Roho Mtakatifu (1) ni lazima awe amezaliwa mara ya pili kweli kweli, na (2) ni lazima yeye mwenyewe awe na shauku ya kujazwa na Roho.

a. Kuzaliwa upya. Biblia inafundisha waziwazi ya kwamba kabla mtu hajabatizwa na Roho Mtakatifu ni lazima awe amezaliwa mara ya pili. Yesu mwenyewe alituambia "ulimwengu hauwezi kumpokea" Roho wa kweli, yaani, Roho Mtakatifu, "kwa kuwa haumwoni wala haumtambui" (Yn 14:17). Ni wale tu ambao kweli wamezaliwa kwa Roho wa Mungu (Yn 3:5-17) ndio wanaoweza kumpokea Roho Mtakatifu. Jambo hili linahusu imani binafsi katika Yesu Kristo kama mwokozi, kujitoa na kutumainia kabisa mapenzi ya Mungu na toba, ambayo ni kule kugeuka kutokana na jambo lolote linalomuudhi Mungu. Je! Umezaliwa mara ya pili kweli kweli? Kama bado, kwa nini usimgeukie Kristo sasa hivi katika imani na toba.

b. Shauku ya kujazwa. Sharti la pili muhimu kabla ya kubatizwa na Roho Mtakatifu ni ile shauku ya kujazwa. Yesu alisema, "Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana hao watashibishwa" (Mt 5:6). Watashibishwa na nini? Watashibishwa na haki ya Mungu ambayo huja kwa utakaso wa Roho mtakatifu (1Kor 6:11, Rum 16:15). Ili kujazwa na Roho mtu ni lazima awe na shauku na Mungu kuliko vitu vyote. Yesu bado anatuita, "Mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe. . ." (Yn 7:37). Je! Unayo kiu kwa ajili ya Mungu? Kama ndivyo, basi umekutana na jambo la pili muhimu kabla ya kujazwa Roho Mtakatifu.

2. Jinsi unavyoweza kumpokea Roho Mtakatifu. Sasa, kama utahitaji kujazwa na Roho Mtakatifu, fanya mambo haya matatu:

a. Mwombe Mungu ili ujazwe na Roho Mtakatifu leo. Yesu amekwisha kutupatia ahadi ya ajabu ya kumpokea Roho. Sikiliza manene yake: *"kwa kuwa kila aombaye hupewa!"* (Lk.11:10). Je! Umesikia tamko hilo? *Kila* aombaye hupewa. Sasa sikiliza maneno haya tena:

> Basi ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vilivyo vyema, Je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao! (Mstari 13).

Je! Unahitaji Mungu akujaze na Roho Mtakatifu? Mwombe tu sasa; Yeye yuko tayari kukujaza leo.

b. Karibia "kiti cha neema" kwa ujasiri. Ujapo kujazwa na Roho Mtakatifu yakubidi ukaribie kiti cha neema kwa ujasiri. Maandiko yanatuambia, "basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri" (Ebr 4:16). Tunaweza kuja mbele za Mungu bila woga tukiwa tumejaa ujasiri kwa sababu tunajua ya kuwa tunakuja sawa sawa na mapenzi yake. Unapokuja kujazwa na Roho Mtakatifu, uje kwa ujasiri ukifahamu ya kuwa Mungu anakukaribisha katika uwepo wake.

c. Msifu Mungu kwa imani yenye tumaini. Sasa anza kumsifu Mungu kwa moyo wako wote, na ufanyapo hivyo tegemea ya kwamba atakujaza kwa Roho Mtakatifu. Hili ndilo wale 120 walilofanya kabla ya siku ya Pentekoste. Biblia inasema, "Nao walikuwa daima ndani ya hekalu, wakimsifu Mungu" (Lk 24:53). Waangaliaji walipoona ya kuwa wale 120 wamejazwa Roho katika siku ya Pentekoste, waliwasikia wakimsifu Mungu katika lugha zao, sikiliza maneno yao: "tunawasikia hawa wakisema kwa lugha zetu matendo makuu ya Mungu!" (Mdo 2:11). Unatakiwa kufanya vile vile kama mitume wa kwanza. Msifu Mungu kwa moyo wote. Unapomsifu, fanya hivyo kwa imani yenye matumaini. Unapoendelea kumuabudu, tegemea ya kuwa Mungu atatimiza ahadi yake. Mtegemee kukujaza na Roho Mtakatifu. Na utegemee kunena kwa lugha kama

Roho atakavyokuwezesha!

3. Ushahidi wa Kubatizwa kwa Roho Mtakatifu. Ukiisha tu kujazwa na Roho hutakuwa kamwe mtu yule yule tena. Tegemea ishara nyingine kufuatia kujazwa kwako.

a. Ishara ya kwanza. Ishara ya kwanza ya kujazwa kwako na Roho Mtakatifu itakuwa ni kunena kwa lugha nyingine kama Roho atakavyokuwezesha (Mdo 2:4). Hii ilikuwa ndio ishara iliyotokea mara kwa mara kwa waumini katika kitabu cha Matendo, na ndiyo "ishara ya awali" ya kubatizwa na Roho Mtakatifu. Soma mwenyewe Biblia katika Matendo ya mitume 2:1-4; 10:47-47; na 19:1-6. Utajua wazi utakapojazwa na Roho, kwa sababu utaanza kunena kwa lugha nyingine!

b. Ushahidi mwingine wa kimaandiko unaohusiana na huduma yenye nguvu. Jinsi unavyoendelea kujifunza kutembea katika Roho ishara za namna nyingi zitafuata. Chini nimeandika namna nane zinazohusiana na huduma ya uinjilisti wenye nguvu:[22]

- Nguvu ya kuwa shahidi (Mdo 1:8)
- Ujasiri (Mdo 2:14-41; 4:31)
- Nguvu ya kufanya kazi za Yesu (Yn 14:16; 16:14)
- Udhihirisho wa huduma mbalimbali za Roho (1Kor 12:1-11)
- Kuongezeka kwa hisia kutambua dhambi zinazomhuzunisha Roho Mtakatifu (Yn 16:7-11)
- Shauku kubwa na uwezo wa kuomba na kuombea wengine (Rum 8:26-29)
- Kuongezeka kwa ufahamu wa kutambua uwepo wa Mungu katika maisha (Yn 14:16-18)
- Upendo mkuu kwa Mungu na kwa watu (Rum 5:5).

KARAMA ZA ROHO NA HUDUMA YENYE NGUVU

Ufahamu sahihi wa karama za rohoni na hasa karama tisa za rohoni (au "udhihirisho wa Roho") zilizoorodheshwa katika 1Kor 12:8-10 ni muhimu kwa

[22]Kuna ishara nyingine nyingi au matokeo ya kujazwa na Roho wa Mungu. Hapa tunataja zile tu zinazohusiana moja kwa moja na huduma yenye nguvu.

huduma yenye nguvu. Tutatoa dibaji fupi kwa ajili ya karama hizo na sehemu yake katika huduma yenye nguvu.

Karama za Roho Zimefafanuliwa

Karama za Roho zimefafanuliwa katika njia mbalimbali. Kwa ajili ya kusudi letu tutatumia maelezo yafuatayo: *Karama za Roho ni upako wa kimiujiza waliopewa wakristo waliojazwa Roho Mtakatifu ili kulitimiza kusudi la Baba.* Hebu tuchukue muda mfupi kuchunguza ufafanuzi wa sentensi hii kipengele kwa kipengele.

Kwanza, tumesema karama za Roho ni *"upako wa kimiujiza."* Kwa hili tuna maana ya kuwa karama za Roho zina chimbuko, si katika uwezo wa mwanadamu, bali katika Roho wa Mungu. Huja kama "upako". Kwa maneno mengine zinatenndeka chini ya upako wa Roho Mtakatifu, na karama zinatolewa wakati Roho anapotembea juu ya mtu aliyejitoa maisha yake kwa Bwana.

Pia tulisema katika ufafanuzi wetu, ya kwamba karama za Roho *"zinapewa kwa wakristo waliojazwa na Roho Mtakatifu."* Hizi ni "karama," kwa hiyo zinatolewa si kwa ushindi au tuzo fulani, bali kama utoaji tu wa neema ya Mungu ya bure. Tusemapo zinatolewa, hatuna maana ya kwamba zinatolewa kama mali ya kuhodhi binafsi bali tuna maana zinatolewa kwa watu binafsi ili kutimiza mahitaji kadha wa kadha kulingana na kazi ya Mungu. Zinatolewa kupitia wakristo "waliojazwa na Roho". Kwa kusema wakristo waliojazwa na Roho tuna maana wale waliobatizwa na Roho Mtakatifu (Mdo 2:4) na wanaendelea kutembea "katika Roho" (Ga 5:25).

Ufafanuzi wetu pia unasema ya kwamba karama za Roho zinatolewa *"na Roho Mtakatifu.*" Ni Roho Mtakatifu ndiye mtoaji wa karama hizi (1Kor 12:4-6), na zinatenda kazi, si kutokana na mapenzi ya mtu, bali kutokana na mapenzi ya Roho (1Kor 12:11). Sababu ambayo karama zinatolewa na Mungu si kwa ajili ya kutimiza mipango na mapenzi ya mtu yeyote. Zinatolewa ili *"kutimiza mapenzi ya Baba"* na kuendeleza ufalme wake duniani.

Karama za Roho zimetambuliwa

Sasa tutaangalia kwa karibu katika 1Wakorintho 12:7-10 na tutazitambua zile "karama" tisa za Roho zilizoorodheshwa. Wakati tukitambua ya kwamba kuna orodha nne zingine za karama za Roho katika barua za Paulo (kama Rum 12:6-8; 1Kor 12:28; 1Kor 12:29-30, Efe 4:11), pia tunaamini ya kwamba karama hizi tisa zina sehemu ya kipekee kabisa katika huduma ya uinjilisti wenye nguvu. Hebu na tuangalie basi karama hizi:

Karama Tisa za Roho (1Kor.12:7-11)

1. Karama za Mafunuo

(Zimetolewa ili kutambua mawazo ya Mungu)

- Neno la Maarifa — ufunuo wa kimuujiza wa ufahamu wa Mungu
- Neno la Hekima — ufunuo wa kimuujiza wa hekima ya Mungu
- Kupambanua Roho — ufunuo wa kimuujiza wa kutambua ni roho gani anayejidhihirisha au ni roho gani aliye nyuma ya tendo fulani.

2. Karama Unabii

(Zimetolewa ili kuyanena maneno ya Mungu)

- Karama ya Unabii — kunena kwa muujiza ujumbe utokao kwa Mungu katika lugha ijulikanayo na mzungumzaji.
- Karama ya aina za Lugha — kunena kwa muujiza ujumbe au sala kutoka kwa Mungu katika lugha isiyoeleweka na mzungumzaji.
- Karama ya Tafsiri za Lugha — kunena kwa muujiza maana ya ujumbe uliotolewa kwa lugha.

3. Karama za Nguvu

(Zimetolewa ili kuzitenda kazi za Mungu)

- Karama za Kuponya — uponyaji wa magonjwa kimiujiza
- Karama ya Imani — msukumo wa kimuujiza wa imani ili kuitimiza kazi fulani ambayo imetolewa na Mungu
- Karama ya Matendo kaziya miujiza[23] — tokeo la nguvu ya kimiujiza ili kuitimiza ya Mungu

[23]Karama hii ingeweza kuitwa “kazi za nguvu” au kwa Kiebrania (Greek: *energemata dunameon*) “utendaji wa kazi za nguvu.”

> Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana. Maana mtu mmoja kwa Roho apewa neno la hekima na mwingine neno la maarifa, apendavyo Roho yeye yule; mwingine imani kwa Roho yeye yule; na mwingine karama za kuponya katika Ruho yule mmoja; na mwingine matendo ya miujiza, na mwingine unabii, na mwingine kupambanua Roho; mwingine aina za lugha, na mwingine tafsiri za lugha. (1Kor 12:7-10)

Karama hizi tisa zinaelekea kujipanga kiasili katika makusudi matatu. Kundi la kwanza tunaliita *"karama za mafunuo."* Karama hizi za mafunuo zimepewa "ili kusudi tupate kuyatambua mawazo ya Mungu." Paulo anaita karama hizi tatu kama neno la maarifa, neno la hekima, na kupambanua Roho. Kundi la pili tunaliita *"karama na unabii."* Hizi zimepewa "ili tuweze kunena maneno ya Mungu." Karama hizi zinajumuisha, karama ya unabii, karama ya aina za lugha, na tafrisi za lugha. Kundi la tatu tunaliita *"karama za nguvu."* Hizi zimetolewa "ili tupate kuzitenda kazi za Mungu." Hizi tatu ni karama za kuponya, karama ya imani, na matendo ya miujiza (au kazi za nguvu). Hebu sasa tujaribu kufafanua kila karama mojawapo katika karama hizi.

Karama za Roho na Huduma yenye Nguvu

Tujadili sasa ni jinsi gani karama hizi zinahusiana na huduma ya nguvu.

1. Karama za Mafunuo na huduma yenye nguvu (Zimetolewa ili kutambua mawazo ya Mungu). Karama za mafunuo ni muhimu katika huduma yenye nguvu. Katika Matendo ilikuwa hasa neno la Maarifa, au kupambanua roho, ambavyo vilianzisha mlolongo wa matokeo yaliyofanya hatimaye karama ya nguvu itokee (angalia Mdo 14:8-10; 16:16-18). Kabla hatujafanya kazi za Mungu ni lazima tujue mawazo ya Mungu, hii ina maana, ni lazima tutambue yakini ni nini mapenzi ya Mungu katika swala fulani tunalolishughulikia. Yesu mwenyewe hakuenda tu ovyo akiponya wagonjwa. Kila wakati alisikia kutoka kwa Baba yake wa mbinguni. Sikiliza vizuri maneno yake: "Mwana hawezi kutenda neno lolote mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda; kwa maana yote ayatendayo yeye, ndiyo ayatendayo mwana vile vile" (Yn 5:19).

Yesu hakufanya lolote pasipo kwanza kuyajua mapenzi ya Baba yake kuhusiana na jambo lalote. Vi vyo hivyo, ni muhimu kwanza tupokee ufunuo wa Mungu kuhusiana na jambo tulilonalo.

Ni muhimu sana pia kwamba karama ya kupambanua Roho itendeke mwanza kabla hatujajua jinsi ya kuiendea huduma fulani ya uponyaji. Ni lazima kwanza tutambue siyo tu endapo mtu ni mgonjwa, bali pia ni kwa nini ni mgonjwa. Je! Ugonjwa huo umeletwa na matatizo ya asili au umesababishwa na uonevu wa

mapepo? Kuna habari iliyosimuliwa inayomhusu Smith Wigglesworth, ambaye alikuwa akiombea watu wawili viziwi. Kwa yule wa kwanza alisema, "Pokea uponyaji!" na mtu yule alipona mara ile ile. Kwa wa pili alisema, "Mtoke mtu huyu wewe pepo wa uziwi." Masikio ya mtu huyu pia yalifunguliwa mara. Baadaye alipoulizwa ni kwa nini alimhudumia kila mtu kwa namna tofauti alisema, "Huhitaji kuponya mapepo, ila kuyaamuru kutoka." Bwana Wigglesworth asingeweza kufahamu namna ya kumhudumia kila mtu vema pasipo utendaji wa karama ya kupambanua roho. Ni mara ngapi tumejaribu "kuponya pepo" na kukemea ugonjwa utoke, wakati tulistahili kufanya tofauti ya hivyo: Kuanza kutenda karama ya mafunuo huwezesha utendaji wa karama za nguvu kufuatia.

2. Karama za unabii na huduma yenye nguvu (Zimetolewa ili kuyanena maneno ya Mungu). Karama za unabii ni za muhimu katika uinjilisti wenye nguvu. Karama ya unabii mara nyingi itatangulia au kufuatia utendaji wa nguvu za Mungu. Ndivyo ilivyokuwa siku ya Pentekoste wakati Petro alipohubiri "mahubiri" madhubuti ya Pentekoste. Kwa kweli mahubiri hayo hayakuwa mahubiri ya kawaida, bali yalikuwa matamko ya unabii yakiwa yamezungumzwa chini ya upako wenye nguvu za Roho Mtakatifu[24] Matokeo ya kuona na kusikia miujiza ya Pentekoste (udhihirisho wa nguvu), na kusikia matamko ya unabii wa Petro (kweli ya neno), watu walichomwa dhamiri kwa ajili ya dhambi zao (Mdo 2:37) na 3,000 waliokolewa na kubatizwa siku ile ile (mstari 41).

Paulo anatufundisha katika (1Kor 14:22) ya kwamba ndimi ni ishara kwa wasioamini ya kwamba Mungu anafanya kazi katikati ya kusanyiko la wakristo. Pia anasema ya kwamba kwa njia ya unabii mwenye dhambi anapata kutambua kuhusu uwepo wa Mungu. Matokeo yake atajiona dhahiri ya kuwa "ni mwenye dhambi,… na siri za moyo wake huwa wazi; Na hivyo atamwabudu Mungu akianguka kifudifudi…" (mistari 24-25). Kutimilika kwa unabii kama ilivyotokea katika manabii wa Agano Jipya, Agabo, yaweza pia kuwa ni ushuhuda wenye nguvu ya uwepo wa Mungu katika kanisa (Mdo 11:27; 21:10).

3. Karama za nguvu na huduma yenye nguvu (Zimetolewa ili kutenda kazi za Mungu). Karama za nguvu kwa kawaida huwakilisha matumizi ya karama za Roho katika uinjilisti wenye nguvu. Kwa njia ya karama za uponyaji na imani watu huponywa, nguvu na uwepo wa Mungu hudhihirika, watenda dhambi

[24]Stanley Horton, *What the Bible says about the Holy Spirit* (Springfield, MO: Gospel Publishing House, 1976), uk. 144.

huletwa macho kwa macho na ukweli wa Mungu aliye hai, na mioyo yao huwa tayari imeandaliwa kusikiliza na kuipokea injili. Katika uponyaji wa Ainea tunaona kitu kama hicho kikitokea:

> Hata Petro alipokuwa akizunguka-zunguka pande zote akawatelemkia na watakatifu waliokaa Lida. Akamwona mtu mmoja huko, jina lake Ainea, mtu huyo amelala kitandani miaka minane; maana alikuwa amepooza. Petro akamwambia, Ainea, Yesu Kristo akuponya; ondoka, ujitandikie. Mara akaondoka. Na watu wote waliokaa Lida na Sharoni wakamwona wakamgeukia Bwana. (Mdo 9:32-35)

Kwa njia ya karama ya kuponya, uamsho mkubwa ulilipuka katika eneo lile lote.

Karama nyingine ambayo ni ya muhimu katika huduma ya nguvu ni karma ya matendo ya miujiza (yaani, "utendaji wa kazi za nguvu"). Utendaji wa karama hii unaonekana kufungulia nguvu za kimungu zinazoleta uponyaji na matokeo ya miujiza (Lk 5:17; 6:19; Mk 5:30). Kutokana na "Full Life Study Bible," (toleo la Biblia lenye mafunzo" "Hizi [karama za matendo ya nguvu za miujiza] ni matendo ya nguvu za miujiza yanayobadilisha kanuni za asili. Hujumuisha matendo makuu ambayo kufanya ufalme wa Mungu kushinda ufalme wa shetani na mapepo … hii hujumuisha kutoa mapepo" (angalia pia Lk 11:20).

MWISHO

Nguvu za Roho wa Mungu ni muhimu kwa ajili ya huduma yoyote ya nguvu. Nguvu hizi zinatolewa wakati mtu akibatizwa na Roho Mtakatifu. Zinaanza kufanya kazi kwa kupitia karama za Roho. Ni muhimu kwa hiyo, kwamba kila mkristo atakayetaka kutumika na Mungu katika eneo hili la uinjilisti wenye nguvu awe amebatizwa na Roho Mtakatifu. Pia, ni lazima, ajifunze kutembea katika Roho ili kusudi hitaji linapotokea na jinsi Roho apendavyo, karama ziweze kutenda kazi katika huduma yake. Kama hujabatizwa na Roho Mtakatifu ni vema uanze kutafuta kujazwa sasa hivi kwa kumuomba Mungu akujaze kwa Roho wake.

— Sura ya Saba —

Kuongozwa Na Roho Mtakatifu Na Huduma Yenye Nguvu

UMUHIMU WA UONGOZI WA ROHO MTAKATIFU
KATIKA HUDUMA YENYE NGUVU

Ilikuwa ni Muhimu Katika Huduma ya Yesu

Uchunguzi wa uangalifu wa vitabu vinne vya injili unaonyesha ya kwamba kila tendo la huduma ya Yesu lilifanyika chini ya uongozi na uangalizi wa Baba yake wa mbinguni. Yesu alikuwa na ushirika nyakati zote na Baba. Kama tulivyokwisha elekeza awali katika Sura ya 5, "Mambo muhimu na Matayarisho ya Huduma yenye Nguvu," wakati wote alitenda kama Baba alivyoelekeza. Soma kwa uangalifu na kwa kutafakari maneno yafuatayo ya Yesu kama yanavyopatikana katika Yohana 5:19, 20:

> Amin Amin nawaambia, *mwana hawezi kutenda neno mwenyewe, ila lile ambalo amwona Baba analitenda;* Kwa maana yote ayatendayo yeye, ndiyo ayatendayo mwana vile vile. Kwa kuwa Baba ampenda mwana, naye humwonyesha yote ayatendayo" (mkazo wa mwandishi, angalia pia Yn 8:28-29 na Yn 12:49).

Mistari ya juu inatuonyesha ya kwamba Yesu alihudumu na kutenda kazi za miujiza chini ya uongozi wa Baba yake wa mbingini. Alifanya yale tu "*aliyomwona Baba akifanya."* Hivyo kwa njia ya Roho aliyekaa ndani yake alikuwa nyakati zote na ushirika na Mungu. Kila muujiza alioufanya ulikuwa umeandaliwa kabla na Mungu. Nyakati zote alifanya yale ambayo Baba yake

alimwambia ayafanye.

Hapo awali kulikuwepo mtu ambaye Mungu mara nyingi alimtumia kuponya wagonjwa. Siku moja mtu mmoja alimpa changamoto, "Kama una karama ya kuponya, kwa nini usiende hospitali na kumponya kila mtu pale?" Mtu yule alimjibu, "Yesu alipokwenda hospitali hakumponya kila mtu pale." Ni lini kwani ambapo Yesu alikwenda hospitali?" Yule mtu wa kwanza alimwuliza. "Aliwahi kwenda "hospitali ya "Bethzatha,'" alimjibu. "Soma mwenyewe katika Yohana 5:1-15. Ingawaje palikuwa na 'namba kubwa ya watu wasiojiweza … vipofu, viwete na waliopooza" pale, Yesu alimponya mmoja tu kati yao.

Nyakati nyingine Yesu aliwaponya wote waliokuwa wagonjwa mahali fulani (angalia: Mt 4:23, 24; 8:16). Nyakati nyingine alimponya mmoja tu, kama kwenye birika la Bethzatha kama ilivyoelezwa juu. Kwa nini Yesu alimponya mmoja tu pale Bethzatha? Katika mistari ifuatayo (mistari 19-20), Yesu alijibu hili swali yeye mwenyewe: "Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda." Yesu alimponya mtu mmoja tu pale Bethzatha kwa sababu Baba yake wa mbinguni alimwelekeza amponye huyo mmoja tu. Kama nyakati zote, alifanya lile alilomwona Baba yake akilifanya.

Utendaji huu, ninafikiri, ni ufunguo muhimu katika huduma yoyote ya mafanikio, na hasa huduma yenye nguvu. Sisi tunaotamani kutumika katika huduma kama hiyo ni lazima tujifunze mfano kutoka kwa Yesu. Kama vile huduma ya Yesu katika neno na tendo ilivyokuwa chini ya uongozi wa Baba yake, sisi pia, kama tutatumika katika nguvu na mafanikio makubwa, lazima tuzitende huduma zetu chini ya uongozi wa Baba wa mbinguni. Njia pekee kwetu sisi ya kupata kuhudumu katika nguvu ni kuisikiliza na kuitii sauti ya Mungu. Kama ilivyokuwa kwa Yesu, sisi pia tunaweza tu kulitenda lile tumwonalo Baba akilitenda—siyo zaidi, wala siyo pungufu.

Kama hivi ni kweli, fikiria tu ilivyo muhimu kuweza kusikia na kutambua sauti ya Baba. Pasipo uwezo huo ni mambo madogo sana katika huduma yatafuatia.

Ilikuwa ni Muhimu Katika Huduma ya Kanisa la Kwanza

Mitume walijifunza jinsi ya kuhudumu hasa kwa kuangalia na kuiga huduma ya Yesu. Kama yeye. wakati wote walitafuta na kupokea maelekezo katika kutenda huduma zao.

Yesu na mitume mara nyingi walishuhudia, kwa kutumia maneno ya John Wimber, "kwa mpango kamili wa Mungu."[25] Kwa maneno mengine, Mungu alipanga tayari ule wakati wao wa kushuhudia, ndipo akawaongoza kupafikia mahali ambapo walijikuta wapo penye uwezekano wa kushuhudia. Tutataja mifano mitatu katika Agano Jipya wa kwanza unamhusu Yesu, wa pili unamhusu Filipo, na wa mwisho unamhusisha mtume Petro.

1. Yesu na mwanamke msamaria. Katika Yohana 4:1-42 soma kuhusu uamsho wa ajabu uliotokea mji wa Samaria uitwao Sikari. Uamsho huo ulianza kutokana na ushuhuda wa Yesu kwa mwanamke huyo wa Samaria. Alimshuhudia, na kumpata mwanamke aliyekutana naye katika kisima cha kijiji. Lakini ni kwa nini Yesu alikwenda Samaria? Alikwenda kwa sababu Baba yake wa mbinguni alimwelekeza aende pale. Katika mstari wa 4 Biblia inasema, "Naye alikuwa hana budi kupita Samaria." Kwa nini ilikuwa ni muhimu hivyo kwa Yesu kupita Samaria? Kwa sababu Baba alikuwa ameshaipanga safari hiyo. Kulikuwa na mwanamke aliyemhitaji Yesu, na pia mji ule ulikuwa tayari umewiva kwa ajili ya uamsho.

2. Filipo na towashi wa Kushi. Habari ya Filipo na towashi wa Kushi ni mfano mmojawapo wa kanisa la kwanza jinsi lilivyohudumu kwa kufuatilia "mpango halisi wa Mungu." (Angalia Mdo.8:26-40). Katika mstari wa 26 Biblia inasema, "Malaika wa Bwana akasema na Filipo, akamwambia, ondoka ukaende upande wa kusini hata njia ile - itelemkayo kutoka Yerusalem kwenda Gaza—nayo ni jangwa." Mungu alikuwa tayari amepanga makutano kati ya Filipo na mwafrika mmoja aliyekuwa ana njaa ya kumjua Mungu aishiye. Alipomwona mtu huyo amepanda gari lake la farasi akisoma kutoka Isaya 53:7-8, Roho wa Bwana akasema na Filipo, "Sogea karibu na gari, ukashikamane nalo" (mstari 30). Alipokaribia gari lile, Filipo alimsikia mtu yule akisoma kwa nguvu kutoka katika kitabu cha Isaya. Filipo akaanza mazungumzo na mtu yule yaliyomfanya hatimaye aokolewe. Hapa tena tunaona waziwazi umuhimu wa Filipo kuweza kuisikia sauti ya Roho. Kama tutahitaji kuwa na huduma yenye mafanikio, sisi pia ni lazima tuweze kuisikia na kuifahamu sauti ya Roho.

3. Petro na nyumba ya Kornelio. Mfano wa mwisho wa kuhudumu kwa "mpango halisi wa Mungu" unapatikana katika Matendo 10:1-48. Katika habari hii Mungu mwenyewe alipanga mkutano baina ya Kornelio, askari wa Kirumi na mtume Petro. Akiwa tayari amepanga mahali pa kukutania, ndipo Mungu

[25]John Wimber, Power Evangelism.

akaanza kuzungumza na wote Kornelio na Petro kwa njia ya maono (mistari 3-4; 10-11). Pia Alisema wazi kwa Petro kwa njia ya Roho wake (mstari 19). Soma habari hii ya ajabu wewe mwenyewe katika Biblia yako. Tena utauona umuhimu wa kuweza kusikiliza na kutii sauti ya Roho.

Kwa kuhitimisha, kama sisi, kama ilivyokuwa kwa Yesu na mitume, tutahudumu chini ya uongozi wa Roho, lazima tujifunze kuisikiliza na kuifahamu sauti ya Mungu. Hii inatuleta kwenye swali la muhimu, "Je! Mtu anawezaje kusikiliza sauti ya Mungu?" Tutajaribu kujibu swali hili katika sehemu ifuatayo ya sura hii.

JINSI YA KUISIKIA SAUTI YA MUNGU

Kama utahitaji kuisikia sauti ya Mungu, fahamu na kuitumia misingi sita ifuatayo:

Tambua ya Kwamba Mungu Anazungumza na Wewe

Kwanza, ni lazima utambue ya kuwa Mungu *huzungumza* na watoto wake leo. Kusema kweli, anazungumza na wewe leo! Mungu, kwa asili yake, ni Mungu asemaye, na kama Baba yeyote mwenye upendo, anazungumza na watoto wake nyakati zote. Endapo wewe huisikii sauti ya Mungu, si kwa sababu hazungumzi na wewe bali bila shaka ni kwa sababu wewe mwenyewe hujui jinsi ya kumsikiliza yeye.

Wakati fulani mtunza bustani alikuwa akitaka kumwagilia maji katika bustani yake. Alisumbuliwa kwa sababu maji yalikuwa hayatoki kwenye mpira wa kumwagilia. Kwa hasira alimpigia kelele mtunza bustani mwenzake, "Maji hayatoki katika mpira huu. Nilikuambia fungulia maji katika bomba ili yapate kutoka!" Alipewa jibu hili: "Rafiki, maji yamekwisha kufunguliwa, lakini kuna mkunjo katika mpira wako, kiasi kwamba maji hayawezi kutoka." Ndivyo mara nyingi ilivyo kwetu. Mungu anasema nasi, lakini sisi hatusikii. Tuna mkunjo katika mpira wetu.

Fahamu Jinsi Mungu Asemavyo

Kama tutahitaji kuisikia sauti ya Mungu ni lazima tufahamu jinsi Mungu anavyozungumza nasi. Yesu alisema, "Kondoo humsikia sauti yake [(mchungaji]… wanaijua sauti yake" (Yn.10:3-4). Zipo njia nne ambazo Mungu anazungumza nasi leo. Tunaweza kuziita (1) kwa njia ya msingi, (2) kwa njia ya

ana kwa ana, (3) kwa njia ya kawaida, na (4) kwa njia yakuthibitisha.

1. Njia ya msingi ambayo Mungu husema nasi. Njia ya msingi ya Mungu kusema na mwanadamu leo ni kwa njia ya Neno lake, Biblia Takatifu. Kama unataka kujua ni nini Mungu anasema kwako, unaweza kuona katika Biblia. Hii ni njia pekee ya msingi tuliyonayo katika kusikia sauti ya Mungu. Njia nyingine yoyote lazima ipimwe na kuhakikishwa na njia hii ya msingi.

2. Mungu pia husema kwa njia ya ana kwa ana. Zaidi ya Neno lake, Mungu pia huzungumza na watoto wake kwa njia ya ana kwa ana. Katika Biblia njia hizi ni pamoja na ndoto, maono, malaika pamoja na kunena kwa sauti ya kusikika. Ni kweli Mungu anaweza kufanya mambo hayo yote leo, ingawa onyo *la*zima litolewe hapa. Nyakati zingine watu kadhaa wasio wakiroho, wakitaka waonekane kuwa ni wa kiroho mbele za wengine, hujifanya eti Mungu amezungumza nao kwa njia kadha, matokeo yake watu wengi wa kiroho huamua kuachana na maswala ya jinsi hii,ya ndoto na maono. Je! Mwangalio wetu uweje katika maswala haya? Kwanza, lazima tufahamu ya kuwa hizo sio njia peke yake ambazo Mungu alitumia kusema na watu wake katika Biblia. Njia muhimu aliyotumia ilikuwa ni kwa njia ya Roho wake katika roho zao. (Tutajadili jambo hili baadaye). Hata kama njia hizo za ndoto na maono siyo njia peke yake ambazo Mungu alinena na watu wake, pia ni kati ya njia anazotumia. Njia pekee ya kufanya ni kule kutokukazania kuzitafuta njia hizo tu. Hata hivyo kama Mungu atachagua kusema nasi kwa njia hizo basi hapo tusiwe na shaka lolote.

3. Njia ya kawaida ambayo Mungu hutumia. Kama tulivyokwisha kuzungumza hapo juu, njia ya kawaida sana ambayo Mungu hutumia kusema na watoto wake ni kwa njia ya Roho wake katika roho zetu. Mistari miwili ya Agano la Kale inatusaidia kuelezea njia hii. Mmoja ni mfano wa nabii Eliya. Hakuisikia sauti ya Mungu katika hali ya ana kwa ana (k.m. kama upepo mkali, tetemeko, au moto), bali alisikia sauti yake kama "sauti ndogo ya utulivu" (1Fal 19:12-13). Mfano mwingine ni ushuhuda wa nabii Isaya. Aliielezea sauti ya Mungu kwa namna hii: "… na masikio yako yatasikia neno nyuma yako likisema, 'Njia ni hii ifuateni'" (Isa 30:20).

Swala hili ya kwamba Mungu hunena na watumishi wake Roho kwa roho limewekwa wazi katika Agano Jipya. Katika Rumi 8:14 mtume anasema, "Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu." Halafu katika mstari wa 16 anaendelea, "Roho mwenyewe hushuhudia pamoja a roho zetu, ya kuwa sisi tu wana wa Mungu." Angalia hapa Paulo anasema ya kuwa Roho wa Mungu husema moja kwa moja na roho za watu waliookoka. Hii ndiyo njia ya kawaida sana ambayo yatupasa kutegemea Mungu kusema nasi leo.

Mtume Paulo anaendeleza jambo hili katika 1Wakorintho 2:9-13. Hebu chukua muda kidogo usome kwa uangalifu na kuyafikiria maneno haya. Hapa Paulo anaweka njia tatu ambazo Mungu hutumia kusema na roho zetu. Kabla ya yote anaeleza ya kwamba Mungu hutufunulia kweli yake kwetu kwa Roho wake:

> Lakini kama ilivyoandikwa, mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu, mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao - *lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho.* Maana Roho huchunguza yote hata mafumbo ya Mungu. (mistari 9-10, mkazo wa mwandishi)

Halafu, Paulo analinganisha kati ya roho ya mtu na Roho wa Mungu. Anasema kwamba roho ya mtu ndani yake inayatambua mawazo yake. Katika hali hiyo hiyo Roho wa Mungu huyatambua mawazo ya Mungu:

> Maana ni nani katika binadamu ayajuaye mambo ya binadamu ila roho ya binadamu iliyo ndani yake? Vivyo hivyo mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye ila Roho wa Mungu. (mstari 11)

Hatimaye, Paulo anaelekeza matumizi ya ukweli huu. Anasema ya kuwa kwa kuwa Roho wa Mungu anayajua mawazo ya Mungu, nasi tumempokea Roho wa Mungu, tunaweza kwa namna hiyo tukayajua mawazo ya Mungu. Roho wake atayatambua na kuziambia roho zetu:

> Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu. Nayo twayanena si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu bali yanayofundishwa na Roho.… (Mistari 12-13a pia angalia mstari 16)

Njia ya kawaida ya Mungu katika kuzungumza na watoto wake ni kwa Roho wake na roho zetu. Kama mwana wa Mungu unaweza kutegemea mara nyingi kuisikia sauti ya Mungu ikisema nawe kwa njia hii.

4. Mungu husema kwa njia ya kuthibitisha. Njia ya mwisho ambayo tunaweza "kuisikia" sauti ya Mungu ni kwa njia ya kile kinachoitwa "njia ya kuthibitisha." Tofauti na zile njia tatu tulizozungumzia hapo juu, njia za kuthibitisha si njia za moja kwa moja za kumsikia Mungu kama zile za ana kwa

ana. Katika njia hii Mungu hutumia matukio au watu wengine kusema nasi. Njia mojawapo katika hizo ni matukio ambayo *hutumwa na Mungu mwenyewe.* Hii ina maana ya kuwa ni yale matukio ya maisha ambayo Mungu huyapanga moja kwa moja kwetu ili kutuonyesha mapenzi yake.

Njia nyingine ya kuthibitisha ambayo Mungu hutumia kusema nasi ni kupitia *wakristo wengine waliojazwa Roho Mtakatifu.* Kwa maneno mengine, Mungu atasema mapenzi yake kwetu kupitia wakristo mwingine. Mara nyingine mtu huyu atajua kuwa ule ujumbe ambao mwenzake anazungumza unatoka kwa Mungu, nyakati nyingine atasema maneno ambayo hayaelewi vizuri, lakini Mungu atayafanya yaeleweke mioyoni mwetu.

Wakati mwingine Mungu atasema nasi kupitia matamko ya unabii ambayo huzungumzwa katika hali ya upendo katika kusanyiko la wakristo. Matamko haya ya unabii huwa ni pamoja na jumbe za lugha na tafsiri pamoja na unabii wa upako. Tena, lazima tutoe onyo kali hapa. Wengi wetu tumekwisha kuona njia hii ikitumika vibaya na wakristo wachanga ambao wana mori wa kupita kiasi. Wengine wamepotolewa na kukwazwa na "manabii wa uongo" wa jinsi hii. Kumbuka mambo haya mawili unapojisikia ya kwamba Mungu anaweza kuwa anasema kwako kupitia wengine: 1) Linalozungumzwa ni lazima likubaliane kabisa na Neno la Mungu. Kama sivyo, ulikatae mara moja kama vile halitoki kwa Mungu. 2) Linalozungumzwa ni vema lihakikishe na jambo ambalo tayari Mungu amekwisha kusema, au atasema, moja kwa moja kwenye roho yako. Kamwe, narudia *kamwe* usimruhusu mtu akuambie Mungu amesema hivi pasipo kupima na kuhakikisha kwa uhakika yake yaliyosemwa. Mara zote mtafute Mungu wewe mwenyewe hadi amezungumza nawe moja kwa moja, kwa Roho wake ndani ya roho yako.

Tayarisha Moyo Wako Kuisikia Sauti ya Mungu

Sababu mojawapo ambayo inatufanya tushindwe kuisikia sauti ya Mungu anaposema ni kwa sababu mioyo yetu haijatayarishwa vema kumsikiliza. Ni sasasawa na redio ambavyo inatakiwa ichomekwe kwenye nguvu ya umeme na pia iyapate masafa ya stesheni inayorusha matangazo kabla haijaweza kupokea taarifa kutoka kwenye stesheni ya redio ya matangazo, sisi pia ni lazima tuyapate masafa ya Roho Mtakatifu kabla hatujaweza kuisikia sauti ya Mungu. Ninaposema ni lazima tuchomekwe kwenye nguvu ya umeme ninamaanisha ya kwamba ni lazima tuzaliwe mara ya pili. Ni kwa njia ya kuzaliwa mara ya pili ndipo roho zetu zinapokuwa zimeunganishwa na nguvu za mitambo ya mbinguni, yaani Roho wa Mungu. Paulo anasema katika 1Wakorintho 6:17, "Lakini yeye

aliyeungwa na Bwana ni Roho moja naye." Roho zetu "zimeungana" na Roho wa Mungu. Ni pale "tukizaliwa katika Roho" (Yn.3:5) ambapo Roho Mtakatifu anaingia ndani yetu, ndipo tunapofanyika kuwa "viumbe vipya" katika Kristo (2Kor.5:17). Ndiyo maana Yesu alisema ya kwamba mara mtu akizaliwa mara ya pili ndipo anapoweza "kuuona ufalme wa Mungu" (Yn.3:3). Paulo alisema "Mwanadamu wa tabia ya asili… hayapokei [mambo ya Roho wa Mungu], maana kwake hayo ni upuuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya Rohoni" (1Kor.2:14).

Zaidi ya kule kuzaliwa mara ya pili, "kuchomekwa" katika nguvu ya mitambo ya mbinguni kunahusu pia kubatizwa na Roho Mtakatifu. Kama tutahitaji wakati wote kusikia sauti ya Roho, ni lazima tujazwe na Roho Mtakatifu.[26] Kujazwa na Roho kutatuongezea uwezo wa kusikia sauti ya Roho. Inaweza kulinganishwa na kuongezea nguvu zaidi katika redio au kuinua waya mrefu zaidi wa mapokezi ya mawimbi ya hewa katika redio. Kwa kujazwa na Roho utapokea nguvu zaidi na pia unakuwa na hisia zaidi katika Roho.

Sio tu lazima tuunganishwe na Roho wa Mungu, lazima pia tuunganishe mitambo yetu na sauti yake. Haitoshi tu redio iungane na chanzo cha mitambo ya nguvu. Kabla ya kupokea ujumbe kutoka kwenye kituo cha kurushia matangazo, ni lazima pia iunganike na kupata masafa yanayohusika. Tunaunganisha masafa yetu na Mungu kwa njia ya kujitoa kwa Mungu na kwa mapenzi yake timilifu kwa maisha yetu. Biblia inatuonya, "Kwa hiyo kama anenavyo Roho Mtakatifu: Leo kama mtaisikia sauti yake, *msifanye migumu mioyo. . ..***"** (Ebr 3:7-8). Tunahitaji kuiweka mioyo yetu wazi na laini mbele zake. Wepesi wa hisia wa namna hiyo kwa Roho wa Mungu waweza kupatikana tu kutoka mioyo yenye unyenyekevu na utii. Hii yaweza kuja kwa njia ile tu ya maisha ya kumtumaini, pamoja na muda mwingi unaotumika katika maombi ya kulitafakari neno.

Jifunze Jinsi ya Kuitambua Sauti ya Mungu

Kama tutahitaji nyakati zote na kwa uwazo kuisikia sauti ya Mungu ni lazima tujifunze kuisikia wakati anaposema. Yesu alisema, "Kondoo kumsikia [mchungaji] sauti yake… na … huijua sauti yake" (Yn 10:3-4). Uwezo wa namna hiyo wa kuijua sauti ya mchungaji, unakuja tu kwa njia ya mazoezi

[26]Kwa majadiliano ni vipi unaweza kujazwa na Roho Mtakatifu, angalia sura ya 6, "Roho Mtakatifu na Huduma yenye nguvu."

(angalia Ebr 5:14). Jinsi tunavyofanya mazoezi ya kuisikia na kutii sauti ya Roho, tunajifunza vema zaidi kuitambua sauti yake asemapo.

Ijaribu Sauti ili Kuhakikisha Kama Kweli ni ya Mungu

Neno la maonyo ni muhimu hapa. Ni muhimu kwamba tunajifunza kuzijaribu sauti "tunazozisikia" ili tuweze kuzitambua kama kweli ni sauti za Mungu. Biblia inatuambia ya kwamba kuna "sauti za namna nyingi duniani (1Kor 14:10). Sauti hizi ni pamoja na sauti za binadamu, vyote sauti yetu ya ndani (mawazo yetu), na sauti zanje (watu wengine). Sauti hizi pia ni pamoja na sauti za kiroho pamoja na mawazo ambayo yanaweza kupandikizwa katika mawazo na Mungu au na Roho wachafu. Ni muhimu kujua jinsi ya kupima sauti hizi, ili kujua kama zinatoka kwa Mungu au hapana. Kama hazikubaliani na neno la Mungu lazima zikataliwe.

Kwa Imani Fanya Mazoezi ya Kuitii Sauti ya Mungu

Msingi wa mwisho ambao lazima tuufahamu ni huu: Kama tutahitaji kujifunza namna ya kuipambanua sauti ya Mungu, lazima kwa imani tuanze kutii sauti yake tunapoisikia. Tunayo sababu moja nzuri ya kusikia sauti ya Mungu: Tunaisikiliza sauti ya Mungu ili tupate kuitii. Je! Tufanye nini basi? Ni lazima tutegemee kuwa Mungu atasema, na atakaposema, sisi lazima tumtii. Jinsi tunavyomtii na kumfuata, tunajifunza kuipambanua sauti ya Mungu vema.

MWISHO

Uwezo wa kujua na imani ya kutii sauti ya Mungu ni mahitaji muhimu kwa huduma yenye nguvu. Tunahitaji tufanye kuwa ndiyo shabaha yetu kujifunza jinsi ya kuyafanya yote.

— Sura Ya Nane —

Silaha Za Vita Vyetu

UTANGULIZI

Katika sura ya 3, "Huduma yenye nguvu na ufalme wa Mungu." tulijifunza ya kwamba Kristo alikuja kuanzisha ufalme wa Mungu duniani. Anaendelea kufananisha malengo yake kwa njia ya kanisa, na upako wa Roho Mtakatifu. Kwa sababu shetani anapinga maendeleo ya ufalme wa Mungu, vita kuu ya kiroho imeanza. Sasa, ikiwa tunapenda au la—ikiwa tunafahamu au hatufahamu—kanisa limo katika vita kubwa dhidi ya ufalme wa shetani (angalia Efe 6:12). Katika vita hii Kristo ametupatia nguvu na mamlaka dhidi ya adui, shetani. Sikiliza yale aliyosema Yesu katika Luka 10:19-20:

> Nilimwona shetani akianguka kutoka mbinguni kama umeme. Tazama nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru.

Ili vita yoyote ipate kupigwa vema, inahitaji silaha. Ni hivyo hivyo, vita vya kiroho vita tunavyopigana vinahitaji silaha za kiroho. Sisi kama jeshi la kiroho la Kristo tumepewa zana zote za kiroho tunazohitaji kumshinda shetani. Katika 2Wakorintho 10:3-5, mtume Paulo anazungumzia kuhusu silaha hizo za kiroho: "Maana silaha za vita vyetu si za mwili bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngume."

Katika sura hii tutazitambua silaha hizi za kiroho na kujadili jinsi ya kuzitumia ili kushinda vita dhidi ya shetani na majeshi yake ya mapepo.

SILAHA ZOTE ZA MUNGU

Katika Waefeso 6:10-18 tunaambiwa tuvae silaha zote za Mungu, au kama Ronald Knox alivyotafsiri sehemu hii, "Unahitaji uvae silaha zote zilizomo katika bohari ya Mungu ya silaha"[27] Tumeambiwa ya kwamba tuzichukue silaha za Mungu ili tukabiliane na shetani. Je! Ni nini basi maana ya *"silaha zote za Mungu"* kama ilivyoandikwa katika Waefeso sura ya 6, na tunaweza kuzitumia vipi ili kumshinda shetani? Hili ndilo tutakalojadili katika sehemu ya kwanza ya sura hii.

Chanzo cha Nguvu ya Vita

Lazima tukumbuke ya kwamba chanzo cha nguvu zetu za vita si za kimwili, bali za kimungu. Hapa katika maandiko haya Paulo anatuambia tuwe "hodari katika Bwana na "katika uwezo wa nguvu zake" (mstari 10). Tunatakiwa tusiangalie katika nguvu zetu, au silaha zetu ili kupigana vita hii ya kiroho. Tunatakiwa kumwangalia Mungu na nguvu zake na silaha zake. Ingawa hatuangalii katika nguvu zetu, kuna jambo, hata hivyo, ambalo lazima tulifanye: Lazima sisi wenyewe "tuvae silaha zote za Mungu [tupate] kuweza kuzipinga hila za shetani."

Makusudi ya Silaha Zote za Mungu

Paulo anatueleza makusudi ya silaha za kiroho. Zipo mbili:
Kwanza, kwamba tunaweza kusimama kinyume cha mashambulizi ya adui (mstari 13), na pili, kwamba tusiangukie katika mtego wa "hila" za shetani (mstari 11). Neno lililotafsiriwa "Hila" katika mstari wa 11 lina asili ya neno la kiyunani, "methodeia." ambalo limetafsiriwa kwa kiingereza katika namna nyingi, pamoja na "njia," "mbinu," "ujanja," "hila," *na* "mitego." Hivyo, tunahitaji kuwa tumejiandaa kwa vyote mashambulizi ya adui na mbinu zake mbalimbali.

Sehemu Mbalimbali za Silaha Zote za Mungu

Paulo sasa anatumia mavazi ya silaha za askari wa Kirumi kama njia ya

[27]The *New Testament in the Translation of Ronald Knox*

kuelekeza sehemu mbalimbali za silaha za mkristo za kiroho. Sikiliza maneno yake:

> Basi simameni, hali mmejifunga *kweli* viunoni, na kuvaa dirii ya *haki* kifuani, sehemu za kufungiwa miguu *utayari* tupatao kwa injili ya amani; zaidi ya yote mkitwaa ngao ya *imani***,** ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Tena ipokeeni chepeo ya *wokovu,* na upanga wa Roho ambao ni *neno la Mungu*; kwa sala zote na maombi *mkisali kila wakati katika Roho*, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote (Efe 6:14-18, mkazo wa mwandishi).

Utatambua ya kwamba tulitilia mkazo maneno saba ya muhimu na sehemu za sentensi katika kifungu cha maneno yaliyopo juu. Kila neno au sehemu ya sentensi inazungumzia silaha yenye nguvu ya mkristo. Tutaangalia kwa kifupi kila silaha:

1. Kujivika silaha ya kweli. Sisi, kama askari wa kikristo, tunahitaji kujivika silaha ya kweli. Kujivika kweli viunoni maana yake ni kwamba tujivike silaha ya Neno la Mungu, ambalo ni kweli (Yn 17:17). Tuijaze mioyo yetu na mawazo yetu na Neno la Mungu. Pia inaweza kumaanisha tujivike na kusema ukweli ambao ni uaminifu wote na tabia njema.

Kutokana na mstari wetu, tunatakiwa tujivike silaha hizi zote ile tuweze kukabiliana na mashambulizi na hila za shetani. Hebu fikiri pamoja nami kwa kitambo. Je! Ni dhidi ya hila zipi za shetani silaha hii ya kweli inaweza kutumika? Inaweza *kutumika dhidi ya uongo wa shetani!* Kumbuka ya kuwa yeye ni mwongo na baba wa huo (Yn 8:44). Moja ya silaha zenye nguvu za shetani ni uongo. Tunaweza kukabiliana na uongo wake kwa kuihubiri kweli ya Neno la Mungu na kwa kuishi maisha ya ukweli na heshima mbele za Mungu na wanadamu.

2. Kuvikwa silaha ya haki. Katika vita vyetu na shetani, tunatakiwa tusijivike silaha ya kweli tu, bali pia lazima tujivike silaha ya haki. Haki inaweza kufafanuliwa kama uhusiano mzuri na pia maisha mema. Tunaweza tukawa kweli watu wa haki kama tuna uhusiano mzuri na Mungu kwa njia ya Yesu Kristo. Kutokana na matokeo yauhusiano huu tunatakiwa sasa kufanya mazoea ya kuishi maisha mema; hii inamaanisha kuishi maisha masafi na matakatifu. Ni lazima tujue namna ya "kusema 'hapana' kwa ubaya na tamaa za kidunia, na tuishi maisha kwa kiasi na haki na utauwa katika ulimwengu huu wa sasa" (Tit 2:12). Hivyo kwa kuvaa dirii ya haki, tutaweza kuizima mishale yote ya shetani

na hila zake ambazo zimewashinda wengi.

3. Kujivika utayari. Tena Paulo anatuambia ya kwamba tujivike na utayari. Kwa maneno mengine, tunahitaji tubakie katika hali ya kuwa tayari na wakati wote tuwe macho kwa mashambulizi ya adui. Petro anatuonya, "Muwe na kiasi na kukesha, kwa kuwa mshitaki wenu ibilisi, kama simba aungurumaye, huzunguka-zunguka, akimtafuta mtu ammeze" (1Pet 5:8). Lazima tujiweke tayari dhidi ya ujanja na mashambulizi ya adui.

Tambua ya kuwa Paulo anasema ya kwamba utayari huu unaletwa na injili. Ni kuhubiriwa kwa injili kunakoleta utayari, maandalizi na kuwavika silaha watu dhidi ya mbinu za maadui.[28]

4. Kujivika silaha ya imani. Silaha nyingine ambayo tunahitaji "tuichukue" katika vita vyetu na shetani ni silaha ya imani. Imani ambayo tunahitaji tuichukue ni lazima kwa hakika ichangamane na imani iokoayo, hii inamaanisha ule msingi wa kumwamini Mungu na wokovu wake kupitia kifo cha Yesu msalabani. Hata hivyo, silaha hii ya imani lazima iende zaidi ya imani ile iokoayo. Ni lazima pia ichangamane na imani yenye nguvu zaidi ijinyoshayo na kuyafikia yale ambayo Mungu ameyaahidi. Imani ya jinsi hiyo inaweza kutumika kama ngao ya "kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu" (Efe 6:16). Kwa silaha hii tunaweza kushinda kila shambulizi la adui. Mashambulizi haya yanaweza kuchanganya mawazo machafu, tamaa na ukaidi, maamuzi ya ukaidi, tamaa na woga.

Sio tu kwamba imani ni silaha madhubuti ya kujikinga, kama ilivyotajwa hapo juu, pia ni silaha yenye nguvu katika mashambulizi. Yaweza kutumika kumshinda adui. Tumia muda kusoma Waebrania, sura ya 11. Katika "sura hii mashuhuri ya imani" utaona jinsi wanaume na wanawake wa zamani walivyoitumia imani kama silaha yenye nguvu ya mashambulizi. Kwa imani "walishinda milki za wafalme, walitenda haki, walipata ahadi" (mstari 33). Kwa imani "walikuwa hodari katika vita, walikimbiza majeshi ya wageni" (mstari 34). Kwa kweli Biblia nzima imejaa watu kama hao ambao walitumia imani kama silaha yenye nguvu ya kuusukuma mbele ufalme wa Mungu duniani. Nasi pia, lazima tutumie silaha za kiroho zenye nguvu.

---

[28]Kwa majadiliano zaidi kuhusu nguvu ya injili angalia Sura ya 4, "Huduma yenye nguvu na kuihubiri injili."

5. Kujivika wokovu/ukombozi. Silaha ya tano katika silaha za mkristo dhidi ya shetani ni silaha ya wokovu. Hapa tunahitaji kutafsiri wokovu katika mapana. Hapa tunazungumzia sio tu wokovu kutoka dhambini na jehanamu, bali pia wokovu wowote, au ukombozi, utokao kwa Mungu. Hii yaweza kuchanganya wokovu, au ukombozi, kutokana na mapepo, hatari, ugonjwa na kifo. Pia hujumlisha ukombozi kutoka kwa shetani na mitego yake iliyofichika.

Wokovu huu unaweza tu kuja kutoka kwa Mungu. Tunalohitaji kulitenda ili kuupokea ni kuliitia jina la Bwana (Rum 10:13). Tunapokuwa tumedanganywa na adui na " kuchukuliwa mateka wa vita," ni lazima tukumbuke ya kwamba hatujapoteza mambo yote. Tunaweza kumwita Mkombozi wetu mwenye nguvu za ajabu, atatuokoa!

6. Kujivika Neno la Mungu. Moja ya silaha za kiroho zenye nguvu ni Neno la Mungu, katika maandiko limeelezwa kwamba ni "upanga wa Roho." Ninaona uwezekano wa aina mbili wa matumizi ya neno hili kwa mtumishi mkristo *"kuchukua . . .neno la Mungu."* Kwanza, ina maana kujivika silaha ya Biblia. Kujivika Biblia lazima tusome, tukariri, tuchambue, tutumie, na tuhubiri Neno la Mungu.

"Neno la Mungu" katika mstari huu pia linaweza kumaansha "neno" la binafsi ambalo tunaweza kulipokea kutoka kwa Mungu. Watafsiri wengine wa Biblia hulieleza neno hili kutoka kwa Mungu kama "neno la *rhema*" wakielezea neno ambalo limetokana na lugha ya Kiebrania. Hili "neno la *rhema*" laweza kuwa sehemu fulani ya maandiko ambalo Mungu husema na moyo wako ili kukutana na hitaji fulani binafsi. Pia inaweza kuwa ufunuo fulani wa binafsi utokao kwa Mungu ambao una nia ya kukutana na hitaji fulani hii inaweza kujumuisha maneno ya maarifa na hekima.

Kwamba ni ushauri mzima wa Mungu (Biblia nzima), au ni mstari fulani wa maandiko, silaha hii inaweza kutumika kwa njia zote mbili, kushambulia na kujikinga katika mapambano. Inaweza kutumika kama silaha ya mashambulizi wakati neno linahubiriwa na kufundishwa chini ya upako wa Roho Mtakatifu. Inaweza pia kutumika kama silaha ya kinga ili kujikinga na mashambulizi ya shetani. Shetani anapotujia na uongo wake tunaweza kumrushia ahadi za Mungu usoni kwake. Atarudi nyuma tu dhidi ya mapambano kama haya.

7. Kujivika maombi katika Roho. Silaha ya mwisho iliyotajwa katika Waefeso 6:18 ni *"maombi katika Roho."* Je! Inamaanisha nini maombi katika Roho? Ina maana ya aina yoyote ya maombi yenye upako wa Roho au yanayoongozwa na Roho. Pia ninaamini, ni kunena hasa katika lugha. (Angalia 1Kor 14:14 na Rum 6:26). Kuomba katika Roho ni silaha ya kiroho yenye nguvu

sana mikononi mwa wakristo waliojazwa na Roho Mtakatifu. Paulo anatuambia kwamba kamwe tusije tukaiweka silaha hii chini; ila "tuombe kila wakati katika Roho" (mstari 18). Askari wa kiroho anapoomba katika Roho baraka nyingi hufuata: akili yake inafanyika upya, maisha yake ya kiroho yanatiwa nguvu (1Kor 14:4), imani yake hujengwa (Yuda 20), na maombi yake yanakuwa ni sawasawa na mapenzi ya Mungu (Rum 8:27).

SILAHA ZA KIROHO NANE ZENYE NGUVU ZAIDI

Jinsi tunavyoendelea na sura hii ya silaha za vita vyetu, sasa tutaeleza kwa kifupi silaha nane za kiroho na zenye nguvu ambazo amepewa muumini. Nyingine kwa sababu zimejadiliwa kwa marefu mahali pengine katika kitabu hiki, tutazielezea kwa kifupi tu. Hata hivyo tunaona ni vema kuziweka zote mahali pamoja katika sura hii. Hii ni kumsaidia msomaji ili apate kuona ni silaha ngapi ambazo tayari anazo katika vita vyake dhidi ya shetani.

Silaha ya Maombi

Tumetaja sasa hivi maombi katika Roho kama silaha ya kiroho, lakini tazama tena Paulo anavyosema katika Waefeso 6:18: "*Kwa sala zote* na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na *kudumu katika kuwaombea* watakatifu wote" (mstari 18, mkazo wangu). Tazama hapa Paulo anasema *"Mkisali kila wakati,"* na tunatakiwa tufanye hivyo *"kwa sala zote na maombi."* Maombi ya namna nyingi ni silaha lubwa lakini isiyotumika mara nyingi katika mikono ya askari wa kiroho. Hivyo tusishindwe kutumia silaha hii yenye nguvu.

Silaya ya Kufunga

Silaha nyingine yenye nguvu ambayo tunayo ni silaha ya kufunga. Kufunga kunatakiwa kutumika pamoja na silaha ya maombi. Katika Marko Sura ya 9 ni habari ya kijana aliyepagawa. Katika habari hii wanafunzi wa Yesu wanajaribu kumtoa pepo kwa kijana; hata hivyo bidii yao haina mafanikio. Baba wa kijana huyo anamwona Yesu akija, anamkimbilia, anamuomba aje amtoe pepo. Yesu anakubali na kumtoa yule pepo na kijana anakuwa huru. Baadaye wanafunzi wa Yesu walimuuliza, "Mbona sisi hatukuweza kumtoa?" Yesu aliwajibu, *"Namna hii* haiwezi kutoka kwa neno lolote isipokuwa kwa kuomba na kufunga" (Mk

9:29, NKJV).[29] Ninaamini ya kwamba "Pepo wa namna hii" bado angalipo na maombi na kufunga ndiyo njia pekee ya ushindi dhidi yapepo wa namna hii.

Maandiko yanataja njia nne ambazo tunaweza kutumia silaha ya kiroho ya kufunga:

1. Kusaidia kuingia katika uwepo wa Mungu (Ezra 8:23).
2. Kuwafungulia wafungwa huru (Isa 58:6).
3. Kupata hekima na ufahamu (Dan 9:2-3, 21-22).
4. Kupata mapenzi ya Mungu katika jambo fulani (Mdo 13:2).

Tumia muda wa kutosha kuangalia mistari hiyo na kutafakari katika kila mstari. Itakusaidia kuelewa nguvu ya ajabu ya silaha ya kufunga.

Silaha ya Sifa

Silaha nyingine ambayo hatujaitaja ni silaha ya sifa. Hata kama sifa huwa haifikiriwi kuwa ni silaha ya kiroho, hata hivyo iko nguvu kubwa ya kiroho inayotokea katika sifa iliyo na upako wa Roho. Wana wa Israeli walipopiga kelele ukuta wa mji ulianguka (Yos 6:16-20). Wakati waimbaji wa Yehoshafati walipoanza kuimba na kusifu uzuri wa utakatifu wa Mungu, Mungu alishuka na akaweka waviziao dhidi ya majeshi ya wana wa Amoni, na wana wa Moabu, na hao wakaao Mlima Seiri na waliangamizwa (2Nyak 20:1-26). Kama Paulo na Sila walivyoomba na kuimba nyimbo za kumsifu Mungu usiku wa manane katika jela ya Kirumi, nguvu ya Mungu ilidhihirika: "Ghafla pakawa tetemeko kuu la nchi hata misingi ya gereza ikatikisika, na mara hiyo milango ikafunguka, vifungo vya wote vikafunguka" (Mdo 16:26).

Tunapomsifu Mungu, uwepo na nguvu zake huja na kutawala mahali iliyopo sifa (Zab 22:3), ndipo adui yetu huchanganyikiwa na kushindwa. Sifa ni silaha nyingine yenye nguvu mikononi mwa muumini.

Silaha ya Upendo

Upendo ni moja ya silaha zetu za kiroho na yenye nguvu. Upendo wa kweli una nguvu za ajabu katika kuwaongoza watu kwa Kristo. Wengine ambao hawawezi kumwamini Yesu kwa njia ya majadiliano yetu, au kwa njia ya utendaji wa nguvu wa matendo makuu ya Mungu, wanaweza kuja kwa Kristo

[29]NKJV - Tafsiri mojawapo ya Biblia katika Kiingereza.

kwa njia nyepesi ya udhihirisho wa upendo wa kweli. Sauli wa Tarso alimgeukia Kristo kwa sababu ya udhihirisho wa upendo aliouona katika ushuhuda wa Stefano. Kwa jinsi mawe yalivyompiga Stefano na kuuondoa uhai wake, aliomba, "Bwana usiwahesabie dhambi yoyote" (Mdo 7:60). Udhihirisho huo wa upendo ulikuwa na nguvu sana kwenye ufahamu wa Sauli, na ukamtayarisha kukutana kwake na Kristo aliyefufuka katika njia ya Dameski. Baadaye, katika Warumi 12:17, 20-21, Paulo anatuambia jinsi ambavyo sisi pia tunaweza kutumia silaha hiyo ya upendo:

> Msimlipe mtu ovu kwa ovu, angalieni yaliyo mema machoni pa watu wote… 'lakini adui yako akiwa na njaa mlishe; akiwa na kiu, mnyweshe, maana ufanyapo hayo, utampalia makaa ya moto kichwani pake.' Usishindwe na ubaya bali uushinde ubaya kwa wema.

Hivyo, uovu unaweza kushindwa na wema, na wanaume na wanawake wanaweza kumjia Kristo kwa silaha ya upendo.

Ubatizo wa Roho Mtakatifu

Katika Matendo 1:8 Yesu alisema ya kuwa wafuasi wake watapokea nguvu baada ya kuwajilia Roho Mtakatifu. Alikuwa akizungumza habari ya kubatizwa na Roho Mtakatifu (Mdo 1:4). Jambo hili ni silaha muhimu sana ya vita vya kiroho.[30]

Karama za Roho Mtakatifu

Sababu mojawapo kwa nini karama za Roho zilitolewa kwa kanisa (hasa zile karama tisa za Roho zilizoandikwa katika 1Kor 12:8-10) ni kwa ajili ya vita za kiroho. Kwa kupitia karama hizi jeshi la Mungu, kanisa, linaweza kupokea amri na maelekezo kutoka kwa Kamanda wake mkuu (karama za ufunuo); silaha hiyo inaweza kunena maneno yenye nguvu kutoka mbinguni (karama za unabii); na kuweza kudhihirisha nguvu za Mungu dhidi ya adui (karama za nguvu).[31]

---

[30]Kwa maelezo ya kina kuhusa karama hii angalia sura ya 6, "Roho Mtakatifu na Huduma Yenye Nguvu"

[31]Kwa maelezo kamili ya asili na matumizi ya karama za Roho katika huduma ya nguvu angalia Sura ya 6, "Roho Mtakatifu na Huduma yenye nguvu."

Silaha ya Jina la Yesu

Yesu ametupatia Jina lake kama silaya ya kiroho ya kutumika dhidi ya majeshi ya uovu. Mamlaka yote ya mbinguni inasimama nyuma ya Jina la Yesu. Na, tutumiapo Jina lake kama alivyoelekeza, sisi pia tunakuwa tunazungumza na mamlaka ya mbinguni. Nguvu zote za kuzimu lazima zitii Jina ambalo ni juu ya kila jina (Fil 2:9-11). Sikiliza maneno ya Yesu kuhusu matumizi ya Jina lake:

> Amin Amin nawaambieni, yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam na kubwa kuliko hizi atazifanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba. Mkiniomba neno lolote *kwa jina langu,* nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya mwana. Mkiniomba neno lolote kwa jina langu nitalifanya (Yn 14:12-14).

> Tena siku ile hamtaniuliza neno lolote, Amin Amin nawaambia, mkimwomba Baba neno lolote atawapa *kwa jina langu,* hata sasa hamkumwomba neno *kwa jina langu;* ombeni nanyi mtapata furaha yenu iwe timilifu (Yn 16:23-24).

Mitume mara nyingi walitumia jina la Yesu kuponya wagonjwa, kutoa pepo, na kuzitenda kazi za Yesu (Mdo 3:6). Sisi pia tunaweza kutumia silaha hii ya kiroho na yenye nguvu ili kutimiza mambo yale yale.

Silaha ya Injili. Injili, ambayo ni ujumbe wa Kristo, ni silaha kubwa na yenye nguvu. Katika Warumi 1:16 Paulo anaiita "nguvu ya Mungu iletayo wokovu kwa kila mtu aaminiye." Katika mioyo ya wale waisikiao ikihubiriwa. Injili inapohubiriwa nguvu ya Mungu huachiliwa. Jinsi ilivyo silaya ya ajabu, kuhubiriwa kwa Kristo![32]

MWISHO

Mungu ametupa silaha za kiroho nyingi zenye nguvu ili tuzitumie katika kupambana na kuzishinda nguvu za shetani. Sisi kama mashujaa wake wa kiroho, tunahitaji kujifunza jinsi ya kuitumia vema kila silaha.

---

[32]Kwa maelezo kamili ya asili na matumizi ya karama za Roho katika huduma yenye nguvu angalia Sura ya 6, "Roho Mtakatifu na Huduma yenye Nguvu."

Kifungu Cha III

Utendaji Wa Huduma Yenye Nguvu

— Sura Ya Tisa —

Jinsi Ya Kuponya Wagonjwa

UTANGULIZI

Sasa tunaanza kifungu cha tatu na cha mwisho cha mafunzo haya, kinachoitwa "Namna ya" kuifanya huduma yenye nguvu. Makusudi ya kifungu hiki ni kukusaidia wewe ujue namna ya kutumia misingi uliyokwisha jifunza katika vifungu viwili vilivyotangulia. Katika somo la kwanza la kifungu hiki tutajifunza jinsi ya kuponya wagonjwa; sehemu ya pili tutaangalia jinsi ya kutoa pepo; katika sehemu ya tatu tutajadili jinsi ya kupambana na kuyashinda "mapepo ya maeneo"' na katika somo la mwisho tutajadili jinsi ya kuwaongoza watu kubatizwa kwa Roho Mtakatifu. Nia yetu ni kujifunza masomo haya vema, kisha tutaenda kuyatenda yale tuliyojifunza. Mungu akubariki unapoendelea katika vipindi hivi vitatu vya kuburudisha.

Kama ulivyosoma hapo juu, makusudi ya somo hili ni kutoa maelekezo jinsi ya kuponya wagonjwa. Njia ambayo tutapendekeza hapa ni ya kimaandiko na kichungaji. Tunasema ni ya "kimaandiko" kwa sababu inatokana na jinsi walivyofanya Yesu na mitume. Tunasema ya kwamba ni ya "kichungaji kwa sababu tutaanza maelekezo kutoka muangalio wa kuchungaji. Tofauti na mwinjilisti wa mikutano ya nje, mchungaji mara nyingi anahusika na kuomba, si kwa makundi ya watu kwa ujumla bali kwa mtu mmoja kwa wakati. Mtu anayemwombea ni mtu anayemfahamu, anayempenda, na anayehusiana naye katika maisha ya kila siku. Mchungaji wa kweli anahusika sana na mahitaji na hali ya yule anayemhudumia. Lengo lake ni kwamba,kwa vyovyote vile katika kumhudumia mtu huyo nia yake ni kumfanya ajisikie na kuona ya kuwa anapendwa zaidi na Mungu, anapendwa zaidi na kanisa kuliko ilivyokuwa kabla ya kuanza huduma hiyo kwake. Mchungaji hawezi kumwingia au kufanya kipapara kwa mtu, wala hawezi kumlaumu au kumlaani kwa kutokuwa na imani,

bali, kama Yesu atamhudumia siku zote katika upendo huku akijali sana hisia ya mtu yule.

MATAZAMIO YA AWALI

Kabla hatujajadili mambo mbalimbali yanayohusika na kuponya wagonjwa, tutaelekeza umuhimu wa matazamio ya awali. Kabla ya yote tutajadili kile tunachoita "mazingira ya uponyaji."

Mazingira ya Uponyaji

Kwa kusema "mazingira ya uponyaji" tunakuwa tunazungumzia hali ya kiroho inayozunguka mahali pa huduma hiyo. Huduma hiyo inaweza kujumuisha kuponya wagonjwa, kutoa pepo au huduma yeyote inayohitaji udhihirisho wa nguvu za Roho. Mhudumu anapokaribia kuanza huduma na namna hiyo ni muhimu kutambua pia swala hilo la mazingira ya uponyaji.

Katika injili yake, Luka alizungumzia habari ya mazingira hayo ya uponyaji ambayo ilikuwepo katika huduma ya uponyaji ya Yesu. Sikiliza maneno yake: "Wakakutanika makutano wengi wamsikilize na kuponywa magonjwa yao… Na uweza wa Bwana ulikuwapo apate kuponya" (Luka 5:15, 17). Tambua hapa kwamba Yesu alihudumu uponyaji katika mazingira yaliyojaa uwepo wa kimungu: "nguvu ya Mungu ilikuwapo."

Wakati fulani, alipotoka kumfufua binti Lazaro kutoka kwa wafu, tunamwona Yesu akijihusisha na mazingira ya kiroho yaliyoizunguka huduma yake:

> Alipokwisha kuingia, akawaambia, mbona mnafanya ghasia na kulia, kijana hakufa, amelala tu, wakamcheka sana. *Naye alipokwisha kuwatoa nje wote,* akamtwaa babaye wa yule kijana na mamaye, na wale walio pamoja naye, akaingia ndani alimokuwamo yule kijana, akamshika mkono kijana, akamwambia, 'Talitha, kumi! … Mara akasimama yule kijana akaenda.' (Mk 5:39-42, msisitizo omeongezewa)

Tambua hapa ya kwamba kabla Yesu hajafanya muujiza ule, kwanza aliwaweka nje wale wote waliokuwa hawaamini na ni kinyume na huduma yake.

Alikuwa kwa maneno mengine, anatengeneza mazingira ya kiroho.[33]

Taarifa mbili za injili zinaeleza ya kuwa wakati fulani Yesu alizuiliwa kuitimiza huduma yake kwa sababu ya mazingira ya kutokuamini. Biblia inasema kwamba ilikuwa ni nyumbani kwa ke Nazareti,

> Wala hakuweza kufanya muujiza wowote huko, isipokuwa aliweka mikono yake juu ya wagonjwa wachache akawaponya. Akastaajabu kwa sababu ya kutokuamini kwao. (Mk 6:5-6: Mt 13:58)

Kutokana na matukio haya tunaweza kusema ya kuwa yapo mambo mawili yanayotujulisha mazingira ya uponyaji:

1. Uwepo wa Mungu. Kwanza, mazingira ya uponyaji yanatambulikana kwa uwepo wa Mungu. Hapa hatusemi kuhusu tabia ya Mungu kwamba yupo kila mahali nyakati zote, bali hapa tunasema jambo tofauti kidogo. Tunamaanisha uwepo wa Mungu unaodhihirika wazi. Uwepo wa jinsi hiyo ulizungumzwa katika Luka 5:17 hapo juu: "uwepo wa Bwana ulikuwapo apate kuponya."[34]

2. Imani yenye Matumaini. Jambo lingine, mazingira ya uponyaji yanategemea uwepo wa imani yenye matumaini. Imani hii yenye matumaini ni namna ya imani iliyodhihirika kwa yule mwanamke katika Marko 5:28, aliposema: "Nikiyagusa mavazi yake tu nitapona." Imani yenye matumaini ni imani inayokuwepo wakati watu wanapotegemea muujiza kutoka kwa Mungu. Mhudumu mwenye hekima anaweza, akahubiri ujumbe wa injili huku akisisitiza kuhusu imani na uponyaji, akasaidia kuumba imani yenye matumaini katika mioyo ya watu.

Maandalizi ya Binafsi ya Mtumishi

Hata kama katika Sura ya 5 tumezungumzia kwa ujumla kuhusu matayarisho kwa ajili ya huduma yenye nguvu, tunaona ni muhimu kuzungumza tena hapa kuhusu maandalizi kwa ajili ya huduma ya uponyaji. Yapo mambo sita ambayo

---

[33]Soma Matendo 9:40, utaona Petro akifanya jambo la jinsi hiyo hiyo alipomfufua Dorkasi kutoka kwa wafu.

[34]Kwa ajili ya mifano mingine ya uwepo wa Mungu angalia Kutoka 3:1-6; 2Nyakati 7:1-3; Luka 2:8-9; Matendo 2:1-13; Matendo 4:31 na 1Wakorintho 14:22-25.

mtu anaweza kuyafanya ili kujiandaa kwa ajili ya huduma hiyo.

1. *Omba kwa ajili ya ujazo mpya wa Roho Mtakatifu.* Omba hadi unapousikia upako wake.
2. *Jikumbushe Yesu ni nani, amefanya nini na amekuagiza ufanye nini.* Usisahau kwamba ni kwa njia ya Yesu tu, na imani katika yeye, kwamba ushindi unaweza kuja.
3. *Angalia ya kwamba umejishusha "ubinafsi."* Kumbuka ya kwamba, wewe mwenyewe huwezi kutenda neno lolote (Yn 15:5).
4. *Jaribu kuondoka katika mawazo yako mwenyewe kuhusu uponyaji au ukombozi ambao utatokea.* Tambua ya kwamba hakuna huduma mbili zilizofanana, uponyaji ulikuwa tofauti katika huduma hizo.
5. *Muulize Mungu, Je! Unataka nifanye nini?* (Angalia: Yn 5:19-20). Ukiisha tu kugundua mapenzi ya Mungu katika jambo, jitoe kikamilifu katika mapenzi yake. Ndipo sasa unaweza kuendelea katika ujasiri wa imani.
6. *Mara zote omba katika Roho Mtakatifu, ukisikiliza nyakati zote sauti yake inavyokuelekeza.*

Jinsi Upako wa Huduma Unavyokuja

Katika Sura ya 6, "Roho Mtakatifu na Huduma yenye Nguvu", tulisema karama za Roho, hujumuisha karama tatu za nguvu, na huja kama "upako" wa Roho Mtakatifu. Je! Upako huo unakujaje juu ya mtu kwa ajili ya huduma" Wengine wameshuhudia uwepo wa nguvu kutoka ndani, au nguvu ijayo kwa ghafla, "joto," au "msisimko". Wengine wanasema upako huja kwa hali ya huruma nyingi kwa ajili ya yule anayehudumiwa, au uhakika mkubwa ya kwamba kazi itafanyika. Katika vitabu vya injili mara nyingi tunamwona Yesu "akijawa na huruma" kabla ya kuponya wagonjwa (Mk l 1:41). (Tutaangalia somo hili baadaye). Bado wengine hushuhudia ya kwamba pamoja na hisia hizo za ndani mara nyingine huja "ufahamu" kwamba Mungu anataka uponyaji ufanyike, au imani ya ghafla yenye uhakika ya kwamba Mungu ataponya au kutenda muujiza. Hata hivyo upako ukikujia binafsi utahisi katika roho yako kwamba Roho wa Mungu anatenda kazi katika jambo hilo.

JINSI YA KUPONYA WAGONJWA

Tunapendekeza hatua tatu za mtindo wa kichungaji wa kuponya wagonjwa. Hii ni njia ya kawaida ambayo inafanana na huduma ya uponyaji ya Yesu na mitume. Njia hii inahitaji kujibu maswali matatu ya muhimu kuhusu huduma ya uponyaji: Je! Ni nini hasa hitaji la mtu? Je! Nitaitendaje huduma? Je! Nitamshauri vipi mtu huyu baada ya huduma kutendeka:

Hatua Tatu za Mtindo wa kichungaji wa Kuponya Wagonjwa

1. Hatua ya 1: Mahojiano. Hatua ya kwanza katika huduma ya uponyaji ni kugundua hitaji kamili la mtu. Mara nyingi huwa tunaanza mara moja kuomba, hata bila kufahamu tuombee jambo gani. Jambo hili ni ujinga na pia ni hatari, kwa sababu mara nyingi tunaombea jambo lisilohusu tatizo, na matokeo yake mtu huondoka pasipo kutatuliwa tatizo lake. Kwa hivyo ni lazima tuanze huduma ya uponyaji kwa kuuliza maswali.

Swali zuri la kuanzia kwa mtu aliyekuja kwa ajili ya hitaji la uponyaji ni "Je! Ungehitaji Mungu akutendee nini?" Baada ya kuuliza swali hilo, ni vema tusikilize kwa makini sana jibu la mtu huyo. Tunahitaji kusikiliza kwa njia nne: kwa masikio yetu, kwa macho yetu, kwa moyo na kwa roho zetu. Kwa masikio yetu tunamsikiliza vema mtu huyo anasema nini, kwa macho yetu tunaangalia kama Mungu tayari anatenda nini, na jinsi gani mtu anaonyesha dalili za uitikio kwa Mungu. Kwa mioyo yetu tunajisikia maumivu yake na tunahisi imani yake; na roho zetu tunasikiliza kwa makini sana kama Roho wa Mungu anatuambia nini.

Kabla ya kuendelea na huduma lazima tufanye maamuzi ya aina mbili. Kwanza, lazima "tutoe uamuzi wa kiuganga," yaani tuamue tatizo ni nini. Halafu lazima tufanye "uamuzi wa huduma"; yaani ni kwa jinsi gani tutaendelea na huduma.

a. Uamuzi wa kiuganga. Katika uamuzi wa kiuganga tunaamua ni nini tatizo la mtu huyo na ni nini chanzo cha tatizo lake. Kabla ya kuanza huduma ya uponyaji tunahitaji kujua ni wapi mtu anapoumia, kwa nini ana hali hiyo, na ni kwa jinsi gani tutaendelea na huduma. Je! Chanzo cha ugonjwa ni cha asili au ni mapepo. Jibu la maswali hayo litasaidia kuelekeza ni kwa jinsi gani tuendelee na huduma.

b. Uamuzi wa huduma. Baada ya hapo lazima tuamue tutaendeleaje na huduma. Jiulize mwenyewe, "Je! Ninahitaji kutoa mapepo au kuomba maombi ya imani? Kama nitahitaji kuendelea na huduma, nitumie njia gani ya

kimaandiko?" Hapa ni muhimu sana tuendelee kuwa na hisia kali kwa uongozi na sauti ya Roho Mtakatifu.

2. Hatua ya 2: Kuhusika na Huduma. Hatua inayofuata katika huduma ya uponyaji ni ile tunayoiita "kuhusika na huduma." Sasa tunatenda kutokana na uamuzi wa kiganga na uamuzi wa huduma. Katika hatua hii tunaweza kuendelea kwa kumwomba Roho Mtakatifu aje na kudhihirisha uwezo wake. Sasa ndipo tunapohudumu uponyaji kwa njia ya kuweka mikono, maneno ya imani, amri ya imani, matamko, maombi, mafundisho na uachiliaji wa nguvu, maombi ya mapatano, kufunga na kufungulia au njia nyingine za Biblia. (Tutajadili kati ya njia hizi katika sura ijayo).

Ni muhimu kukumbuka ya kwamba tunapoendelea na huduma, ni lazima tuendelee wakati wote kuwa macho ya kile Mungu anachofanya. Uwe macho kwa dalili zozote za utendaji wa Roho. Jiulize,"Je! Mungu anafanya nini sasa hivi katika swala hili?" Unaweza kumuuliza anayehudumiwa kwamba "Unajisikiaje? Je! Maumivu yametoka, au je! Unahisi kuwa jambo lolote linatokea?" Jinsi unavyogundua nini Mungu anafanya kwa mtu huyo endelea kuhudumu, kufuata uongozi wa Roho.

Ni muhimu tusisimame mapema katika huduma hiyo ya uponyaji. Wakati mwingine uponyaji huchukua muda mrefu (Mk 8:22-25). Endelea kuomba hadi mtu amepona au unahisi mtiririko wa Roho umesimama.

3. Hatua ya 3: Maelekezo baada ya Maombi. Huduma yetu inakuwa haijamalizika hadi tumetoa maelekezo baada ya huduma hiyo ya maombi kwa mtu tuliyemwombea. Yesu pia alifanya hivyo.[35] Kama mtu amepokea uponyaji, mtie moto aendelee katika imani na utii. Kama amepona kwa sehemu tu -- na hii ndivyo ilivyo mara nyingi --mtie moyo amwamini Mungu kwa ajili ya utimilifu wa uponyaji huo. Kama hapokei uponyaji, mhakikishie kuwa upendo wa Mungu na nguvu ya uponyaji wa Yesu vinaendelea. Mhakikishie ya kuwa utaendelea kumwombea na unaamini Mungu pamoja naye kwa uponyaji wake. Pia unaweza kumwambia arudi tena kwa kipindi kingine cha maombi.

[35]Mfano wa Yesu alipotoa maelekezo baada ya maombi angalia Yn 5:14; Mk 5:19; na Yn 9:35-39.

Jinsi Yesu Alivyoponya Wagonjwa (Njia ya Biblia ya Kuponya Wagonjwa)

Je! Yesu aliwaponyaje wagonjwa? Hili ni swali la muhimu kwa sababu Yesu ndiye mfano wetu kwa ajili ya huduma. Tukiichunguza huduma ya uponyaji ya Yesu, hiyo inakuwa ndio mfano wa huduma zetu za uponyaji.

Kuhusu huduma ya uponyaji ya Yesu, Jim Miller amesema: "Jambo la muhimu ambalo linajionyesha lenyewe unapochunguza njia ambazo Yesu aliponya wagonjwa: Hakuwaponya wagonjwa kwa namna ile ile mara mbili. Hata hivyo pia ni muhimu kuona ya kwamba alitumia njia kadha tu, hakutumia zaidi ya njia kumi mbalimbali"[36] Katika ratiba zake mbili, "Huduma ya Uponyaji ya Kristo na "Njia Zilizotumika na Kristo katika Huduma yake ya Uponyaji," Miller anaandika ya kwamba vitabu vya injili vinaonyesha rekodi 41 tofauti za uponyaji wa Yesu (kadhaa zikiwa za uponyaji zaidi ya mmoja). Sehemu kubwa ya maandiko yanayofuata yalipatikana kwa njia ya kuzisoma ratiba hizo (Angalia hitimisho ! Na 2)

1. Kusema neno. Njia mojawapo ya Yesu katika kuponya wagonjwa ilikuwa ni kwa njia ya kutamka neno kwa yule aliyekuwa akiponywa.

- Wakati mwingine hii ilikuwa *ni amri kwa mtu mgonjwa kufanya jambo fulani:*
  "Simama ujitwike godoro lako, uende" (Yn 5:8);
  "Nyosha mkono wako" (Mk 3:5);
  "Akasema, kijana, nakuambia, inuka" (Lk 7:14).

- *Nyakati nyingine ilikuwa ni amri kwa mapepo:*
  "Fumba kinywa, mtoke!" (Mk 1:25);
  "Ewe pepo mchafu mtoke mtu huyu!" (Mk 5:8);
  "Ewe pepo bubu na kiziwi, mimi nakuamuru mtoke huyu, wala usimwingie tena: (Mk 9:25).

- *Nyakati nyingine alisema moja kwa moja kwa ule ugonjwa au hali ile:*
  "Nataka takasika!" (Mt 8:3; Mk 8:41);

[36]Jim Miller, "Jinsi ya kuponya wagonjwa, (maandiko yasiyochapishwa), uk.3.

"Upewe kuona" (Lk 18:42);
"Funguka!" (Mk 7:34).

- *Nyakati nyingine neno lake lilikuwa ni kuitikia kwa ajili ya imani ya mpokeaji uponyaji:*
  "Imani yako imekuponya" (Mt 9:22);

- Au tamko rahisi lililoonyesha ya kuwa uponyaji umetokea:
  "Umefunguliwa katika udhaifu wako" (Lk 13:12);
  "Mwanao yu hai" (Yn 5:50).

2. Kugusa na kuweka mikono. Njia nyingine ya kawaida ambayo Yesu alitumia kuponya wagonjwa ilikuwa kugusa au kuwawekea mikono wagonjwa:

"Akamgusa mkono, homa ikamuacha" (Mt 8:15);
"Yesu… akawagusa macho yao; mara wakapata kuona. . ." (Mt 20:34);
"Yesu akatia vidole masikioni mwake...akamgusa ulimi. Mara masikio yake yakafunguka, kifungo cha ulimi wake kikafunguka. . ." (Mk 7:33-35);
"Akaweka mikono yake juu ya kila mmoja, akawaponya" (Lk 4:40).

3. Imani. Nyakati nyingine Yesu alijibu ili kuonyesha ya kuwa imani ilikuwa ndiyo kiungo kilicholeta uponyaji.

- Nyakati nyingine alitambua imani ya mpokeaji wa uponyaji:
  "Enenda… imani yako imekuponya" (Mk 10:52); "Mama, imani yako ni kubwa, na iwe kwako kama utakavyo." (Mt 15:28).
- Nyakati nyingine alitambua imani za wengine: "Naye Yesu alipoiona imani yao [rafiki za aliyepooza]" (Mk 2:5).

4. Huruma. Kama ilivyoandikwa hapo juu, maandiko mara nyingine huonyesha wazi ya kuwa huruma ni kiungo cha muhimu katika kuponya wagonjwa:

"Akawahurumia akawaponya wagonjwa wao (Mt 14:14); "Naye akamhurumia akanyosha mkono wake akamgusa" (Mk 1:41-42);
"Bwana alipomwona alimwonea huruma… akaligusa jeneza. . .yule maiti akainuka, akaketi akaanza kusema" (Lk 7:13-15).

5. Kuachilia Nguvu. Biblia inaonyesha waziwazi ya kuwa Yesu alifanya kazi zake zote katika nguvu za upako wa Roho Mtakatifu (Mdo 10:38; Lk 5:17). Miujiza yake mingi ilitendeka kutokana na uachiliaji wa nguvu iliyotiririka kutoka kwake hadi kwenye miili ya wagonjwa na kuleta uponyaji:

> "Uweza ulikuwa ukimtoka ukiwaponya wote" (Lk6:19); "Kuna mtu amenigusa; ninajua kwa sababu nguvu imenitoka" (Lk 8:46).

6. Jina la Yesu. Ulinganifu makini wa uponyaji uliofanywa na mitume katika kitabu cha Matendo unaonyesha ya kuwa wao pia waliiga njia zake za uponyaji; hata hivyo, kulikuwepo na ongezeko moja la muhimu. Wao walifanya katika jina la Yesu (Mk 16:17-18; Mdo 4:10). Leo, sisi pia inatubidi tuige njia za Yesu pamoja na ongezeko hili la muhimu kabisa—lazima tufanye katika nguvu kuu ya Jina la Yesu!

MWISHO

Sisi kama watumishi wa Kristo, tumepewa agizo la wazi. Tunatakiwa tuhubiri injili, na kuponya wagonjwa. Pia , Yesu ametupa mfano mzuri wa jinsi ya kufanya hivyo. Kazi yetu ni kutoka kwa imani na utii, tukiiga njia zake na kumtegemea yeye kulihakikisha neno lake kwa ishara zitakazofuatana.

— Sura Ya Kumi —

Jinsi Ya Kutoa Mapepo

UTANGULIZI

Kanisa linapokwenda duniani na injili, moja ya agenda zake za kazi ni kupambana na kuzishinda nguvu za giza katika jina la Yesu. Inafurahisha kuona ya kuwa muujiza wa kwanza wa Yesu ulioandikwa katika injili ya unahusu kutoa pepo (Mk 121-27), na pia ishara ya kwanza itakayofuatana na watu walioamini iliyonenwa katika agizo kuu katika Marko (16-15-18) ni "kwa jina langu watatoa pepo..." (Mstari 17). Katika Sura ya 3, "Huduma yenye Nguvu na Ufalme wa Mungu," tulizungumzia jinsi kuja kwa ufalme wa Mungu duniani kutakavyoleta mapambano na shetani na majeshi yake ya mapepo. Majeshi haya ya uovo yatapinga kuja kwa ufalme wa Kristo iwe katika eneo la mahali au katika maisha ya mtu binafsi. Kwa hiyo mapepo ni lazima yapingwe na kutolewa popote pale yatakapoonekana na mhudumu wa injili

Katika sura ijayo tutazungumzia jinsi ya kushindana na kuyashinda mapepo yanayowaonea na kuwaweka katika hali ya utumwa watu wa eneo la mahali fulani. Katika sura hii tutazungumzia jinsi ya kuyatoa mapepo yaliyopagaa miili na maisha ya watu tunaokutana nao katika huduma ya injili. Hata hivyo, kabla hatujajadili jinsi ya kuyatoa mapepo, tutaangalia kwanza kwenye Biblia ili tugundue jinsi mapepo yalivyo, na jinsi yanavyowapagaa na kuwatesa mateka wao.

KUWAELEWA MAADUI ZETU

Mapepo ni Nini

1. Chanzo cha kuwepo kwa mapepo. Watafsiri wa Biblia wa kiinjili mara nyingine hukataa kukubaliana kuhusu chanzo cha mapepo. Wengine husema ni roho wasio na miili wa kizazi kilichokuwepo kabla ya kuumbwa Adamu; wengine wanabishia na kusema kutokana na ushahidi wa Biblia, mapepo bila shaka ni wale malaika waliotenda dhambi wakaanguka pamoja na shetani katika uasi wake dhidi ya Mungu (Mt 25:41; Ufu 12:9). Jambo moja ambalo tunaweza kuwa na uhakika nalo ni uwepo wa mapepo yenyewe. Biblia, na hasa injili nne, hazina shaka kuhusu uwepo huo. Pia tuna uhakika wa kazi zake. Kazi hizo kutokana na Wilbur Odonovan ni pamoja na kuwapa "nguvu watu watenda dhambi (kama wachawi) wanaotafuta nguvu za kimiujiza dhidi ya watu wengine."[37] Yesu mara nyingi alipambana na kuyatoa mapepo. Halafu akatuambia sisi, kanisa lake, tutahusika katika huduma ya jinsi hiyo hiyo (Mk 16:17; Lk 9:1-2).

2. Tabia za Mapepo. Je! Mapepo yakoje? Je! Asili yao na tabia zao zikoje? Biblia inafundisha mambo yafuatayo kuhusu asili na tabia ya mapepo:

a. Ni viumbe vilivyo hai (Mdo 16:16-17; Lk 4:33-35; 8:28-31; Yak 2:19). Sio tu nguvu zisizo na uhai, zilizopo au zinazofikiriwa. Ni viumbe halisi vilivyo hai vyenye ufahamu, utashi

b. Ni roho (Mwa 3:1; Ufu 16:13). Ni roho ambao hawana miili wanatafuta kuishi katika miili ya wanadamu.

c. Wana nguvu. Wana ufahamu, uwezo na nguvu (Lk 8:29; Mdo 16:16-17; 2Thes 2:9). Lakini hata kama wana nguvu, wakati huo huo nguvu hizo zina kipimo tofauti na Mungu, ambaye ni mwenye nguvu zote na hakuumbwa, wakati mapepo yameumbwa na nguvu kiasi. Hayana uwezo kwa namna yoyote wa kumlingana Mungu.

d. Ni maovu. (Mk 1:23; Efe 6:12). Yana tabia iliyo ya kiwango cha chini kabisa, ni maovu kupita kiasi, makatili tena yaliyobobea katika kila uovu.

3. Malengo ya Mapepo. Kama wakristo wanavyopenda kutimiza mapenzi ya Baba yao wa mbinguni, mapepo pia yanatafuta kutimiza mapenzi ya baba yao,

---

[37]William O. Donovan, Jr., Introduction to Biblical Christianity from an African perspective. (Ilorin, Nigeria: Nigeria Evangelical Fellowship, 1992), uk. 235.

shetani. Inaonekana ya kwamba moja ya malengo ya kwanza kabisa ya shetani ni kujaribu kupambana na Mungu na kumletea madhara ya kumuumiza, mapepo pia yanashiriki kusudi hilo. Yakijua ya kuwa hayawezi kushindana na Mungu wala kumdhuru moja kwa moja, shetani na mapepo yake wanajaribu kumdhuru Mungu kwa njia ya kuwaumiza na kuwatia uwete wale ambao Mungu anawapenda—kizazi cha wanadamu. Kwa hiyo kusudi la msingi la mapepo ni kumshambulia mwanadamu (hivyo kinyume cha Mungu) kwa kuiingilia miili ya wanadamu, nafsi na roho. Hufanya hayo kwa njia kama tatu hivi:

a. Kwa kutafuta wanadamu wayaabudu (1Kor 10:19-21). Mapepo yanataka abudu ambayo Mungu anastahili.

b. Kwa kutafuta kumweka mtu katika utumwa wa woga, ugonjwa na tabia mbalimbali zinazomfunga. Kwa namna hii yanaharibu ule mfano wa Mungu katika mwanadamu.

c. Kwa kumtia upofu mwanadamu katika kweli ya injili (Ebr 2:14; Mdo 10:38; 2Kor 4:4; 2Tim 2:25). Kwa namna hiyo yanamwondoa mwanadamu katika ushirika na Mungu kwa wakati uliopo na katika umilele.

Katika kitabu chake *Introduction to Biblical Christianity* from an African perspective,' Wilbur O'Donovan, Jr. ameorodhesha shughuli mbalimbali ambazo mapepo yanajihusisha nazo. Hapa nimeorodhesha kati ya shughuli hizo pamoja na maelezo yake:

- *Udanganyifu.* Kwa njia ya uongo mapepo yanaleta chuki, dini za uongo, na hata mafundisho ya uongo kanisani (Yn 8:44; 1Tim 4:1; 2Pet 2:21).
- *Fujo na mauaji.* Kama yakiachiwa kutimiza mapenzi yao mabaya mapepo huleta fujo, madhara, na hata vifo kwa mateka wao (Yn 8:44).
- *Mateso.* Mapepo hutesa watu na kuwapiga upofu, ububu (Mt 12:22), uharibifu wa viungo (Lk 13:11-17); ugonjwa (Ayu 2:7; Mdo 10:38), na kuharibikiwa akili (Lk 8:27-29).
- *Zinaa.* Biblia mara nyingi huzungumzia jambo la "pepo wachafu" kuelezea uchafu wao kizinaa na ambavyo yanawasha tamaa za watu ambao yamewapagaa (Mt 10:1; Mk 1:23; 3:11).
- *Kizuia kazi ya Injili.* Kama tulivyokwisha kutaja hapo juu, mapepo hukazana kupinga maendeleo ya injili wakati wowote yapatapo nafasi (1Thes 2:18; Efe 6:12).
- *Kuwavuruga watu wa Mungu* (Lk 22:31; 2Kor 12:7). Mapepo hutafuta njia ya kuwavuruga, kuleta matatizo, kusumbua na kuwakatisha tamaa

watu wa Mungu popote yanapoweza.

- *Kuendeleza uchawi na kuabudu sanamu* (Kumb 32:16-17; 1Sam 15:23). Mara nyingi huwa ni mapepo yanayokuwa nyuma yakiongoza na kutia nguvu uchawi, na kuabudu mababu kama tunavyoona duniani leo (1Kor 10:19-20).[38]

Kupagawa na Mapepo

Mapepo yanatafuta kuwaandama na kuwatawala mateka wao katika njia kadhaa. Njia kuu ya shambulio la mapepo linaitwa "kupagawa na mapepo" katika Biblia zetu. Wakati pepo (au mapepo) yanapompagaa mtu, yanamwingia mtu na kuyatawala maisha yake. Kumtawala huku kunaweza kuwa ni kumtawala kwa sehemu tu au kumtawala kabisa. Kunaweza kuwa ni kwa muda au kwa wakati wote. Kupagawa kwa pepo humdhuru mtu katika hali mbaya sana, zifuatazo ni kati ya hali hizo:

1. Mabadiliko ya mtu, au wingu linalompunguza ufahamu (Mk 9:26).
2. Mamlaka nyingine huzungumza katika mtu aliyepagawa (Lk 8:28-30).
3. Nguvu Nyingi mwilini (Lk 8:29).
4. Elimu isiyoelezeka, au nguvu za kichawi (Mdo 16:16-17).
5. Usumbufu katika mwili (Mk 1:26), ni pamoja na uziwi na upofu (Mt 12:22-30; 9:32-34).
6. Kujidhuru au kujiua (Mk 9:22, 5:5).
7. Kuhamasika au woga wa Kristo na jina lake (Mk 1:24).

Wengine husema ya kwamba mkristo anaweza kupagawa na pepo. Wengine wanakataa jambo hili. Je! Ukweli ni upi? Je! Mkristo anaweza kupagawa? Jibu ni, sivyo, mkristo hawezi kupagawa na pepo. Hata kama mkristo anaweza kujaribiwa, kudanganywa, kushambuliwa na hata kuonewa na mapepo kwa hali ya nje ya mwili wake, haiwezekani kwa mkristo kupagawa (pepo kuishi ndani yake/au kutawaliwa ufahamu wake) na pepo. Zipo sababu nne zinazokubaliana na jibu hili. Kwanza kabisa katika Agano Jipya hakuna rekodi ya mkristo aliyezaliwa mara ya pili kupagawa au kutolewa pepo. Pili, katika maandiko kuna sababu kamili za kuamini ya kuwa ukombozi kutokana na mapepo mara nyingi

[38]O'Donovan, kurasa 231-235.

ulitokea wakati wa mtu kuokoka.[39] Tatu, hatuoni popote katika nyaraka kupagawa kukiwa tatizo la wakristo au wakristo wakionywa kuhusiana na jambo hilo. Na hatimaye, tunahitaji tukumbuke ya kuwa, ingawa mkristo hawezi kupagawa na pepo, kupagawa kunawezekana kwa mkristo aliyerudi nyuma au aliyeikana imani. Wengi, katika uzoefu wangu, ambao wanasema ya kuwa wamewahi kushughulikia "mkristo aliyepagawa na pepo" walikuwa kwa kweli, wanashughulika na wakristo waliorudi nyuma au walioikana imani.

Shetani, Adui Aliyeshindwa

Katika kushindana na mapepo ni muhimu kushika ukweli wa namna mbili. Kwanza, lazima tusije tukasahau ya kwamba nguvu ya shetani katika nyakati hizi imezuiliwa vikali sana na Roho Mtakatifu (2Thes 2:7). Kwa njia ya nguvu za Roho tunazo nguvu za kumwamuru shetani. Pili, lazima tusije tukasahau ya kwamba, nguvu za shetani na mapepo yake zilivunjwa kabisa pale Kalvari (Yn 12:31). Sikiliza maneno haya ya mtume katika Kol 2:15: "Akiisha kuzivua enzi na mamlaka, na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba huo."

"Nguvu na mamlaka" zilizozungumzwa katika mstari huu ni nguvu za shetani na mapepo duniani. Msalabani Yesu alivunja mgongo wa shetani. Shetani na mapepo yake sasa ni maadui walioshindwa kwa sababu ya kazi kuu ya Yesu pale msalabani.

JINSI YA KUTOA PEPO

Sasa tunaelekea katika kichwa cha kutoa mapepo. Kabla hatujasema kuhusu jinsi ya kutoa mapepo, lazima kwanza tuzungumze kuhusu mhudumu mwenyewe wa ukombozi huo.

[39]Tambua hasa maelezo ya Biblia kuhusu uamsho wa Filipo kule Samaria katika Matendo 8:5-8.

Mhudumu wa Kutoa Mapepo

Kuna mambo ya muhimu ambayo mtu yeyote anayehitaji kuhusika katika huduma ya ukombozi anahitaji kufahamu jinsi ya kufanya. Hapa chini yameorodheshwa mambo matano ya muhimu kwa mhudumu wa ukombozi huo:

1. Lazima atambue kuwa kutoa pepo ni vita kamili na ya uhakika, dhidi ya shetani, hivyo asichukulie vita hiyo kirahisi tu.
2. Kwa sababu vita ni ya kiroho, ni muhimu sana awe amejazwa na Roho Mtakatifu.
3. Lazima pia awe amejitoa kabisa kuwa chini ya mapenzi ya Mungu (Yak.4:7).
4. Lazima awe na ufahamu kamili juu ya silaha za vita vyake (Efe 6:10-18) na pia lazima afahamu jinsi ya kutumia silaha hizo katika vita vyake.
5. Lazima awe na imani iliyo hai katika ushindi wa Kalvari, damu ya Kristo, na ushindi uliomo katika Kristo.

Kuhudumia Ukombozi Kutokana na Mapepo

Sisi kama watumishi wa Kristo, tumetumwa na kuvikwa silaha ili kuhudumu ukombozi kwa wale ambao wameonewa na nguvu za mapepo. Kumbuka, Yesu ni mfano wetu na kiongozi wa vita hivyo vya kiroho Angalia: Luka 4:18-19; 31-37) na ametuagiza tumfuate katika vita hivyo (Marko 16:15-18).

Sio tu kwamba Yesu ametuagiza, bali pia ametupatia silaha za kuhudumu ukombozi kwa walioonewa. Kwa njia ya kujazwa karama za Roho Mtakatifu (yaani karama za ufunuo, hasa ile ya kupambanua roho) tumepewa uwezo wa kuwatambua na kuwaweka wazi mapepo. Pia tumepewa nguvu na mamlaka ya kuwaamuru na kuwatoa mapepo (Luka 9:1-2; 10:17-19).

Jinsi ya Kutoa Mapepo

Kutoa mapepo na kuvunja vifungo vya mapepo ni kazi ya Mungu kwa njia ya Roho Mtakatifu. Ni ishara ya uwepo wa ufalme wa Mungu na pia ni udhihirisho wa nguvu na ubwana wa Yesu juu ya dunia hii. Kama ilivyo katika uponyaji wa wagonjwa, mambo matatu yafuatayo yanahusika katika ukombozi:

1. Mahojiano (uvumbuzi). Endapo mahojiano yanawezekana -- ingawa huwa siyo hivyo mara nyingi -- basi hapo itakuwa ndiyo hatua ya kwanza katika shughuli ya ukombozi. Ni katika hatua hii ya kutaka kugundua tatizo ambapo kwa njia ya karama ya kupambanua ruho, tunaweza kugundua uwepo wa kazi ya mapepo. Pia mara nyingine mapepo yakihamakishwa na uwepo wa Mungu,

hujidhihirisha yenyewe kama yalivyofanya katika huduma ya Yesu (Mk 1:23; 5:6-7).

Kabla ya ukombozi kuanza, mara nyingi ni vema, inapowezekana kumhitaji yule anayehitaji kukombolewa kujikabidhi kwa Mungu. Mwongoze kwa njia ya maombi, sala ya toba na kuzitubia dhambi zake, hasa dhambi zile ambazo zinakaribiana au kuhusiana na kufungwa kwake mapepo. Hapa ni lazima azikane kwa ujasiri pia ayakatae mapepo, na kazi zote za mwili katika maisha yake.

2. Utendaji wa huduma. Kufikia sehemu hii mhudumu anaweza sasa kuingia katika huduma yenyewe ya mapambano dhidi ya nguvu za mapepo. Anaweza kuamua kuanza kuliitia jina la Yesu na kuja kwa Roho Mtakatifu. Mara anapohisi uwepo wa Mungu anaweza kuendelea kutoa pepo. Moja au zaidi ya njia moja kati ya zifuatazo zaweza kutumika:

- Anaweza kuyafunga mapepo katika jina la Yesu (Mt 16:17-19; 18:18).
- Anaweza kuyaamuru mapepo yatoke, au yamwachilie mtu huyo (Lk 4:35).
- Anaweza pia kuyaamuru mapepo yasimrudie mtu huyo tena (Mk 9:25).

Nyakati nyingine huwepo mapambano na kukatalia kwa mapepo (Lk 8:29; 11:14). Katika hali kama hizo mhudumu lazima akakamae kwa imani hadi ushindi utakapokuja. Ukombozi mara nyingi huandamana na udhihirisho wa mapepo kwa aina nyingi (Lk 4:33-35; 9:42; Mk 7:30). Katika hali kama hizo mhudumu anatakiwa asitahayari wala asiyumbishwe na mbwembwe za namna hiyo, bali aendelee na mapambano katika nguvu za Roho, ili kuyanyamazisha mapepo (Mk 1:25;34), na katika mamlaka aliyonayo katika Kristo, kuyaamuru yatoke na kwenda (Mk 9:25).

Full Life Study Bible (tafsiri mojawapo ya Biblia), katika "Nguvu dhidi ya shetani na mapepo" imetoa hatua zifuatazo kuchukuliwa katika kuwakomboa watu kutokana na vifungo vya mapepo:

- Tambua ya kuwa hatumo katika mapambano dhidi ya damu na nyama bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili (Efe 6:12).
- Ishi mbele za Mungu ukiwa umejitoa katika kweli na haki (Rum 12:1-2; 6:14).
- Uwe na imani kwamba nguvu za shetani zinaweza kuvunjwa katika sehemu yoyote ile ya ufalme wake (Mdo 26:11; Efe 6:16; 1Thes 5:8), Pia utambue ya kwamba mkristo ana silaha za kiroho na zenye nguvu

ambazo Mungu amezitoa kwa ajili ya kuharibu ngome ya shetani (2Kor 10:4-5).

- Tangaza injili ya ufalme katika nguvu za Roho Mtakatifu (Mt 4:23; Lk 1:15-17; Mhu 1:8, 2:4; 8:12; Rum 1:16; Efe 6:15).
- Pingana na shetani ana kwa ana kwa kuamini katika jina la Yesu (Mdo 16:16-18). Kwa kutumia neno la Mungu (Efe 6:17), kwa kuomba katika Roho (Mdo 6:4; Efe 6:18). Kwa kufunga (angalia Mt 10:1; 12:28; 17:17-21; Mk 16:17; Lk 10:17; Mdo 5:16; 8:7; 16:18; 19:12; . . .).
- Omba hasa ili Roho Mtakatifu aihukumu mioyo ya walipotea kuhusu dhambi, haki na kuja kwa hukumu (Yn 16:7-11).
- Omba na uwe na shauku ya udhihirisho wa Roho kwa njia ya karama za uponyaji, lugha, miujiza, ishara na maajabu (Mdo 4:29-33; 10:38; 1Kor 12:7-11).[40]

3. Maelekezo baada ya maombi. Hatua ya mwisho katika ukombozi wa mapepo ni maelekezo baada ya maombi na ushauri. Mara nyingi mtu anapokuwa chini ya kutawaliwa au chini ya nguvu ya mapepo, ushauri na msaada wa maombi baada ya huduma ni vitu vya muhimu. Mtu huyo anahitaji maombi mengi, ushauri na misaada mingine ya kumjenga. Huu badi sio muda wa kumwacha tu mtu huyo; ni wakati wa kumwonyesha kumjali kwa upendo. Pia ni muhimu mara moja kupima hali yake ya kiroho. Kama hajaokoka au kuzaliwa mara ya pili, basi ni vema aongozwe mara moja katika hatua za wokovu. Lazima pia tumwongoze mtu huyo katika hatua za kubatizwa katika Roho Mtakatifu.[41] Yesu alionya kwa vikali jambo la kuzembea mambo haya muhimu:

> Pepo mchafu, amtokapo mtu, hupitia mahali pasipo maji, akitafuta mahali pa kupumzika asipate. Halafu husema, nitarudi nyumbani kwangu nilikotoka; hata akija, aiona tupu, imefagiwa na kupambwa. Mara huenda akachukua pamoja naye pepo wengine saba walio waovu kuliko mwenyewe, nao huingia na kukaa humo; na mtu yule hali yake ya mwisho huwa mbaya kuliko ya kwanza. (Mat 12:43-45a)

---

[40]Full Life Study Bible, New Testament, "Power over Satan and Demons", uk. 81.

[41]Angalia Sura ya 12, "Jinsi ya kuomba na watu wajazwe na Roho Mtakatifu."

Hivyo ni muhimu kwamba hali ya kiroho ya mtu ishughulikiwe baada tu ya ukombozi dhidi ya mapepo. Mhudumu lazima abakie na mawasiliano ya karibu na mtu huyo hadi akombolewe kabisa kutokana na kifungo.

MWISHO

Kama wahudumu wa injili tumeamriwa kutoa mapepo. Lazima tufanye hivyo katika nguvu na upako wa Roho na katika njia ambayo inaonyesha upendo na heshima kwa watu wale tunaowahudumia.

— Sura Ya Kumina Moja —

Jinsi Ya Kupambana Na Kuyashinda Mapepo Na Maeneo

MAPEPO YA MAENEO NI NINI?

Tunapotumia neno "mapepo ya maeneo" tunazungumzia kuhusu mapepo kama tulivyozungumza katika Sura ya 10; ingawa katika hali hii tunazungumzia mapepo yenye maagizo ya namna nyingine na yale yanayowaonea wanadamu. Tunazungumzia kuhusu mapepo yanayotawala na kuhusika na tabia mbalimbali, sio za watu binafsi, bali juu ya maeneo fulani, makundi ya watu, au jamii.[42]

Mapepo Yana Ngazi na Vyeo

Biblia inafundisha wazi ya kwamba mapepo fulani yana vyeo mbalimbali na kazi mbalimbali:

> Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na *mamlaka,* juu wa *wakuu wa giza hili*, juu ya *majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho* (Efe 6:12, angalia pia Kol 2:15).

Uchunguzi zaidi wa Biblia unatuonyesha ya kwamba kati ya mapepo hayo yanayotawala yamepangiwa maeneo fulani, jamii, watu, vikundi, makabila, n.k katika dunia nzima. Kutokana na C. Peter Wagner, "shetani hupanga au kutoa

[42]Kwa sababu wengi wa roho hao wachafu wamepangiwa kutawala sio tu maeneo ya kijiografia, bali pia watu, jamii, mara nyingine huitwa "mapepo watawalao" au mapepo ya jamii."

mamlaka ya juu kwa mapepo yake ya ngazi za juu kutawala nchi, mikoa, miji, watu, vikundi, vitongoji na sehemu za starehe za jamii ya watu katika dunia nzima."[43]

Katika kitabu chake, "Touch the World through Prayer," Wesley Beuwel amesema kuhusu ngazi za vyeo vya mapepo:

> Jinsi shetani alivyoyapanga mapepo katika ufalme wake hatuwezi kufahamu. Maandiko yanatumia majina kadhaa kwa mapepo hayo, katika njia inayoonyesha yako chini ya utawala wa shetani. Hapa kuna kati ya majina hayo katika Kiyunani pamoja na sehemu ambapo maneno hayo yametumika katika Biblia:

Maneno haya yanaweza kuelezea ngazi mbalimbali za mamlaka au vyeo mbalimbali chini ya shetani. Jambo la muhimu ni kwamba hao wote wanazo nguvu za kiasi tu, ufahamu, na pia maeneo ya shughuli. Wahusika wa ngazi hizo zote walishindwa na Kristo msalabani. Na wote wanafahamu kuwa wanasubiri hukumu yao ikatayofuatiwa na hukumu ya milele (Mt 8:29)."[44]

archa	wafalme	(1Kor 15:24; Efe 1:21; 3:10; 6:12; Kol 1:6; 2:10, 15)
exousiai	mamlaka	(1Kor 15:24; Efe 1:21; 3:10; 6:12; Kol 1:16)
dunameis	nguvu	(Rum 8:38; 1Kor 15:24; Efe 1:21)
kuriotes	usultani ubwana	(Efe 1:21; Kol 1:16)
throni	viti vya enzi	(Kol 1:16)
archontes	watawala	(1Kor 2:6)
kosmokratores	wafalme wa dunia	(Efe 6:12)

[43]C. Peter Wagner, "Territorial Spirits," Wrestling with Dark Angels, ed., C. Peter Wagner and F. Douglas Pennoyer, (Ventura California: Regal Books, 1990), uk. 77.

[44]Wesley Deuwel, "Touth the World Through Prayer, (Grand Rapids, MI: Francis Asbury Press, 1986), kurasa 104-105.

Shetani ni Kamanda Wao Mkuu Hawa pepo watawala wako chini ya uongozi wa kamanda wao mkuu, shetani, kwa kuwa Biblia inasema, "Twajua … dunia yote pia hukaa katika yule mwovu: (1Yn 5:19). Kwa neno "dunia yote (Kiyunani, kosmos) Biblia hapa inazungumzia kuhusu mitindo yote inayoendeshwa kidunia, hii ni pamoja na tawala za siasa, dini, elimu, jamii, uchumi n.k. Kutokana na George Otis, Jr., "Lengo la shetani… ni kuupata utawala juu ya maisha ya wanadamu kwa kutawala njia zote za dunia—siasa, uchumi na dini—ambazo wamezitengeneza."[45]

Shetani hutawala kwa kupitia mtandao wenye nguvu wa mapepo "falme" … mamlaka… wakuu wa giza hili … na majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho (Efe 6:12). Otis anaendelea kusema kuhusiana na mtandao huo wa utawala wa mapepo:

> Leo mpangilio wa mapepo ya uovu umetanda juu ya dunia nzima ili kutawala maeneo na watu walio tayari chini ya utawala wa shetani na kupiga vita dhidi ya wale ambao bado hawajawa chini ya utawala huo. Katika maandiko 'watu wenye nguvu' (mapepo yenye ngazi za juu) yanatajwa majina kufuatana na maeneo ambayo yanashikilia. Hii ni pamoja na ufalme wa Uajemi (Daniel 10:13), mkuu wa Uyunani (Daniel 10:20, mfalme wa Tiro (Ezekiel 28:12), Babeli mkuu (ufu 17:3-5). Sehemu nyingine mtawala wa giza ametumia jina la miungu ya eneo fulani kama Beli katika Babeli (Yer 51:44), Baal-Zebubu wa Ekroni (2Waf 1:2-3), na Apolioni wa kuzimu (ufu 9:11).[46]

Katika hitimisho, mapepo ya maeneo ni mapepo ya ngazi za juu yaliyopewa kutawala maisha ya watu kwa kutawala maeneo au jamii ambapo wanakaa.

JE NI NINI KAZI NA SHUGHULI ZA MAPEPO YA MAENEO?

Kazi za Mapepo ya Maeneo

Kama ilivyotajwa hapo juu, kazi ya awali ya mapepo ya maeneo ni kuyashikilia maeneo fulani na kuwaweka watu katika utumwa. Pia yanawatia

---

[45]George Otis, Jr., The Last of the Giants, (Tarrytown, NY: Chosen Books Publishing, 1991), uk. 88.

[46]Ibid, uk. 94.

watu ugumu wa kutoiamini injili na kuokoka (2Kor 4:4). Njia mojawapo wanayofanya ni kutawala au kuwa na uwezo juu ya viongozi na serikali (angalia Ufu 16:14). F. Douglas Pennoyer amezungumzia juu ya "utumwa wa pamoja," uliowekwa juu ya watu na mapepo ya ngazi za juu. Njia moja ambayo mapepo hayo yanaweza kutawala eneo au jamii, anasema, ni kwa kuwatawala na kuwaongoza watu wa jamii hizo:

> …mapepo yanapofanya kazi kupitia watu yanaweza kutawala jamii na kutumia uongozi wa mahali pale kuzuia injili kupenya katika maisha ya jamii ile… Lengo la mapepo ni kuwaweka wawe watumwa katika vifungo vya shetani, katika namna ya utumwa wa pamoja unaokatisha tamaa watu binafsi kujikomboa kwa kupasua katikati ya ufungwa huo hadi kwenye ufalme wa nuru."[47]

Kazi za Mapepo ya Maeneo

Je! Mapepo haya yanazuiaje jamii kutoka katika nuru? Njia moja ni kwa kuwafunga watu kutokana na kweli ya injili:

> Lakini ikiwa injili yetu imesitirika, imesitirika kwa hao wanaopotea; ambao ndani yao mungu wa dunia hii amepofusha fikra zao wasioamini, isiwazukie nuru ya injili ya utukufu wake Kristo aliye sura ya Mungu (2Kor 4:3-4).

Shetani anawezaje kupofusha fikra za ufahamu wa watu billioni tano dunia nzima? Akiwa ni kiumbe aliyeumbwa hawezi kufanya hivyo peke yake; lazima afanye hivyo kupitia mtandao wa utawala na uongozi wa mapepo.

Njia nyingine ambayo shetani anatawala maeneo na jamii ni kwa njia ya asili ya dhambi iliyo katika watu wote kwa kuwafanya wazame katika hali ya dhambi. Watu na jamii wanavyozidi kushuka kiwango chao cha utu pia watazidi kufungwa. Hiyo ndiyo njia yatumiayo mapepo ya maeneo.

JINSI YA KUPAMBANA NA KUYASHINDA MAPEPO YA MAENEO

Sawasawa na mapepo yote, mapepo ya maeneo yanaweza kupingwa katika nguvu na mamlaka ya Jina la Yesu. Kuna njia tatu ambazo tunaweza kupambana

[47]F. Douglas Pennoyer, "Dungeons of Collective Captivity, Wrestling with Dark Angels, (City: Publisher, Date), uk 250.

na kuyashinda mapepo haya yatawalayo ili injili iweze kupenya maeneo yasiyofikiwa.

Kwa "Vita Kali ya Maombi"

Njia ya kwanza ambayo tunaweza kupambana na kuyashinda mapepo ya maeneo ni kwa kile kilichoitwa "vita kali ya maombi." Katika namna hii ya maombi tunakuja kinyume cha mapepo haya tawala katika jina la Yesu na katika nguvu ya Roho Mtakatifu. Kama vile tunavyoamuru mapepo yanayowatesa watu, tunayaamuru mapepo haya pia kuachilia utawala wao juu ya maeneo na jamii. Tunapofanya hivyo tunaita pia nguvu za Roho Mtakatifu kuleta uamsho katika maeneo hayo ya watu. Uwepo wa Roho Mtakatifu utafanyika kizuizi kwa nguvu za mapepo (2Thes 2:7). Maombi ya jinsi hiyo mwisho wake utakuwa "milango iliyofunguka" kama mara nyingi inavyotajwa katika maandiko. (Angalia 1Kor 16:9, 2Kor 2:12; Kol 4:3; Ufu 3:8). Kabla ya kuingia nchi, eneo, mji, kitongoji, au kijiji kuihubiri injili, ni hekima kwamba tupange muda kamili kwa ajili ya vita kali ya maombi ya jinsi hii.

Kwa Kumfunga Mtu mwenye Nguvu

Njia ya pili ambayo tunaweza kupambana na kuyashinda mapepo ya maeneo ni kwa njia ya "kumfunga mtu mwenye nguvu." Yesu alisema kuhusu kutumia silaha hii ya kiroho katika Mathayo na Luka:

> Lakini mimi nikitoa pepo kwa Roho wa Mungu, basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia. Ama awezaje mtu kuingia ndani ya nyumba ya mtu mwenye nguvu na kuviteka vyombo vyake, asipomfunga kwanza yule mwenye nguvu? Ndipo ataviteka vitu vyake (Mt 12:28-29).
>
> Mtu mwenye nguvu aliyejifunga silaha zake, alindapo nyumba yake, vitu vyake ni salama; lakini mtu mwenye nguvu kuliko yeye atakapomwendea na kumshinda amnyang'anya silaha zake zote alizokuwa akizitegemea na kuwagawa mateka yake (Lk 11:21-22).

Je! Ni nani mtu huyu "mwenye nguvu" ambaye Yesu anazungumzia katika sehemu hii ya maandiko? Ni pepo mwenye nguvu anayetawala au mtu binafsi, jamii au eneo fulani. Tambua kuwa Luka 11:21 anazungumzia pepo huyu mwenye nguvu akiwa "amejifunga silaha." Nyumba ya mwenye nguvu yaweza kuwa au mwili wa mtu ambamo roho huyo hukaa au eneo fulani analotawala. Vitu vyake ni roho za wanaume na wanawake aliowashikilia mateka.

Kutokana na mistari hii miwili ya maandiko, tunajifunza namna mbili muhimu kuhusu kupambana na kuyashinda mapepo ya maeneo.

1. Kwanza tunajifunza ya kuwa mapepo ya maeneo yanatolewa kwa Roho wa Mungu (Mt 12:28). Katika Luka 11:21 Yesu anaelezea Roho wa Mungu kama "mmoja mwenye nguvu zaidi" kuliko pepo ambaye ni mtu mwenye nguvu. Ni kwa njia ya nguvu za Roho tu ndipo tunaweza kuyashinda hayo mapepo yenye nguvu.
2. Tena, tunajifunza ya kwamba tunamshinda mtu mwenye nguvu kwa kuingia nyumbani mwake na "kumfunga." Tunafanya hivyo kwa kuingia katika eneo la mapepo na kuyaamuru na kuyafunga katika jina la Yesu na katika nguvu ya Roho Mtakatifu. Katika jina la Yesu tunaamuru yaachilie utawala juu ya watu yanaowashikilia mateka. Kwa njia ya nguvu ya Roho na upako, tunayanyang'anya silaha na kuyamaliza nguvu.

Kwa Njia ya Kuitangaza Injili katika Nguvu ya Roho

Njia ya tatu ya kupambana na kuyashinda mapepo ya maeneo ni kwa kuitangaza injili katika nguvu ya Roho. Kama tulivyojifunza katika Sura ya 5, kuna nguvu nyingi mno katika injili ya Kristo. Hakika ni "nguvu ya Mungu iletayo wokovu." Watu wanaposikia na kuamini injili, nguvu ya mapepo kushikilia watu huachilia. Jinsi nuru ya injili inapong'aa zaidi na zaidi katika mahali, giza linaondolewa na watu wanawekwa huru.

Maelekezo Sita Muhimu ya Kupambana Katika Vita za Kiroho Dhidi ya Mapepo ya Maeneo

Tunafunga sura hii kwa kupendekeza maelekezo matano muhimu katika kupambana vita za kiroho dhidi ya mapepo ya maeneo:

1. Uwe na uhakika ya kuwa una uhusiano mzuri na Mungu. Kabla mtu hajadiriki kupambana na Roho hawa wa giza ni lazima kwanza atambue ya kuwa ni kweli amezaliwa mara ya pili. Lazima ajue ya kuwa ana maisha mazuri ya maombi, na pia ya kuwa ana uhusiano wa karibu na Mungu. Kumbuka, tunahudumu kutokana na uhusiano na Mungu. Ni wale tu ambao kweli "wanamjua Mungu wao," watakuwa "hodari na kutenda mambo makuu." Ili kupambana na mapepo ya giza mtu ni lazima ajue hasa kumtegemea Mungu.

2. Ukiri na kuziacha dhambi zote uzijuazo. Mtu hawezi kuingia katika mapambano ya vita vya kiroho bila kuzitubia dhambi zake. Kumbuka Isaya 59:1-2:

> Tazama mkono wa Bwana haukupunguka, hata usiweze kuokoa; wala sikio lake si zito, hata lisiweze kusikia; lakini maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu, na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone, hata hataki kusikia."

Kama inawezekana, yeyote atakayepanga kufanya vita ya kiroho lazima kwanza atafute ukombozi wake binafsi kutokana na dhambi katika maisha yake mwenyewe. Dhambi yoyote au matendo ya mwili (Angalia: Gal 5:19-21) yanayoendelea kujitokeza maishani mwa mtu ni mpenyo kwa shambulizi la mapepo, na ni lazima yashughulikiwe na kuyashinda. Tafuta ukombozi na uponyaji kabla ya kuanza vita vya kiroho.

3. Jivike silaha zote za Mungu. Katika Waefeso 6:10-18 tumeambiwa "tujivike silaha zote za Mungu" kabla ya kuhusika katika vita vyovyote vya kiroho. Kusiwe na askari mjinga ambaye ataingia katika mapambano bila kwanza kujivika silaha zote za Mungu.

4. Ujazwe na Roho Mtakatifu. Tunatoa mapepo kwa njia ya Roho wa Mungu (Lk 11:20). Hivyo kabla mtu hajaingia katika mapambano ya kiroho, ni lazima kwanza abatizwe na Roho Mtakatifu. Zaidi ya hili, lazima pia atembee daima katika uwepo na nguvu za Roho.

5. Uwe tayari kudumu katika maombi hadi ujapo ushindi. Kama katika kila vita, ushindi haupatikani katika vita moja. Kama Daniel lazima tuwe tayari kuvumilia katika maombi hadi ushindi upatikane (Angalia: Dan 10:2:12).

6. Changanya maombi na mahubiri ya injili yenye upako yakifuatiwa na ishara na maajabu ya kibiblia. Hatimaye, lazima tufahamu ya kuwa wokovu na ushindi vyaweza kuja tu katika eneo lililo chini ya uonezi wa mapepo wakati maombi yakichanganywa na mahubiri ya injili katika nguvu za Roho ikifuatana na ishara na maajabu.

— Sura Ya Kumi na Mbili —

Jinsi Ya Kuomba Na Watu Ili Wajazwe Na Roho Mtakatifu

UTANGULIZI

Katika Sura ya 6, "Roho Mtakatifu na Huduma yenye Nguvu," tulizungumzia umuhimu wa kubatizwa katika Roho Mtakatifu inavyowiana na huduma yenye nguvu. Tulisema kwamba kabla mtu hajajihusisha na huduma yenye nguvu, lazima aelewe na kubatizwa katika Roho Mtakatifu. Katika sura ile ile tulizungumzia jinsi mtu anavyoweza kujazwa na Roho wa Mungu. Katika somo hili tutazungumzia jinsi ambavyo tunaweza kuwaongoza wengine katika jambo hili la muhimu la kikristo.

Katika sura hii tutaelekeza kwa vitendo "namna ya" kuomba na watu wanaohitaji kubatizwa na Roho Mtakatifu. Mwandishi ametumia njia hii ya kuombea watu kote marekani na Afrika, na binafsi ameshuhudia mamia ya watu wakijazwa na Roho.

Wengine wameuliza endapo ni vyema kuwaelekeza watu jinsi ya kujazwa na Roho Mtakatifu. Katika kitabu kiitwacho *Pneumatology* Stanley Horton anasema kuhusiana na swala hili: "Je! Unaweza kusema ni vibaya kuwapatia watu maelekezo kuhusu kumjia Kristo Mbatizaji na kumwelekezea imani zao?" Anajibu swali lake mwenyewe: "Wakristo wengi wanafikiria kuwa hakuna jambo lolote baya kuhusu kuwapatia watu maelekezo ya jinsi ya kuokoka, Kwa

nini basi tusiwasaidie watu kubatizwa?"[48] Kweli ukihitaji kuwaona watu wakijazwa na Roho katika huduma yako, itakuwa ni muhimu kwako kuwafundisha na kuhubiri juu ya somo hili mara nyingi. Kabla hatujazungumzia dondoo kuhusu jinsi ya kuomba na mtu ili ajazwe na Roho, kwanza tutashughulika na matazamio ya awali.

MATAZAMIO YA AWALI

Kabla mshauri wa kiroho hajaomba na mtu ili ajazwe na Roho yapo mambo mawili muhimu ambayo ni vizuri ayaelewe. Lazima afahamu ni nani ambaye anaweza kujazwa na Roho na pia ni nani astahiliye kuombea wengine wapate kujazwa na Roho. Lazima pia aelewe mambo manne muhimu yanayohusika katika mtu kujazwa na Roho Mtakatifu.

Ni Nani Anayeweza Kujazwa na Roho Mtakatifu?

Kabla ya yote, lazima ufahamu kuwa yeyote aliyezaliwa mara ya pili kweli anastahili na anatakiwa mara moja ajazwe na Roho. Jambo hili sio la watu fulani tu waliofikia ngazi fulani ya "utakatifu" au kukua kiroho katika maisha yao ya kikristo. Wala sio kwa ajili ya daraja fulani la watu ambao ni wa kanisa fulani au dhehebu. Ni ahadi ya wakristo wa nyakati zote (Mdo 2:17, 18; 38, 39).

Je! Ni Nani Wanaostahili Kuombea Wengine Ili Wajazwe na Roho?

Tena, mshauri wa kiroho inabidi aelewe ya kuwa yeyote ambaye yeye mwenyewe amejazwa na Roho anaweza kumuongoza mwingine katika jambo hili. Hitaji kubwa kwa ajili ya kuombea wengine wapate kujazwa na Roho ni ile shauku ya kweli ya kutaka kuona wengine wakibarikiwa na kutumika na Mungu.

Hatua Zinazohusika katika Kupokea Roho Mtakatifu

Zipo hatua nne za muhimu zinazohusika kwa mtu yeyote anayejazwa na Roho Mtakatifu: Shauku, imani, sifa na kujitoa kwa Mungu. Hebu tuangalie kwa kifupi moja ya kila hatua hizi.

1. Shauku. Tumekwisha kuzungumzia shauku au nia kuhusiana na kubatizwa

[48]Stanley M. Horton, Pneumatology, A Study Guide (Irving, TX: ICI University, 1993), kurasa 241-242.

katika Roho Mtakatifu katika Sura ya 6. Unaweza kutaka kurejea mazungumzo yale wakati huu. Biblia mara nyingi huwekea mkazo na umuhimu wa kiu au shauku katika kupokea baraka za Mungu. Wakati mmoja alipokuwa akifundisha jinsi ya kujazwa na Roho, Yesu alisema, "tafuta [yaani, "endelea kutafuta"] nawe utaona" (Lk 11:9). Kutafuta bila kuchoka ni tunda la kiu au shauku. Mungu ametuambia, "nanyi mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote (Yer 29:13). Mwelekeze mtafutaji ya kuwa lazima awe na shauku kwa moyo wake ili kujazwa na Roho Mtakatifu.

2. Imani. Imani ni jambo muhimu sana katika kupokea lolote kutoka kwa Mungu—pamoja na Roho Mtakatifu. Katika Wagalatia 3:2 Paulo anawakumbusha wakristo wa Galatia ya kuwa walimpokea Roho Mtakatifu, sio kwa matendo ya sheria, bali kwa kuyaamini yale [waliyo] yasikia." Nia moja ya mtu atakaye kuwaongoza wengine katika ubatizo wa Roho ni kujenga imani katika mioyo ya watafutaji. Tutazungumzia zaidi kuhusu hili baadaye.

3. Sifa. Katika kila wakati watu waliokuwa wanajazwa kwa Roho katika kitabu cha Matendo tunawaona wakiwa na juhudi na furaha wakimsifu Mungu. Biblia inatufundisha kuwa kabla ya siku ya Pentekoste mitume "walikuwa daima ndani ya hekalu, wakimsifu Mungu" (Lk 24:53). Biblia pia inatufundisha kwamba, "Mungu [huketi] juu ya sifa za Israeli" (Zab 22:3). Tunapomsifu Mungu anadhihirisha uwepo wake katikati yetu (2Nyak 7:1-3; Mdo 4:31). Njia nyingine ya mtu atakaye kuwasaidia wengine wajazwe na Roho ni kuwafanya wamtukuze na kumsifu Mungu kwa furaha na imani yenye matumaini.

4. Kujitoa kwa Mungu. Kujitoa kwa Mungu ni jambo jingine la muhimu katika kumpokea Roho. Mtu atakaye kujazwa na Roho ni vema aelekezwe jinsi ya kujiachilia kabisa kwa Mungu. Kujiachilia huku kuhusishe roho yake, mawazo yake na mwili wake (Rum 6:13; 12:1). Ni kwa njia hiyo ndipo Roho Mtakatifu atatawala mawazo ya mtu pamoja na viungo vyake vya sauti na kuanza kunena kwa njia yake kwa lugha nyingine.

NJIA: JINSI YA KUOMBA NA MTU ILI AJAZWE NA ROHO MTAKATIFU

Kama tulivyofanya katika sura za kuponya wagonjwa na kutoa mapepo, tutafuata njia ya hatua tatu, inayohusisha, mahojiano, maombi, na maelekezo baada ya maombi.

Hatua ya 1: Mahojiano

Katika hatua ya kwanza ya mahojiano tutajaribu kutimiza mambo manne: Kwanza tutajaribu kujenga uhusiano na mhusika. Halafu tutajaribu kumhakikishia na kujenga ujasiri wa imani. Tatu, tutajaribu kugundua hali yake ya kiroho na kumpenda Mungu. Hatimaye, tutajaribu kumueleza mhusika afanyeje ili ajazwe na Roho Mtakatifu.

1. Kujenga uhusiano. Nia ya kwanza katika hatua ya mahojiano ni kujenga uhusiano[49] na mhusika. Kama tayari unamfahamu mtu huyo, hili linakuwa halina umuhimu. Lakini endapo humfahamu kabisa mtu huyo, anza kujitambulisha mwenyewe kwake. Sema, "Ndugu, jina langu ni fulani, je! Jina lako mwenzangu ni nani?" Mwangalie machoni (kama jambo hili halina matatizo kijamii), halafu sikiliza kwa makini kwa yale atakayojibu. Rudia jina lake kwake, halafu tumia jina lake wakati wote wa kumhudumia.

2. Kumtia Moyo. Halafu, tafuta kumtia moyo[50] mtu na kumjenga imani. Unaweza kusema, "Nimefurahi sana kwamba umekuja; umefanya jambo jema." Unaweza pia kusema, "Hii yaweza kuwa siku kubwa katika maisha yako. Mungu analo jambo la muhimu na la kipekee sana kwako leo." Kumbuka, mtu huyo anaweza kuwa bado ana woga hadi muda huu. Maneno ya jinsi hii yanaweza kumsaidia kuondoa woga na kuuandaa moyo ili kupokea.

3. Uvumbuzi. Lengo moja hapa ni kutafuta ni kwa nini mtu anayehitaji kujazwa Roho amekuja mbele, na kutambua wazi yupo mahali gani kiroho. Unaweza kumuuliza maswali kama yafuatayo:

- Je! Unataka Mungu akutendee nini leo?' au "je! Umekuja ili ujazwe na Roho Mtakatifu leo?" Usichukulie tu kwamba amekuja kujazwa na Roho. Anaweza kuwa amekuja kwa sababu nyingine. Kama amekuja kujazwa, ni vema aseme mwenyewe hivyo. Kwa kusema hivyo kutamtia nguvu uamuzi wake wa kujazwa.

[49]Kujenga uhusiano na mtu ni kule kuanza joto la uhusiano wa ujirani watu wawili wakutanapo.

[50]Kumtia moyo mtu ni kutamka maneno kadhaa kwake yatakayomfanya ajisikie vizuri yeye mwenyewe au kwa yale aliyofanya.

- "Je! Umewahi kujazwa kabla?" Kama amewahi kujazwa kabla anaweza akahitaji kutiwa moyo tu ili ajazwe tena. Kama hajawahi kabisa kujazwa, anahitaji maelezo zaidi.
- "Je! Umewahi kumwona mtu yeyote akiwa amejazwa na Roho?" Kama amekwisha kuwaona wengine wakiwa wamejazwa na Roho anaweza kuwa na ufahamu ni nini kitatokea kwake. Kama hajawahi, atahitaji maelekezo ya kina.

Ukisha uliza maswali haya, sikiliza sana majibu yake. Ugunduzi huo utakusaidia jinsi ya kuendelea hatua inayofuata.

4. Maelekezo. Katika sehemu hii katika mahojiano kunakuwa na malengo mawili:

- kuhamasisha imani yenye matumaini katika moyo wa mhusika; na
- kumleta katika ufahamu kamili wa kuelewa anatakiwa afanya nini na ni nini anategemea kitokee.[51]

Njia moja ya kuinua imani ni kumkumbusha mhusika juu ya ahadi za Mungu kuhusu Roho Mtakatifu. Mhakikishie ya kuwa kama kweli amezaliwa mara ya pili Mungu yuko tayari sasa kumjaza Roho Mtakatifu. Mkumbushe ahadi ya Yesu katika Luka 11:10, "kwa kuwa kila aombaye hupokea." Lazima aamini ya kuwa Mungu anaweza, muda anapomwomba, kumjaza kwa Roho Mtakatifu. Hii ndiyo tunayoiita "imani yenye matumaini" au "imani ipokeayo." Hivyo ategemee kujazwa, na pia kunena kwa lugha kama Roho atakavyomjalia kutamka. Na awe tayari kutenda sawa na matumaini yake.

Tena, jaribu kumleta katika ufahamu halisi kuhusu afanye nini ili ajazwe, na ni nini ategemee kutokea. Anahitaji kufahamu ya kuwa kujazwa na Roho Mtakatifu sio kitu kigumu au kisicho cha kawaida kwa mkristo. Ni jambo la kawaida kufanyika. Hatajazwa na "Roho Mtakatifu mwingine" bali Roho Mtakatifu yule yule akaaye ndani yake tokea wakati wa kuzaliwa mara ya pili. Unaweza kumwambia mhusika, "Kumpokea Roho Mtakatifu ni rahisi! Ni kitu cha kawaida kufanya. Kwa mtu aliyeokoka ni rahisi kama vile kupumua." Na ni kweli! Unakumbuka Yesu alivyofanya na kuwaambia wanafunzi wake katika

[51]Mengi ya maelekezo haya yanaweza kutolewa katika mahubiri kabla ya muda wa huduma.

Yohana 20:22? "Naye akiisha kusema hayo, akawavuvia akawaambia, pokeeni Roho Mtakatifu."

Kwa maneno mengine, kupokea Roho Mtakatifu ni kama kuvuvia (kupumua). Kama kupumua kulivyo ni kitendo cha kawaida mtu kufanya, kupokea Roho Mtakatifu pia ni kitu cha kawaida kwa mwana wa Mungu. Halafu, mfanye mhusika ajue wazi ya kuwa ni kitu gani anatazamia kufanya na pia ni nini kitatokea kwake. Unaweza kusema kama hivi:

Kwanza, tutaomba pamoja. Hatafu, nitakuongoza katika sala ambayo tutamwomba Mungu atujaze kwa Roho Mtakatifu. Bwana atasikia na kujibu maombi yetu. Ninajua atajibu kwa sababu tutaomba katika mapenzi yake (1Yn 5:14). Baada ya hapo, nitakuhitaji uchukue hatua ya imani na upokee Roho Mtakatifu. Nitakuongoza katika sala nyingine fupi. Itakuwa kama hivi, "Bwana sasa hivi, katika Jina la Yesu, ninapokea Roho Mtakatifu." Ndipo nitakuomba uanze kumsifu Bwana kwa moyo wako wote. Unapofanya hivyo, tegemea Bwana kukujaza kwa Roho wake. Utahisi uwepo wake ukikujaza, na kisha utaanza kunena katika lugha ambayo hujawahi kujifunza. Usiogope, wewe uendelee tu kunena. Je! Uko tayari kujazwa na Roho? Je! Una swali lolote?

Endapo mhusika ana mawali, yajibu. Kama hana maswali endelea kumwombea.

Maombi

Katika maombi yakujazwa Roho Mtakatifu tutafanya mambo mawili:

- tutamwongoza mhusika katika maombi ya kujazwa na Roho Mtakatifu; na
- tutamwongoza mhusika katika hatua ya imani ili kupokea Roho Mtakatifu.

1. Mwongoze mhusika katika maombi. Kama ambavyo unavyoweza kumwongoza mwenye dhambi katika sala ya toba, sasa mwongoze mkristo mpya katika kuomba ili ajazwe na Roho. Sala inaweza kuendelea kama ifuatavyo, mhusika akirudia kila mstari:

> Bwana ninakuja sasa nijazwe kwa Roho Mtakatifu …Sasa hivi, hakuna lolote maishani mwangu ninalohitaji zaidi …Umeahidi ya kuwa mtu yeyote aombaye, hupokea. . . Ninaomba; kwa hiyo, nategemea kupokea …Ninapoanza kukusifu nitaachilia imani yangu … Nitaanza kuomba kwa lugha kama Roho atakavyoniwezesha …Sitaogopa.

Baada ya kuomba, mhakikishie mhusika ya kuwa Mungu amesikia maombi yake, na Mungu yuko tayari sasa kumjaza kwa Roho.

2. Mwongoze mhitaji katika hatua ya imani. Sasa mwambie mhitaji wa kujazwa Roho Mtakatifu anyanyue mikono yake yote miwili na aombe sala fupi pamoja na wewe, "Bwana sasa hivi, katika jina la Yesu, ninapokea Roho Mtakatifu." Sala hii inaruhusu muda kamili ambapo anaweza kuelekeza imani yake kwa Mungu ili kupokea Roho Mtakatifu. Sasa mtie moto ili aanze kumwabudu Mungu kwa moyo wake wote. Mara nyingi katika hatua hii mhitaji atajazwa mara moja na Roho na kuanza kunena kwa lugha kama Roho atakavyomwezesha. Kama hataanza kunena kwa lugha mara moja, mtie moyo aendelee kumsifu Bwana. Unaweza kuabudu pamoja naye, wewe pia ukimruhusu Mungu kukujaza tena kwa Roho Mtakatifu. Hii mara nyingi humtia moyo mhusika kumsifu Mungu hadi yeye pia amejazwa.

Kama mhitaji ana tatizo la kuweka mawazo yake kwa Bwana, ni vema kurudia tena hatua ya kwanza kama ilivyoonyeshwa hapo juu. Unapofanya hivyo, mwelekeze vema zaidi jinsi anavyoweza kujiachilia kwa Roho Mtakatifu. Akiisha kuanza kunena katika lugha, mtie moyo aendelee. Baki naye wakati wote anapoendelea kuomba katika Roho.

Ni vema pia nyakati nyingine kumwelekeza mhitaji ya kuwa, wakati ni muhimu atafute kipawa cha Roho, ni muhimu zaidi amtafute mtoaji wa Roho mwenyewe. Hivyo anatakiwa aweke mawazo yake kwa Yesu na sio kujawa tu na fikra za kupokea kipawa cha Roho na kunena kwa lugha kiasi kwamba anamsahau Bwana ambaye ndiye mtoaji wa vipawa hivi.

Maelekezo Baada ya Maombi

Kama ilivyo katika maombi ya wagonjwa na katika ukombozi dhidi ya mapepo, ni muhimu kwamba ushauri baada ya maombi utolewe kwa mhusika. Kama amejazwa na Roho Mtakatifu utatoa ushauri wa aina moja, endapo hajajazwa utatakiwa kumpa ushauri wa aina nyingine.

1. Kama amejazwa na Roho. Kama mhusika amejazwa na Roho na kunena kwa lugha, ushauri ufuatao ni muhimu: Mwambie ya kuwa kupokea Roho si mwisho wa mambo yote; bali ni njia ya kuendea mwisho. Kusudi la kupokea Roho ni ili kwamba tupokee nguvu kwa ajili ya maisha ya utumishi. Unaweza kusema, "Huu sio mwisho; ni mwanzo tu. Mungu sasa ataanza kukutumia katika hali mpya ya nguvu. Tegemea kuwa na nguvu mpya maishani mwako. Nenda sasa hivi ukamshuhudie mtu habari za Yesu." Unaweza kutaka kuongeza,

"Unahitaji pia kutumia muda fulani kila siku ukiomba katika Roho (yaani kuomba kwa lugha). Hii itakupatia nguvu na itakukumbusha uwepo wa Roho maishani mwako."

2. Kama hajajazwa na Roho. Kama hajajazwa na Roho, unaweza kumpa ushauri ufuatao pamoja na kumtia moyo: Mwambie asikate tamaa kwa sababu hajapokea Roho Mtakatifu wakati huo. Mhakikishie ya kwamba ahadi ya Yesu ingali ni kweli -- "Yeyote aombaye hupokea" (Lk 11:10). Mwambie aendelee kuomba atapokea, aendelee kutafuta ataona, na aendelee kubisha atafunguliwa mlango (Tafsiri ya Luka 11:9). Unaweza kumuuliza endapo anahitaji kuomba tena. Kama anataka, rudia tena kama ilivyoelekezwa hapo juu, mtie moyo atende kwa imani.

MAMBO MENGINE MUHIMU

Tunapomalizia sura hii tutataja kwa ufupi mambo mengine matatu ambayo ni muhimu tunapohitaji kuwaongoza wengine katika ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Fahamu Biblia Inasema Nini kuhusu Somo Hilo

Kwanza, endapo mtu atahitaji awasaidie wengine kujazwa na Roho Mtakatifu, ni wazi anahitaji atafute mambo yote anayoweza kuyapata juu ya somo hilo. La muhimu zaidi, lazima asome Neno la Mungu, hasa kitabu cha Matendo ya mitume, ili kuona kinasema nini kuhusu somo hili. Pia anaweza kusoma vitabu vingine vizuri kuhusu somo hilo. Jinsi mtu anavyoelewa zaidi kuhusu Roho Mtakatifu na utendaji wake katika maisha ya watu, ndivyo atakavyokuwa katika hali nzuri zaidi ya kuwasaidia wengine ili wazipokee baraka za Mungu.

Usiachilie Uvivu wa Kiroho Ukufanye Ushindwe

Jambo la pili, kama utahitaji kuwasaidia watu kupokea Roho wa Mungu, usije ukaachilia roho wa uvivu akufanye ushindwe. Kwa sababu ni vigumu mara nyingi kuombea watu wajazwe na Roho, wengine wanakwepa kuhubiri kuhusu somo hili au kuwaongoza wengine katika baraka hii kubwa. Kama jambo hili ndivyo lilivyo kwako, tubia uvivu wako wa kiroho, halafu ujitoe kwa moyo wako wote kwa ajili ya huduma hii muhimu.

Angalia Kiwango cha Ujazo Wako

Hatimaye, unapoomba na mtu ili ajazwe na Roho Mtakatifu, ni muhimu uangalie kiwango cha ujazo wako. Kwa hili nina maana uwe na ujazo wa juu unapoomba nao. Uachie ujasiri wako katika kudhamiria jambo hili kuonekana wazi! Wakati huo huo ni vema pia usiwe msukumaji mno wa mambo. Hekima itakuonyesha kiwango chema cha kutendea kazi hii na kuwatia moyo watu wajazwe na Roho.

MWISHO

Katika somo hili tumezungumzia jinsi ya kuwa hodari kuwaongoza watu katika ubatizo wa Roho Mtakatifu. Tumezungumzia mambo muhimu katika kumpokea Roho, na jinsi unavyoweza kufanya ili kuwatia moyo wengine wapokee. Tunategemea ya kuwa sasa utajitoa kwa ajili ya kazi hii ya kuwasaidia wengine wajazwe na Roho. Hakuna jambo la kuridhisha kuliko kusaidia watu katika kupokea baraka hii ya Mungu.

Appendix 1
Huduma Yauponyaji Ya Yesu

Vitabu Vitatu Vya Injili

Tendo ya Uponyaji	Mt	Mk	Lk	Njia iliyotumika
1. Mtu mwenye pepo mchafu		1:23	4:33	Kutoa pepo kwa neno.
2. Mama mkwe wa Petro	8:14	1:30	4:38	Kugusa, neno.
3. Makusanyiko	8:16	1:32	4:40	Kugusa, neno, imani
4. Mapepo mengi yatolewa		1:39		Kuhubiri, kutoa pepo
5. Mwenye ukoma	8:2	1:40	5:12	Kugusa, neno, imani ya mwenye ukoma, huruma,
6. Makusanyiko		5:15		Kuitikia uhitaji.
7. Mwenye kupooza	9:2	2:3	5:17	Neno, imani ya marafiki
8. Mtu mwenye mkono uliopooza	12:9	3:1	6:6	Neno, utii, imani.
9. Makusanyiko	12:5	3:10		Kugusa, imani, kutoa pepo.
10. Mwenye pepo wa nchi ya Wagerasi pepo.	8:28	5:1	8:26	Neno, kutoa
11. Kufufuliwa Binti Yairo	9:18	5:22	8:41	Neno, kugusa, imani ya baba yake.
12. Mwanamke aliyetokwa damu	9:20	5:25	8:43	Kugusa, kuachilia nguvu.
13. Wagonjwa wachache	13:58	6:5		kugusa, (Alizuiliwa kwa kutokuamini kwao).
14. Makusanyiko	14:34	6:55		Kugusa, kuachilia nguvu
15. Binti ya mwanamke Msirofoinike	15:22	7:24		Kuikubali imani yake
16. Kiziwi na mwenye utasi		7:37		Kugusa, neno.
17. Mtu kipofu		8:22		Kugusa, (kupona polepole).
18. Kijana mwenye roho mchafu	17:14	9:14	9:38	Neno, kugusa, imani ya baba yake.
19. Bartimayo kipofu	20:30	10:46	18:35	Neno, kugusa, huruma, imani.
20. Mtumwa wa Akida	8:5		7:2	Kuitikia kwa imani.

Appendix 1

Huduma Yauponyaji Ya Yesu

Vitabu Vitatu Vya Injili

Tendo ya Uponyaji	Mt	Mk	Lk	Njia iliyotumika
21.Vipofu wawili	9:27			Neno, kugusa.
22. Mwenye pepo, kipofu na bubu	12:22		11:14	Kutoa pepo.
23. Mtu bubu na mwenye pepo	9:33			Kutoa pepo.
24. Makusanyiko (magonjwa na udhaifu wa kila namna)	4:23		6:17	Kufundisha, kuhubiri, kuponya
25. Makusanyiko (magonjwa na udhaifu wa kila namna)	9:35			Kufundisha, kuhubiri, kuponya
26. Makusanyiko	11:4		7:21	Ushuhuda wa Yohana
27. Makusanyiko	14:14		9:11	Huruma
28. Makutano mengi (vipofu vilema na mabubu)	15:30			Imani ya marafiki
29. Makusanyiko makubwa	19:2			Haikutajwa
30. Vipofu na viwete hekaluni	21:14			Kuitikia hitaji la watu
31. Mwana wa mjane wa Naini			7:11	Neno, kugusa, huruma
32. Mariamu Magdalena na wengine			8:2	Kutoa pepo
33. Mwanamke mwenye pepo wa udhaifu			13:10	Neno, kugusa
34. Mtu mwenye ugonjwa wa Safura			14:1	Kugusa.
35. Kumi wenye ukoma			17:11	Amri.
36. Sikio la Malko			22:49	Kugusa

Injili ya Yohana

37. Mwana wa Chiwani	Yohana 4:46	Neno, imani ya baba yake.
38. Mtu aliyekuwa hawezi	Yohana 5:2	Neno, imani yake.
39. Mkutano mkuu	Yohana 6:2	Huruma
40. Mtu aliyezaliwa kipofu	Yohana 9:1	Neno, kugusa
41. Lazaro afufuliwa kutoka	Yohana 11:1	Amri Kwa wafu

Tambua: Orodha Hii Imenakiliwa Kutoka Orodha Nyingine Ya Jim B. Miller.

Appendix 2
Njia Za Uponyaji Za Yesu

Utaona katika orodha iliyotangulia njia kadha za uponyaji za Yesu pamoja na mstari wa kwanza wa Biblia, mahali na namna mbalimbali za jinsi Yesu anavyotumia njia fulani za kuombea. Huduma ya uponyaji ya Yesu ilifanyika ili pia iwe kama mfano wetu wa kufuata (Yn 20:21; 1Pet 2:21; 1Kor 11:1).

KUTAMKA NENO: Njia ambayoYesu alitumia mara nyingi katika uponyaji wa wagonjwa ilikuwa ni kwa kusema neno tu. Mara nyingine hili neno lililotamkwa ilikuwa ni amri kwa mtu aliye mgonjwa afanye tendo fulani. Wakati mwingine ilikuwa ni amri ya mapepo kutoka. Kuna wakati Yesu alitamka moja kwa moja kwa ule ugonjwa. Wakati mwingine neno lake lilikuwa ni la kuikubali imani ya mpokeaji uponyaji, au tamko la kuonyesha ya kuwa uponyaji umekwisha tendeka. Usomapo mistari ifuatayo ya matukio utamwona Yesu akitamka neno na kuponya wagonjwa:

(Mk 1:23; Lk 4:33); (Mt 8:14, Mk 1:30, Lk 4:38); (Mt 8:16; Mk 1:32, Lk 4:40); (Mt 8:2, Mk 1:40, Lk 5:12); (Mt 9:2, Mk 2:3, Lk 5:17); (Mt 12:9, Mk 3:1, Lk 6:6); (Mt 8:28, Mk 5:1, Lk 8:26); (Mt 9:18, Lk 9:38); (Mt 20:30, Mk 10:46, Lk 18:35); (Mt 9:27); (Lk 7:11); (Lk 13:10); (Lk 17:11); (Yn 4:46); (Yn 5:2); (Yn 9:1); (Jn 11:1).

AMRI YA IMANI: Njia mojawapo ambayo Yesu aliitumia mara kwa mara kuponya wagonjwa ilikuwa amri ya imani kama ilivyotajwa hapo juu. Aliweza kuamuru ugonjwa upone, mapepo yatoke na wagonjwa kuitika kwa tendo la imani. Hapa ipo mifano kwa ajili yako ili uisome:

(Mt 8:14, Mk 1:30, Lk 4:38); (Mt 9:2, Mk 2:3, Lk 5:17); (Mt 12:9, Mt 3:1, Lk 6:6); (Mt 9:18, Mk 5:22, Lk 8:41); (Mk 7:32); (Mt 20:30, Mk 10:46, Lk 18:35); (Mt 9:27); (Lk 7:11): (Lk 13:10); (Lk 7:11); (Yn 4:46); (Jn 5:2); (Yn 9:1); (Yn 11:1).

KUGUSA: Yesu mara nyingi aliwagusa watu na kuwaponya. Kugusa huku kulikuwa ni kuuchukua mkono wa mtu, kumgusa mgonjwa mahali alipohitaji uponyaji utendeke, na namna zingine za miguso. Soma mistari ifuatayo ili kuona jinsi Yesu alivyotumia kugusa katika kuponya wagonjwa:

(Mt 8:14, Mk 1:30, Lk 4:38); (Mt 8:16, Mk 1:32, Lk 4:40); (Mt 8:2, Mk 1:40; Lk 5:12); (Mt 9:18; Mk 5:22, Lk 8:41); (Mt 13:58, Mk 6:5); (Mk 7:32); (Mk 8:22); (Mt 17:14), (Mk 9:14, Lk 9:38); (Mt 20:30; Mk 10:46, Lk 18:35); (Mt 9:27); Lk 13:10); (Lk 14:1); (Lk 22:49); (Yn 9:1).

Appendix 2
Njia Za Uponyaji Za Yesu

IMANI YA MPOKEAJI: Yesu mara nyingine aliponya alipoona imani ya mtu inahitaji uponyaji. Hapa ipo kati ya mifano:

(Mt 8:2, Mk 1:40, Lk 5:12); (Mt 12:15, Mk 3:10); (Mt 9:20, Mk 5:25, Lk 8:43); (Mt 20:30, Mk 10:46, Lk 18:35); (Mt 9:27); (Yn 5:2).

IMANI YA WENGINE: Nyakati nyingine Yesu aliponya alipoona imani ya marafiki au familia ya mtu aliyehitaji uponyaji:

(Mt 8:14, Mk 1:30, Lk 4:38); (Mt 8:16, Mk 1:32, Lk 4:40); (Mt 9:2, Mk 2:3, Lk 5:17); Mt 9:18, Mk 5:22, Lk 8:41); (Mt 14:34, Mk 6:55); (Mt 15:22, Mk 7:24); (Mk 7:32); (Mk 8:22); (Mt 7:14, Mk 9:14, Lk 9:38); Mt 8:5, Lk 7:2); (Yn 4:46).

KUTOA MAPEPO: Mara nyingi Yesu aliwaponya wagonjwa kwa kutoa mapepo ambayo yalisababisha ugonjwa:

(Mk 1:23, Lk 4:33); (Mt 12:15, Mk 3:10); (Mt 8:28, Mk 5:1, Lk 8:26); (Mt 9:32); (Mt 12:22, Lk 11:14); (Lk 8:2); (Lk 13:32).

HURUMA: Huruma kwa ajili ya wagonjwa na wenye mateso kilikuwa ni kiungo kilichopatikana katika huduma ya uponyaji ya Yesu. Huruma yake ilimfanya awafikie na kuwaponya kama ifuatavyo:

(Mt 8:2, Mk 1:40, Lk 5:12); (Mt 20:30, Mk 10:46, Lk 18:35); (Mt 14:14, Lk 9:11, Yn 6:2); (Lk 7:11).

UTHIBITISHO WA KUHUBIRI AU KUFUNDISHA: Uponyaji mara nyingi ulifanyika ili kuthibitisha ujumbe aliofundisha au kuhubiri, kama mistari ifuatayo inavyothibitisha:

(Mk 1:39); (Mt 4:25, Lk 6:17); (Mt 9:35); (Mt 11:4, Lk 7:21).

MATENDO YA AJABU: Wakati mwingine Yesu aliponya kwa kutumia matendo ya ajabu kama ifuatavyo:

(Mt 9:20, Mk 5:25, Lk 8:43); (Mt 14:34, Mk 6:55), (Mk 8:22); (Yn 9:1).

Tambua: Orodha hii imenakiliwa kutoka orodha nyingine iliyotengenezwa na Jim B. Miller.

Bibliography

Bennett, Dennis and Rita Bennett. 1971. *The Holy Spirit and You*. Plainfield, NJ: Logos`International.

Bonnke, Reinhard. 1994. *Mighty Manifestations*. Eastbourne, UK: Kingsway Publication.

Bosworth, F. F. 1973. *Christ the Healer*. Old Tappan, NJ: Revell.

Carter, Howard. 1968. *Spiritual Gifts and Their Operation*. Springfield, MO: Gospel Publishing House.

Duewel, Wesley. 1986. *Touch the World Through Prayer*. Grand Rapids, MI: Zondervan.

Evans, W.I. 1954. *This River Must Flow*. Springfield, MO: Gospel Publishing House.

Exley, Richard. 1988. *Perils of Power: Immorality in the Ministry.* Tulsa, OK: Honor Books.

Fitzpatrick, Graham. 1987. *Miracles, Faith, and God's Will*. N.S.W., Australia: Spiritual Growth Publications.

Gramenz, Stuart. 1986. *How You Can Heal the Sick*. Chichester, UK: Sovereign World.

Haltom, Fred. 1989. "Old Testament power encounters." in *Power Encounter, A Pentecostal Perspective,* ed. Opal Reddin, 94–122. Springfield, MO: Central Bible College.

Horton, Stanley M. 1993. *Pneumatology*. Irving, TX: ICI University.

———. 1976. *What the Bible Says About the Holy Spirit*. Springfield, MO: Gospel Publishing House.

Jeter, Hugh. 1977. *By His Stripes*. Springfield, MO: Gospel Publishing House.

Kuzmic, Peter. 1988. "Kingdom of God." In *Dictionary of Pentecostal and Charismatic Movements,* ed. Stanley Burgess, Gary McGhee, and Patrick Alexander, 521–526. Grand Rapids, MI: Zondervan.

Ladd, George Eldon. 1981. "The Gospel of the Kingdom." In *Perspectives on the World Christian Movement, A Reader*, ed. Ralph D. Winter and Steven C. Hawthorne, 51–69. Pasadena, CA: William Carey Library.

Marshall, Tom. 1988. *Foundations for a Healing Ministry*. West Sussex, England: Sovereign World.

Miller, Jim. n.d. "How to Heal the Sick." Unpublished manuscript (available through the author).

Moon, Jessie K. 1989. "Power Encounter in Evangelism." In *Power Encounter, A Pentecostal Perspective,* ed. Opal Reddin, 232–255. Springfield, MO: Central Bible College.

O'Donovan, Jr., William. 1992. *Introduction to Biblical Christianity From An African Perspective*. Ilorin, Nigeria: Nigeria Evangelical Fellowship.

Osborn, T. L. 1955. *How to Receive Miracle Healing*. Nairobi: Evangel Publishing House.

Otis Jr., George. 1991. *The Last of the Giants*. Tarrytown, NY: Chosen Books.

Pennoyer, F. Douglas. 1990. "Dungeons of Collective Captivity." In *Wrestling with Dark Angels,* ed. C. Peter Wagner and F. Douglas Pennoyer, 249–279. Ventura, CA: Regal.

Pyches, David. 1985. *Spiritual Gifts in the Local Church.* Minneapolis: Bethany House Publishers.

Stamps, Don. 1992. “Acts 4:8, Peter Filled with the Holy Spirit.” In *The Full Life Study Bible,* 1651. Grand Rapids, MI: Zondervan Publishers.

———. 1992. “Baptism in the Holy Spirit.” In *The Full Life Study Bible,* 1642–1643. Grand Rapids, MI: Zondervan Publishers.

———. 1992. “Power over Satan and Demons.” In *The Full Life Study Bible,* 1484–1485. Grand Rapids, MI: Zondervan Publishers.

Summerall, Lester. 1979. *Demons, the Answer Book*. South Bend, IN: LeSEA Publishing.

Unger, Merril C. 1971. *Biblical Demonology*. Wheaton, IL: Scripture Press.

Wagner, C. Peter. 1990. “Territorial Spirits.” In *Wrestling with dark angels,* ed. C. Peter Wagner and F. Douglas Pennoyer, 73–91. Ventura, CA: Regal.

Williams, Don. 1989. *Signs, Wonders, and the Kingdom of God*. Ann Arbor, MI: Servant Publications.

Wimber, John. 1986. *Power Evangelism.* San Francisco: Harper and Row.

_____. 1987. *Power Healing*. San Francisco: Harper & Row.

Huduma Yenye Nguvu

Katika kanisa leo kuna kuongezeka kwa shauku ya kutaka kufahamu zaidi kuhusu huduma yenye nguvu. Viongozi wa kanisa pamoja na wakristo wa kweli dunia nzima wameanza kutambua kwamba endapo kanisa litahitaji kutimiza Agizo kuu la Kristo, na kuufikia ulimwengu kwa injili katika kizazi hiki, lazima kanisa lijifunze tena siri ya jinsi ya kutumika katika nguvu ya upako wa Roho Mtakatifu.

Mafanikio makubwa ya kanisa la Agano Jipya tunayoyasoma katika Biblia ni wazi yalitokea kwa sababu kanisa lilihudumu katika nguvu za miujiza - na ishara zilizofuatana. Leo kanisa linaamka likipata ufahamu wa kuwa, njia za huduma ya Yesu na kanisa la kiumitume ndizo njia bora kabisa. Viongozi wengi zaidi wa kanisa wanauliza swali, "Je! Tunawezaje kuwa na nguvu zile zile na mafanikio katika huduma zetu leo?"

Kitabu hiki kimeandikwa ili kujibu swali hilo. Kimeandikwa kama kitabu cha utendaji, "Jinsi ya" maelekezo ya huduma yenye nguvu. Kinazungumzia mambomuhimu matatu kuhusu huduma yenya nguvu:

- Kuitambua Huduma yenye Nguvu
- Matayarisho ya Huduma yenye Nguvu
- "Jinsi ya" kuifanya Huduma yenye Nguvu

Kitabu hiki kimetolewa ili kukusaidia ujifunze na kuyatendea kazi masomo haya muhimu katika huduma yako.

Kuhusu Mwandishi

Denzil R. Miller ni Mmisionari wa kanisa la Assemblies of God katika Afrika. Kwa sasa anaishi katika nchi ya Malawi, ambako ni mkufunzi katika chuo cha Theologia cha Assemblies of God katika mji mkuu wa Lilongwe. Mchungaji Miller pia anaendesha makongamano ya Roho Mtakatifu na Huduma yenye nguvu katika Afrika nzima. Anaweza kufikiwa kwa kumwandikia, Springfield, MO, USA.

Acts in Africa Initiative